Nipashe
Jumatatu Oktoba 31, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581115
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13

JACKPOT BABA LAO!
TZS. 374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Waomba** dua kupinga kampuni ya nje kupewa zabuni uwanja wa ndege Zenj

UKURASA 2

BAA LA UKAME

# Hivi ndivyo ilivyo hali ya wananchi

• **Watumia** maji yenye tope, waweka majivu, serikali yagawa ndoo moja kwa kaya kila siku... *Endelea ukurasa 4*



Wananchi wa Kijiji cha Nanja wilayani Monduli mkoani Arusha wakichota maji katika mashimo waliyochimba. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

## Samia aanika fursa lukuki uwanja ndege mpya

UKURASA 2

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (wa pili kulia), akifurahia jambo baada ya kuzindua kampeni ya NMB Mastabata – Kote-kote mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. Wa pili kushoto ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, (kulia) ni Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu, Emmanuel Akonaay na Mkuu wa Idara ya Kadi, Philbert Casmir. **Habari Uk.21. PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## Askofu Shoo: Taasisi za dini zisigeuzwe kuwa NGO

UKURASA 3

MICHEZO TANZANIA YATWAA TAJI MISS VIZIWI 2022 UK.31 KABWELA UK.7

# Samia aanika fursa luluki uwanja mpya wa ndege

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja faida tano za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato ikiwamo kuchochea ukuaji wa uchumi na kutoa ajira kwa Watanzania.

Aliagiza pia kazi zinazofaa kufanywa na Watanzania wapewe huku akionya udokozi wa vifaa vya ujenzi.

Akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa awamu ya kwanza wa uwanja huo jana jijini hapo, Rais Samia alisema mradi huo ulipangwa kukamilika mwaka 2025 na kwamba makandarasi wakisimamiwa utakamilika Desemba mwaka 2024 na utakuza sekta ya kilimo na biashara.

"Ujenzi huu wa viwanja vya ndege na miradi mingine ya barabara, bandari na meli ni lengo ni kukuza ushindani wa biashara ukanda wa Afrika Mashariki na duniani, kukuza utengamano wa kikanda kwa nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki, kukuza soko la bidhaa zetu," alisema.

Alisema usafiri ukiimarika kwenye makao makuu ya nchi Dodoma ni kichocheo cha maendeleo nchini.

Samia alisema mradi huo ni wa kitaifa na kuwaomba kutohujumu ujenzi kwa kudokoa mifuko ya saruji, misumari, nondo.

"Kiwanja kinajengwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya Shirika la Anga Duniani, uwezo wake utafanya kiwe na uwezo wa kutua na kuruka ndege za dream liner na airbus, na ndege za kimataifa," alisema.

Alisema usafiri wa anga umepewa kipaumbele katika sera ya usafiri ya mwaka 2003 ambao kila mkoa unatakiwa kuwa na kiwanja chenye uwezo wa kuhudumia ndege zinazobeba abiria si chini 179.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema ujenzi wa uwanja huo wa kimataifa utakamilika muda uliopangwa mwaka 2024.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Rogatus Mativila, alisema eneo hilo lina ukubwa wa hekta 4500 na Sh. bilioni 15.20 zimetumika kulipa fidia wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya mradi.

Alisema mwaka 2015 serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka AfDB kwa ajili ya marejeo ya upembuzi yakinifu na usanifu kwa kina na mwaka 2017 serikali kupitia TAA iliingia mkataba na kampuni ya kihandisi ya nchini Tunisia kwa kampuni ya Tanzania kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 1.885 kazi iliyokamilika mwaka 2019.

"Kiwanja hiki lengo kijengwe kiwe na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 32 kwa mwaka, kiwango ambacho kitafikiwa baada ya miaka 100."

Alisema mpango mkakati wa kiwanja unaonesha kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa kama airbus 380 yenye uwezo wa kubeba abiria 500.

Alieleza kuwa jengo la abiria la kuhudumia abiria milioni 1.5 kwa mwaka na litaongezwa kulingana na mahitaji pia kuwa na jengo la Rais na watu mashuhuri.

Alisema ujenzi huo utafanyika kwa awamu na kitajengwa kwa kiwango cha daraja la 4E na kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa aina ya Boeing 787 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 350.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) alisema mpaka Machi 2021 Tanzania ilikuwa na viwanja vya ndege 435, serikali ikimiliki viwanja 194 na sekta binafsi ni 241.

Alisema serikali inatarajia kukarabati mradi mkubwa wa jengo la pili la abiria (Terminal II) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambao unatarajia kuanza Juni, 2023 ikiwa ni matunda ya ziara ya Rais Samia aliyoifanya mapema mwaka huu nchini Ufaransa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema jumla ya wakazi wa Dodoma 3,368 wamelipwa fidia ya Sh. bilioni 16.93 kupisha ujenzi huo ambapo wananchi 10 wanaodai fidia ya Sh. milioni 80 wameshapelekwa maombi Hazina.

Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dk.Patricia Laverley, alisema ujenzi wa kiwanja hicho umefadhiliwa na benki yake kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 271 ambao utachukua miaka mitatu.



Nahodha wa meli ya kivita ya India ambayo imetia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam, Nitesh Garg (kushoto), akiwa na Kapteni Ally Juma Lubh'ambo, ambaye ni Ofisa wa Jeshi la Wanamaji (wa pili kushoto), Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan na Ofisa wa INS Tarkash, Kapteni Abraham Samuel (kulia) baada ya kufanya mazoezi ya pamoja na Jeshi la Wanamaji nchini. **Habari Uk. 7 PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto: Kama hauko huru chama chako, njoo kwetu

**Na Jenifer Gilla**

KIONGOZI wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, amewataka wanachama wa vyama mbalimbali vya kisiasa nchini ambao hawapati nafasi ya kufanya kazi walizokusudia katika vyama vyao, kujiunga na chama hicho ili wawe huru kutimiza haja zao.

Hata hivyo, ametoa angalizo kuwa chama hicho kinataka viongozi wanaowajibika kujenga chama na kuwataka waliopo kuongeza juhudi katika ujenzi wa chama kwa kuwa hawatawavumilia viongozi wavivu.

Zitto aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa ofisi mpya za makao makuu ya chama hicho Magomeni mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wageni kutoka vyama mbalimbali vya siasa nchini na nchi za nje ikiwamo Zambia na Zimbabwe na wawakilishi kutoka taasisi na mashirika mbalimbali.

"Hii ni nchi ya kidemokrasia inayotoa uhuru kwa kila mtu kujiunga na chama cha siasa, kinachoweza kufanikisha malengo yake. Ewe mwanasiasa ambaye unataka kufanya siasa lakini chama chako hakikupi nafasi ya kufanya hivyo, njoo ACT-Wazalendo tufanye siasa," alisema.

Zitto alisema chama hicho kinaamini shabaha kuu ya chama chochote cha siasa inapaswa kuwa kuunda sera zitakazowezesha kuondoa shida zinazowakabili wananchi, hivyo kunahitajika viongozi wenye muda wa kutulia na kufikiria.Alisema ujenzi wa jengo hilo ni sehemu ya mipango mingi waliyonayo katika ujenzi wa chama hicho ikiwamo kufanya mabadiliko makubwa katika kila eneo, ikiwamo uongozi na sera.

"Tulianza mapema mwaka huu kwa kuzindua mfumo wa kuandikisha wanachama wetu kidigitali tuliouita ACT Kiganjani.

"Hivi sasa maelfu ya wanachama wetu wanajisajili katika mfumo huo na tunaendelea na kampeni maalum za kuhakikisha kuwa kila mwanachama wetu anasajiliwa katika mfumo wa ACT Kiganjani," alisema.

Zitto pia alisema chama hicho kilizindua Baraza Kivuli la Mawaziri kama Idara Maalum ya Chama ya Wasemaji wa Kisekta, asilimia 52 wakiwa ni wanawake na 45 ni vijana wenye umri chini ya miaka 35.

Kiongozi huyo alisema ofisi hiyo mpya ina hadhi ya chama cha siasa chenye ndoto ya kushika dola na kuongoza serikali, kila siku kikipaza sauti kuibua masuala ya wananchi.

# Waomba dua kupinga ZAA kuteua kampuni ya nje kutoa huduma AAKIA

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAUMINI wa Dini ya Kiislamu zaidi ya 200 katika Kijiji cha Vitongoji, Mkoa Kusini Pemba wamesoma dua maalum kuomba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) isiteue Kampuni ya DNATA kutoka Dubai kuwa mtoa huduma pekee katika jengo la tatu la (Terminal III) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA).

Waumini hao walianza kusoma dua muda mfupi baada ya kumalizika ibada ya Ijumaa katika Msikiti wa Abuu Hanifa, wakiongozwa na Shekhe Abdalla Ali Khamis.

Shekhe Khamis alisema wamepokea kwa masikitiko taarifa ya kuwapo kwa hatari ya wafanyakazi takriban 600 kupoteza ajira kutokana na ZAA kuteua kampuni ya DNATA kuwa mtoa huduma pekee kuanzia Desemba mosi, mwaka huu.

"Katika hali kama hii tunainua mikono yetu juu kumuomba Mwenyezi Mungu awaepushie wenzetu na mtihani wa kupoteza ajira. Badala yake awaongezee neema na baraka na uweza wake ili awalindie ajira zao wasiadhirike na familia zao," alisema Shekh Khamis.

Shekhe Othman Mohammed, kwa upande wake alisema wakati umefika kwa serikali kuchukua hatua za kushughulikia mgogoro uliojitokeza kati ya kampuni za kutoa huduma za Uwanja wa Ndege Zanzibar na ZAA kwa maslahi ya Zanzibar na wananchi wake. Alisema Kampuni ya ZATI na Kampuni ya TRas Word kwa miaka mingi zimekuwa zikitoa huduma katika viwanja vya ndege Zanzibar na hakukuwa na malalamiko yoyote toka kwa abiria au kampuni za ndege zikiwamo za kimataifa.


Akihutubia baada ya sala ya Ijumaa katika msikiti huo mwanaharakati wa haki za binadamu na utawala bora, Ali Makame Issa, alisema wameshtushwa na taarifa za watu 600 kutaka kupoteza ajira Zanzibar.

Aliwaambia waumini hao kuwa kampuni ya DNATA inayomilikiwa na Mfalme wa Dubai imeteuliwa kutoa huduma pekee katika jengo la tatu la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume bila ya kutangazwa zabuni kinyume na sheria ya ushindani ya Zanzibar.

Issa alisema pamoja na wanasiasa kujitokeza kulaani kitendo kilichofanywa na ZAA akiwamo Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jussa ZAA, imeendelea kusisitiza DNATA itaanza kutoa huduma kuanzia Desemba mosi, mwaka huu. Hata hivyo, Jumuiya ya watoa huduma Viwanja vya Ndege Tanzania (TAOA) tayari imetoa indari ya siku saba kwa Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA), kusitisha uamuzi wa ZAA wa kuiteua Kampuni ya DNATA kuwa mtoa huduma pekee katika jengo hilo.

Kwa mujibu wa madai TAOA, iwapo TCAA itashindwa kuchukua hatua watalazimika kufikishwa mahakamani kwa kushindwa kusimamia Sheria ya Mamlaka ya Anga Tanzania.

Alipoulizwa Mkurugenzi wa TCAA, Hamza Johari, alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kwa vile sasa lipo kwa Waziri wa Mawasiliano na Uchunguzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




Waziri wa Habari, Nape Nnauye, akipokea mfano wa hundi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, katika kongamano la sita la TEHAMA Zanzibar mwishoni mwa wiki. **Habari Uk. 5. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi ashindwa kuthibitisha madai ya tuhuma uchunguzi ndani ya NHC

**Na Mwandishi Wetu**

SHAHIDI wa pili wa utetezi, Bernard James katika kesi ya madai ya kuchafuliwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, ameshindwa kuonyesha na kuthibitisha mahakamani nyaraka alizodai kuwa aliziona kupitia vyombo vya uchunguzi.

James ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mahakama na Masuala ya Uhalifu wa Gazeti la The Citizen, alishindwa kufanya hivyo alipotakiwa kuonyesha nyaraka hizo iwapo ziko mahakamani baada ya kuhojiwa na Wakili wa Mchechu, Aliko Mwamanenge wakati akitoa ushahidi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Katika kesi hiyo, Mchechu anaomba mahakama iamuru The Citizen kumlipa Sh. bilioni tatu kwa madai ya kumchafua kupitia gazeti lake toleo la Machi 18, 2018 kwamba Magufuli alimfukuza kazi. Sambamba na hilo, alishindwa kuthibitisha kuwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, alimfukuza Mchechu kama gazeti hilo lilivyoandika kupitia habari yenye kichwa 'How JPM dissolved NHC board, sacked Mchechu'. Maana ya kichwa hicho ni namna JPM (Magufuli) alivyoivunja bodi ya NHC, kumfukuza Mchechu.

Alipohojiwa na Wakili Mwananenge kama kuna sehemu yoyote iliyoeleza kuwa Magufuli alimfukuza Mchechu, shahidi huyo alidai kuwa hakuna sehemu yoyote isipokuwa alimwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi pamoja na vyombo vya kiuchunguzi kufuatilia tuhuma ndani ya NHC, Mchechu akiwamo.

Kuhusu tuhuma za Mchechu kuwa na kampuni inayofanya kazi kama za NHC, hivyo kuwa na mgongano wa kimaslahi, James alidai kuwa walizipata kupitia habari za ndani za kiuchunguzi ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Shahidi huyo alidai kuwa katika kufuatilia habari hizo, alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU (hakumtaja jina) na kwamba uchunguzi ulikuwa kwenye mchakato. Hata hivyo, alipoulizwa kama taarifa hizo ziliwasilishwa kama moja ya vielelezo mahakamani, alidai kuwa hakuzipata kutoka katika chombo hicho.

"Tuliwasiliana na Mkuu wa TAKUKURU na kufanya naye mazungumzo na alitueleza yote hayo lakini hakutupatia kimaandishi kwa sababu walikuwa kwenye mchakato. Pia baadhi ya wajumbe wa bodi waliokuwa wakichunguza walituthibitishia kuwa tuhuma hizo ni za kweli kwa sababu walishamaliza uchunguzi wao," alidai shahidi huyo ndipo Wakili Mwananenge alipomtaka atoe uthibitisho mahakamani na kudai hana vielelezo.

Shahidi huyo pia alidai hivyo alipohojiwa na Jaji Leila Mgonya anayesikiliza shauri hilo na kuongeza kuwa baadhi ya watu wa ndani ya Bodi ya NHC, walimpatia nyaraka zinazoonyesha tuhuma hizo ni za kweli lakini hana na hakuziwasilisha mahakamani.

Alipoulizwa kama hawakuona kuna umuhimu wa mtu kupewa nafasi na kusikilizwa kabla ya kuchapishwa habari hizo, shahidi huyo alidai alimtafuta Mchechu kwa zaidi ya mwezi kupitia simu yake lakini hakupokea na baada ya hapo alimwandikia maswali 10 kupitia mtandao wa WhatsApp na hakujibu.

Baada ya kujibu hivyo, Wakili Mwamanenge alimuuliza shahidi huyo kama anayo maswali hayo na aliyawasilisha mahakamani katika maelezo yake, alidai kuwa hana na kwamba maswali hayo yalifutika kwenye simu yake kwa kuwa ni muda mrefu.

"Pamoja na kwamba unadai ulimtafuta na hakukupa ushirikiano. Je, kuna sehemu yoyote uliandika kuwa mlifanya juhudi za kumtafuta na hakupatikana au kuwajibu chochote?" Alihoji Mwamanenge kisha shahidi huyo kudai kuwa hawakufanya hivyo.

Kuhusu neno 'sacked', James alidai kuwa walikuwa na maana kwamba ameondolewa kwenye nafasi yake kupisha uchaguzi au mtu huyo ametolewa na hawezi kurejea tena katika nafasi hiyo.

Kutokana na jibu hilo, shahidi huyo aliulizwa 'mbona Mchechu amerudi kwenye nafasi hiyo na kwanini hawakuandika sababu za kurudi kwake?' Shahidi huyo akidai kwamba anaamini tuhuma zilizomwondoa bado sahihi na kwamba amerudishwa kwa sababu ya mabadiliko ya utawala wa nchi. Alidai kuwa Rais Samia Suluhu Hassan hakumrudisha Mchechu kwenye nafasi hiyo bali alimteua.

Awali, akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Ambrose Nkwera, James alidai kuwa habari kuhusu Mchechu kufukuzwa, pia zilitokana na alichosema Rais (Hayati) Magufuli wakati wa uzinduzi wa mradi wa nyumba Dodoma.

Alidai kuwa Magufuli katika hafla hiyo alisema kuna ubadhirifu ndani ya NHC na kwamba Mchechu anamiliki kampuni inayofanya kazi kama za shirika hilo, jambo ambalo lina mgongano wa kimaslahi.

Ushahidi kwa upande wa utetezi katika kesi hiyo umemalizika na mawakili wa pande mbili wametakiwa kuwasilisha hoja za maandishi ifikapo Novemba 14 mwaka huu. Jaji Mgonya anatarajia kutaja tarehe ya uamuzi Novemba 17, mwaka huu.

# Askofu Dk. Shoo: Taasisi za dini zisigeuzwe kuwa NGO

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, alisema wanasiasa wameanza kujaribiwa kwa kuichukulia dini kama taasisi isiyo ya kiserikali na kuichukulia kama shirika lisilo la kiserikali (NGO), kitu ambacho sio sahihi.

"Ninawaombeni msijaribiwe kwa kuifanya dini iwe kama NGO, kanisa libaki kuwa kanisa, dini ina nafasi yake katika jamii," Askofu Shoo alisema jana mkoani hapo wakati wa kusimikwa kazini, Askofu Mteule wa KKKT Dayosisi ya Kati, Dk. Syprian Hilinti.

Mkuu wa Kanisa huyo alibainisha kuwa anayasema hayo kwa kuwa kuna sheria alizodai zinaelekea kutungwa ambazo zinataka kuweka dini katika kapu moja na mashirika yasiyo ya kiserikali, akitaka serikali iliangalie vizuri jambo hilo.

Pia aliitaka serikali kushughulia tatizo la uhaba wa maji na umeme ambalo limeyakumba maeneo mengi nchini kwa kuwa wananchi wanapata tabu.

"Tumeona siku za hivi karibuni kuna changamoto ya umeme na maji, tunaomba serikali iweke nguvu katika kumaliza tatizo hili maana nyakati hizi bila umeme na maji ya uhakika, kuzungumzia maisha bora inakuwa jambo gumu sana," alisema.

Alisema maeneo mengi ya ukanda wa kaskazini mwa nchi yamekubwa na ukame ambapo wananchi wanapata tabu kutafuta huduma ya maji.

Askofu Mteule wa KKKT Dayosisi ya Kati, Dk. Hilinti aliingizwa rasmi kazini kuwa askofu wa tano wa dayosisi hiyo huku akihoji matumizi ya tozo na kodi wanazokatwa wananchi.

Dk. Hilinti alisema kodi na tozo zote zikishakatwa, zinapaswa kuleta mrejesho chanya na nafuu kwenye maisha, uchumi na upatikanaji wa huduma bora katika jamii kama afya, maji, umeme, elimu na barabara.

Alisema makato ya kodi na tozo yasiondolewe lakini yafanywe kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya leo.

"Suala la kodi na tozo zote kwa ujumla hatusemi ziondolewe maana hata nchi za wenzetu Ulaya na Amerika ukiuza nyanya, unatozwa kodi. Hata ukifanya kibarua cha siku, unatozwa kodi," alisema.

Askofu Dk. Hilinti alisema jambo la msingi ni kodi na tozo zote zinapokatwa ziangalie uwiano na hali ya kipato na maisha ya watu na sio mtu anamtumia mama yake Sh. 10,000, anakatwa Sh. 6,000.

Askofu Dk. Hilinti aliwaomba wanadayosisi waliopo ndani na nje ya nchi kuhakikisha mambo ya ugomvi, wizi, uchoyo, ukanda, ukabila, unafiki, uongo, wivu, uvivu, kijicho, vijembe na viwiko yasizungumzwe kwenye kanisa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kanisa la KKKT na itaendelea kushirikiana na dini zote.

> **"Tumeona siku za hivi karibuni kuna changamoto ya umeme na maji, tunaomba serikali iweke nguvu katika kumaliza tatizo hili maana nyakati hizi bila umeme na maji ya uhakika, kuzungumzia maisha bora inakuwa jambo gumu sana,"**

**IN THE DISTRICT COURT OF NACHINGWEA**
**AT NACHINGWEA**
**MATRIMONIAL CAUSE NO 05 OF 2022**
**BETWEEN**
**DAINES SANDI MAKOTHA............**
**PETITIONER**
**VERSUS**
**MADUHU SAMSON MAONGO... RESPONDENT**
**TO : MADUHU SAMSON MAONGO**
**P.O.BOX NACHINGWEA**

WHERE the above matrimonial cause is set down for mention on 28 day of November 2022 at 9:00 o'clock in the morning soon. Thereafter, you are hereby to enter appearance the cause/ Appeal/Application/Petition may be heard ex- parte or dismissed.
A copy of application attached herewith.
Given Under my hand and the seal of the court this 26 day of October, 2022

..........................................................
**Resident Magistrate**
**NACHINGWEA**

**KUPOTELEWA NA HATI YA MAUZIANO**

KUPOTELEWA NA HATI YA MAUZIANO KATI YA **CALVIN E. LEMA NA OMARI SAID HASHIM.**
**CALVIN E. LEMA WA S.L.P 106285 DAR ES SALAAM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA MAUZIANO YA ENEO LA SHAMBA ILIOTOLEWA NA **SERIKALI YA MTAA WA MBEZI JUU (JOGOO) TAR: 14/12/2004** KATIKA WILAYA YA KINONDONI. TAHADHARI HATI HII SIYO HALALI KWA MATUMIZI, KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFAKITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0754335165/0715335165.**
POLISI CONTROL NAMBA: **9910833417884**

## BAA LA UKAME

# Hivi ndivyo ilivyo hali wakazi Monduli

**Na Elizabeth Zaya aliyekuwa Monduli**

NI majira ya saa nne asubuhi, wanaonekana wenyeji wa Kijiji cha Nanja wilayani Monduli mkoani Arusha wakichimba mashimo pembeni mwa bwawa ambalo maji yake yamekauka na kubaki tope.

Mahali hapo ni umbali wa Km 37 kusini magharibi mwa Mji wa Monduli na safari yake kwa gari kutoka mjini inachukua takriban nusu saa.

Unapofika kijijini Nanja kwa sasa, mara moja unashuhudia hali ya ukame iliyosababisha mifugo mingi kuhamishwa eneo hilo na kupelekwa maeneo yenye malisho, huku wakazi waliobaki wakikabiliwa na uhaba wa maji.

Kinachoshuhudiwa na Nipashe mahali hapo, wenyeji wamechimba mashimo pembeni mwa bwawa hilo lililobakiwa na tope badala ya maji huku wakiweka miti yenye miiba, wenyewe wakiita masanzu, ili kuzuia mifugo michache iliyobaki kijijini huko kuingia na kuharibu ubunifu wao huo wa kupata maji.

"Tunahangaika sisi, tunakunywa tope, sio maji, tunapochota tunajaribu kuweka majivu kisha tunafunika kwa mfuniko ili yajichuje, tope lishuke chini ili yafae kwa matumizi lakini sasa hayafaa tena. Tope limekuwa zito kupita kiasi, hatuna namna, tunatumia hivyo hivyo," Naomi Stephano, mkazi wa Kijiji cha Nanja anasimulia kero inayowasibu.

Naomi, mama wa familia ya watu wanane, anasema kwa miezi mitatu sasa eneo hilo limekumbwa na ukame unaosababisha kuwe na ugumu katika kupata huduma ya maji kwa kuwa wengi wao walikuwa wanategemea mabwawa kupata huduma hiyo.

Mama huyo anaendelea kuwasilisha kilio chao, akitamka: "Ninatamani sauti yangu hii isikike hadi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, aje atusaidie sisi kinamama wenzake tunavyohangaika huku na watoto, atusaidie tupate maji ya kudumu na sio haya mabwawa, yanatutesa sana.

"Miaka yote tumekuwa tukitegemea maji haya ya mabwawa ambayo tutumia sisi binadamu pamoja wanyama. Sasa kutokana na kukosekana kwa mvua muda mrefu, yamekauka na kusababisha shida hii unayoishuhudia.

"Maji tunayoyatumia kwa sasa ni ya tope lakini nayo upatikanaji wake ni mgumu sana kama unavyoona hapa na wakati mwingine tulazimika kukesha au kuja hapa usiku wa manane kuyatafuta.

"Tunaamka usiku wa manane kuja hapa kuyatafuta kwa sababu ukichelewa tu unakuta wenzio wamechota au mifugo imekunywa kwa sababu nayo inategemea haya haya."



Mifugo ikipatiwa huduma ya maji katika moja ya mifereji iliyochimbwa kwa ajili ya maji ya matumizi ya binadamu katika Kijiji cha Nanja wilayani Monduli mkoani Arusha. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

### WAWEKA MAJIVU

Naomi anasema miezi miwili iliyopita walikuwa wakipata maji ambayo hayana tope jingi na walipokuwa wakiweka majivu, yalisaidia kuchuja, lakini kwa sasa hata wakiweka hayajichuji kutokana na tope hilo kuzidi.

"Maji yanatoa harufu, kama una kinyaa huwezi kunywa, lakini kwa sababu hatuna namna nyingine unafumba macho unakunywa hivyo hivyo. Kikubwa unamwomba Mungu usiugue, japo tunafahamu kwamba siyo salama kwa afya yetu," anasema.

Naomi anafafanua kuwa katika kusaka mbinu mbadala kutafuta maji, wamebuni njia ya kuchimba mashimo pembezoni mwa bwawa la Nanja ambalo nalo limekauka, akibainisha kuwa linategemewa na wakazi wa vijini vyote vinane vya Kata za Lepurko na Sepeko wilayani Monduli vilivyoathiriwa na ukame.

"Kama unavyoona, haya ndio mashimo tunayochimba kuyafuata maji chini. Na huwezi kuchimba siku moja na maji yakatoka, hapana! Inabidi usubiri, ulale hapo mpaka kesho yake ndipo uchote.

"Kwa hiyo, tunaanza na maandalizi ya kuandaa shimo na njia ya kupitisha maji (mfereji) kwa siku moja na siku ya pili ukibahatika kama umechimba sehemu sahihi, maji yanaingia taratibu mpaka siku ya pili unaweza kuchota.

"Na wakati mwingine kama hujachimba kwenye eneo sahihi, hayaingii. Kwa hiyo, siyo rahisi kama unavyofikiri, yaani pamoja na kwamba ni tope lakini kuyapata kwake nako ni kubahatisha. Na ukibahatika yakaingia, usiende mbali, vinginevyo unakuta mifugo imekunywa yote au wenzio wamechota na huwezi kujua nani amefanya hivyo.

"Na wakati mwingine tunafukuzana na mifugo hapa, unakuta mifugo inang`ang`ania kuingia, inakunywa na hata ukiifukuza inakwenda hatua chache inageuka tena. Kwa hiyo inabidi uchote haraka kabla mifugo haijaja.

Kipindi hiki sisi kunywa maji kwa kuchangia na mifugo tumeezoea kutokana na shida hii inayotukumba.

"Kwa hiyo, tunachofanya ukimaliza kuchimba unaweka uzio wa miti ya miiba ili kuweka ulinzi ambao hata hivyo watu huwa wanatoa, na ukikuta wamechota, inabidi ukae usubiri tena kuona kama yatatoka mengine," Naomi anahitimisha ufafanuzi wake.

### MSAKO WA MAJI

Naseriana Meloki, mkazi wa Kijiji cha Kilotorok, Kata ya Sepeko, anasema wanalazimika kufuata maji umbali wa zaidi ya Km 15 katika bwawa hilo lililoko Kijiji cha Nanja, Kata jirani ya Lepurko, wakiamshana usiku wa manane na kwenda huko kwa makundi ya wanawake wakihofia kubakwa na kukutana na wanyama wakali.

Anasema kijiji chao kilikuwa na bwawa ambalo walikuwa wakilitegemea kupata maji, lakini limekauka na hivyo wanalazimika kuyafuata kwa umbali huo katika Kijiji cha Nanja.

"Na huko Nanja kwenyewe kumeshakauka, vimebaki 'vimaji' ambavyo vimetuama kwenye sehemu ndogo ndogo. Kwa hiyo tunachofanya kwa sababu kuna unyevunyevu, tunachimba mashimo pembeni yake, halafu tunatengeneza mifereji kutoka kwenye bwawa hadi kwenye mashimo tuliyotengeneza na tunayasubiria.

"Kwa hiyo mara nyingi sisi tunaotoka mbali sana, huwa inabidi tujipange wengine watangulie siku moja kwenda kuandaa shimo ili wengine wabaki kuwaangalia watoto, halafu siku inayofuata ndipo wengine mnakwenda kuchota sasa.

"Na ni lazima mwamshane usiku ili muwahi kwa sababu mkichelewa sana mnaweza kukuta yamechotwa yote au mifugo imekunywa," Naseriana anasimulia na kubainisha kikwazo kingine kwamba wakati mwingine wanakutana na wanyama wakali.

"Shida hii ya maji inaweka maisha yetu hatarini, wakati mwingine mnatembea mnaona kwa mbali tembo au mbogo, inabidi mkimbie sana, na nafikiri nao wanakuwa wanahangaika kutafuta maji usiku huo.

"Wakati unahangaika namna hiyo kutafuta maji, wanaume nao baadhi yao hawaelewi, wanafikiri kwamba wakati mwingine tunakwenda kwa wanaume wengine.

"Kwa mfano, unakwenda ukifika unakutana na mifugo imekunywa maji kwenye shimo lako, inabidi usubiri. Sasa mwanamume mwingine ukimwambia kwamba umekutana na shida hiyo, haelewi anaanza kukufokea na kukuita majina mabaya mpaka watu wanakuja kuamulia ugomvi.

"Pia watoto wanapata shida sana, wanaachwa na wazazi wao kwa muda mrefu bila kunyonyeshwa kwa sababu ni vigumu kutembea nao usiku. Wakati wewe na wenziko mnatoka saa nane usiku kuanza safari, kuna kijiji kingine wanaanza safari saa saba au saa sita usiku. Kwa hiyo, inakuwa kama kila mtu anamuwahi mwenzake," anabainisha.

### NDOO 1 KILA KAYA

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nanja, Yamati Lemomo, anasema kwa sasa mifugo na binadamu wanahangaika kupata maji, akikiri wananchi wa vijiji vinane vya kata za Lepurko na Sepeko wamekuwa wakifika katika kijiji chake hicho kuchota maji katika bwawa pekee lenye unafuu la Nanja.

"Kwa sasa bwawa hili nalo limekauka, kumebakia kama maji kidogo yaliyotuama, kwa hiyo wananchi wengi wanatoka huko kwenye vijiji vyao usiku wa manane na kuja hapa na kwa sasa kazi iliyoko ndio hiyo ya kuchimba mashimo kuyafuata maji chini ambayo kwa kiwango kikubwa ni tope," anasema.

Kiongozi huyo anathibitisha kuwapo ongezeko la migogoro ya ndoa kijijini huko, mingi ikisababishwa na wanawake kushindwa kutulia nyumbani, wakisaka maji.

"Huwa ninakwenda bwawani ninaona wanavyohangaika. Kwa hiyo, inabidi niwaeleze kwa kina waume zao ndipo angalau kunatulia.

"Lakini kuna ndoa tatu ambazo zenyewe ninaona zimenishinda sasa, au kwa lugha nyingine ninaweza kusema hazipo, zimevurugika na sababu kubwa ndio hii ya mambo ya kuhangaikia maji," anabainisha.

Lemomo anasema kwa sasa wanapatiwa maji ya dharura ambayo yanagawiwa kwa vijiji hivyo vinane vilivyoathirika zaidi.

"Lakini maji haya nayo hayatoshelezi kwa sababu watu ni wengi, awali wakati tumeletewa maji haya, lengo lilikuwa ni kugawiwa kila kaya ndoo mbili kwa siku, lakini baadhi ya kaya zilianza kukosa, tumeaona tuanze kuwagawia ndoo moja moja kwa kaya kila siku.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kuliona hili na kutuletea maji ya dharura, lakini kama ikiwezekana watuongezee zaidi kwa sababu ndoo moja haitoshelezi na ndio maana bado wengine wanalazimika kunywa haya ya tope kwa sababu ya ukubwa wa familia. Watu wanatumia hayo maji machafu kuongezea, wengine wanaweka majivu ili tope likae chini, watu wanaumia sana," anawasilisha kilio chao.

■ITANDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

# CRDB yatenga mabilioni ya kuwezesha vijana, wanawake

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

IKIENDELEZA jitihada zake za kukuza ujumuishi wa kiuchumi nchini, Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Tume ya TEHAMA imezindua programu mpya ya uwezeshaji vijana na wanawake wajasiriamali, Sh. bilioni tano zikitengwa.

Programu hiyo iliyopewa jina la 'IMBEJU' ilizinduliwa katika kilele cha Kongamano la Sita la TEHAMA lililofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Golden Tulip na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi kutoka ndani na nje ya nchi mwishoni mwa wiki.

Akielezea kuhusu programu hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kupitia 'IMBEJU', benki hiyo itakuwa ikitoa mitaji wezeshi kwa vijana na wawawake wajasiriamali wenye biashara na mawazo bunifu.

Nsekela alisema kupitia programu hiyo vijana watakuwa wakiwasilisha mpango wa biashara zao na mawazo bunifu kwa upande wa wanafunzi, kisha wataalamu wabobezi watakuwa wakichambua na kuidhinisha mtaji na mafunzo kulingana na vigezo.

"Katika programu ya IMBEJU, tutakuwa pia tukitoa mafunzo ya usimamizi wa biashara, matumizi ya mifumo ya TEHAMA, elimu ya fedha na masoko, na usaidizi wa kuboresha bidhaa na mawazo bunifu," alisema Nsekela.

Aliongeza kuwa benki hiyo pia imeanzisha kituo maalum cha mafunzo na ubunifu wa biashara katika Makao Makuu ya zamani ya benki hiyo Mtaa wa Azikiwe jijini Dar es Salaam. Kituo hicho kitasimamiwa kwa ushirikiano na Tume ya TEHAMA nchini.

"Katika programu za vijana wajasiriamali, tumeweka mkazo mkubwa zaidi katika biashara zinazoanza katika sekta ya TEHAMA tukilenga zaidi kuchochea uchumi wa kidijitali. Biashara katika sekta nyingine pia zitakuwa zikipata uwezeshaji," alifafanua. Katika kuwawezesha wanawake wajasiriamali, Nsekela alisema benki hiyo itakuwa ikifanya kazi na taasisi na mashirika yaliyojikita katika kufanya uwezeshaji kwa wanawake. Uwezeshaji utafanyika kwa vikundi na mjasiriamali mmoja mmoja.

Kwa kuanzia katika uzinduzi huo wa programu ya IMBEJU, Benki ya CRDB ilikabidhi Sh. milioni 50 kwa Tume ya TEHAMA ikiwa ni uwezeshaji wa biashara changa katika sekta ya TEHAMA (digital start-ups).

Akizindua programu hiyo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha programu hiyo ya 'IMBEJU' akisema itasaidia kukuza ujumuishi wa kiuchumi kwa vijana na wanawake. "Idadi kubwa ya watu nchini ni vijana na wanawake. Licha ya hivyo ndio watu tegemezi zaidi kiuchumi. Serikali imekuwa ikiweka jitihada kubwa katika kuliwezesha kundi hili. Niipongeze Benki ya CRDB kwa kuunga mkono," alisema.

Mkurugenzi wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema wamejipanga vilivyo kuhakikisha programu ya 'IMBEJU' inakwenda kuchochea kwa kasi ukuaji wa biashara changa nchini.



# Ushirikiano Tanzania na Uturuki wapaisha uchumi

**Na Maulid Mmbaga**

TANZANIA imeeleza dhamira ya kuimarisha uhusiano wake na Uturuki katika sekta za afya na elimu ambazo nchi hiyo ya Ulaya imepata maendeleo makubwa.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (pichani), alitoa ahadi hiyo wakati wa hafla ya kuadhimisha miaka 99 tangu kutangazwa kwa Jamhuri ya Uturuki mwishoni mwa juma.

Alisema Tanzania inathamini dhamana ya urafiki na ushirikiano na nchi hiyo, hususan katika utaalamu wa sekta tajwa.

"Tangu zipate uhuru, Tanzania na Uturuki zimedumisha uhusiano mzuri na wa kindugu ambao umeendelea kukua hadi kufikia viwango vya juu, hasa baada ya kufunguliwa tena kwa Ubalozi wa Uturuki jijini Dar es Salaam mnamo Mei 2009 na ule wa Tanzania huko Ankara mwaka 2017," alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa kwa sasa kuna zaidi ya wanafunzi 400 wa Kitanzania wanaosoma katika vyuo vikuu vya Uturuki katika fani mbalimbali zikiwamo za afya, uhandisi, kilimo na sayansi ya jamii.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kwa sasa kuna takribani kampuni 48 za Uturuki zilizowekeza nchini katika sekta mbalimbali zikiwamo za viwanda, kilimo, ujenzi, rasilimali watu, utalii na usafirishaji.

"Hadi sasa, uwekezaji wa Uturuki nchini wenye thamani ya karibu dola milioni 324 na umetoa jumla ya ajira 3,455 kwa wakazi wa eneo hili na hivyo kuboresha maisha ya Watanzania wengi wadogo na wa kati," alisema.

Katika hotuba yake, Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu alisema kiwango cha biashara kati ya Tanzania na Uturuki kimeongezeka hadi dola milioni 300 katika kipindi cha miaka 10 kutokana na juhudi za mabalozi wa nchi hizo mbili katika kuimarisha zaidi uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia.

"Biashara yetu baina ya nchi haijatambua uwezo wake wa kweli na tunaamini kwamba kuna nafasi kubwa ya ukuaji, sio tu kwa suala la wingi, lakini katika anuai ya bidhaa na huduma," alisema.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

# UNAUDITED RESULTS
FOR THE NINE MONTHS ENDED 30 SEPTEMBER 2022

**CHAIRMAN'S STATEMENT**
Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results when compared to the same period 2021. Both the sales volume and revenue increased compared to the same period 2021. Revenue increased by 9% compared to the same period last year. This increase is due to the continued demand of cement products within Tanzania and outside Tanzania.

The high availability and efficiency of the plant and machinery has contributed to the improved performance compared to the same period 2021, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The Company continues to focus on delivering excellent customer service, selling of high quality products and maintaining strong customer relationships to enable TPCPLC to demonstrate its strength as the leading player in the industry.

| INCOME STATEMENT | JAN - SEP 2022 TZS'000 | JAN - SEP 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 358,338,268 | 328,423,941 |
| Cost of sales | (226,239,925) | (202,248,754) |
| **Gross profit** | **132,098,343** | **126,175,187** |
| Other operating income | 1,584,600 | 1,349,253 |
| Selling and administrative expenses | (2,205,913) | (2,197,480) |
| Administrative expenses | (15,564,513) | (14,224,974) |
| Depreciation and amortisation | (15,503,480) | (14,880,674) |
| Other operating expenses | (2,088,469) | (2,383,788) |
| **Operating profit** | **98,320,568** | **93,837,524** |
| Financial items | 2,211,669 | 992,428 |
| **Profit before tax** | **100,532,237** | **94,829,952** |
| Taxes on income | (30,564,898) | (29,010,234) |
| **Profit for the year** | **69,967,339** | **65,819,718** |

| BALANCE SHEET | 2022 TZS'000 | 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 861,623 | 1,054,842 |
| Tangible fixed assets | 144,210,083 | 134,849,020 |
| Other non-current assets | 6,370,423 | 3,332,492 |
| **Non.current assets** | **151,442,129** | **139,236,354** |
| Inventories | 74,386,616 | 58,109,925 |
| Trade and other receivables | 71,106,797 | 56,315,009 |
| Cash and cash equivalents | 89,219,635 | 117,873,050 |
| **Current assets** | **234,713,066** | **232,297,984** |
| **TOTAL ASSETS** | **386,155,195** | **371,534,338** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **272,033,024** | **250,650,668** |
| Lease liabilities | 5,378,124 | 2,219,941 |
| Long term provisions | 9,766,965 | 6,992,932 |
| Provision for deferred taxes | 9,808,603 | 12,008,872 |
| **Non-current liabilities** | **24,953,692** | **21,221,745** |
| Lease liabilities | - | - |
| Current income tax payable | 982,398 | 2,162,853 |
| Trade and other payables | 85,212,738 | 94,546,798 |
| Dividend payable | 2,973,343 | 2,952,274 |
| **Current liabilities** | **89,168,479** | **99,661,924** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **386,155,195** | **371,534,338** |

**Prospects**
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its leadership.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
19/10.2022

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.co.tz**
**Email: info@twigacement.co.tz**

217122701

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga malizeni kazi kwa Mkapa kufuzu shirikisho

**MABINGWA** watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, keshokutwa, Jumatano watatupa karata yao ya kwanza dhidi ya Club Africain ya Tunisia kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga ambayo itakuwa mwenyeji kwenye mechi hiyo ya kwanza itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, imeangukia hatua hiyo ya kucheza mechi ya mtoano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho, baada ya kutolewa katika raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1.

Hivyo, kwa mujibu wa kanuni za waandaaji wa michuano hiyo, Shirikisho la Soka Afrika (CAF), timu zote zinazotolewa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, hucheza mechi ya mchujo nyumbani na ugenini dhidi ya zilizopenya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho ili kuwania kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Kwa mantiki hiyo, Yanga inahitaji kupata matokeo ya jumla nyumbani na ugenini dhidi ya Watunisia hao, ili kufuzu hatua hiyo ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa ukubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Kikubwa Yanga inachotakiwa kufanya ni kuhakikisha keshokutwa inapata ushindi mkubwa wa magoli ili kurahisisha kazi katika mechi ya marudiano Novemba 9, mwaka huu nchini Tunisia.

Tunatambua ujanja wa timu za Mashariki, maarufu za Kiarabu, ambao huutumia zikiwa ugenini, huhakikisha zinapoteza muda kwa kujiangusha, kutoa presha kwa mwamuzi kwa kumlalamikia mara kwa mara, huku zikitumia mashambulizi ya kushtukiza.

Hivyo, Yanga haina budi kuwa makini katika ujanja huo na kuepuka kuingia mtegoni kwenye mbinu hizo za Waarabu kwani mara nyingi wanachotafuta ugenini ni sare na ikiwezekana ya mabao ili baadaye kwenda kunufaika na bao la ugenini.

Sote tulishuhudia namna Club Africain walivyocheza kwa mbinu hizo kwenye raundi ya kwanza dhidi ya Kipanga FC ya Zanzibar na kufanikiwa kupata sare tasa katika Uwanja wa Amaan visiwani humo.

Matokeo hayo yaliifanya Kipanga kuiona Club Africain ni ya kawaida na kuamini inaweza kwenda kuwachapa kwao, lakini ilipofika Tunisia, ilibebeshwa kitu kizito kichwani kwa kuchapwa mabao 7-0 na kutolewa kwenye michuano hiyo.


Hivyo, Yanga haina budi kukwepa mtego huo kwa kuhakikisha inapata mabao mengi nyumbani na kutoruhusu wapinzani wao kuziona nyavu zao, ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufuzu hatua ya makundi katika mechi ya marudiano.

Tunatamani kuiona timu nyingine kutoka Tanzania ikifuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo ya CAF kwa ngazi ya klabu baada ya Simba kuwa klabu pekee kutoka nchini kutinga hatua hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Inafahamika wazi kuwa na timu zaidi ya moja kwenye hatua ya makundi katika michuano hiyo ya CAF, zinasaidiana kuiongezea nchi pointi na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuingiza timu nne kwenye mashindano hayo msimu unaofuata.

Hivyo, tunaamini Yanga imefanya na inaendele kufanya maandalizi makubwa kuelekea mechi hiyo ya mchucho, lakini ikichukua tahadhari zote nje na ndani ya uwanja na katika hilo Nipashe tunaungana na wadau wote wa soka na Watanzania kwa ujumla kuwaunga mkono wawakilishi wetu hao wa nchi kimataifa ili kufanikisha lengo lao la kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kushindwa kwenye Ligi ya Mabingwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi sasa ndio 'kirusi' cha soka letu

**KWENYE** mitandao ya kijamii nimekutana na sehemu ambayo waandishi wa michezo wa nchi za Ghana, Nigeria, Burkina Faso na Cameroon, wakipostiana video na picha za mechi kati ya Geita Gold dhidi ya Yanga, wakiulizana ni kwa nini mwamuzi aliamua iwe penalti?

Walikuwa wakiizungumzia mechi ya juzi kati ya Geita Gold dhidi ya Yanga iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, ambapo moja ya tukio lililowaacha watu hoi ni mwamuzi wa kati, Florentina Zablon, kuamuru mkwaju wa penalti ambao mchezaji George Wawa alikuwa ameushika mpira nje ya eneo la hatari.

Kwa bahati mbaya sana penalti hiyo ya utata ndiyo iliyoamua mshindi kwenye mechi hiyo, Yanga ikishinda kwa bao 1-0.

Nilichofurahi ni kwamba kumbe Ligi ya Tanzania imekuwa ikifuatiliwa sana miaka ya hivi karibuni, tofauti na huko nyuma. Ilikuwa si rahisi kuona waandishi, wachambuzi na wadau wa soka kwenye nchi kubwa zilizoendelea kisoka kama hizo zikiifuatilia Ligi Kuu Tanzania Bara.

Lakini kutokana na uwekezaji mkubwa wa pesa, ligi kuonyeshwa karibuni mechi zote za msimu, pamoja na wachezaji kutoka kila pembe ya Afrika na dunia, wakimiminika kucheza soka la kulipwa nchini, hivyo kuifanya Ligi ya Tanzania kufuatiliwa sana na kutajwa kama ni moja kati ya ligi bora Afrika.

Hata hivyo, nasikitika kusema kuwa ligi bora inachezeshwa na waamuzi ambao si bora. Tumeona kwa siku za karibuni waamuzi wamekuwa wakisimamishwa, kupelekwa kwenye kamati na kufungiwa kutokana na kuboronga.

Kwa kawaida mchezo wa soka ni wa makosa, na tunaona hata huko nje waamuzi wanakosea, lakini si kwa namna ambayo waamuzi wa Tanzania wanakosea.

Mfano tukio la juzi halikuwa ni la kutafsiri sheria, bali lilihitaji umakini tu kwa sababu ni kweli mchezaji wa Geita Gold alishika, lakini je, ni ndani ya eneo la 18?

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, alishawahi kusema mwamuzi wa mpira wa miguu ni sawa na hakimu au jaji, hivyo anatakiwa kuwa makini sana.

Na tunaambiwa kwenye moja kati ya mafunzo yao wanaambiwa kuwa ni bora umuache mhalifu kama hakuna ushahidi uliokamilika kuliko kumfunga mtu ambaye hana kosa.

Hata kwenye uamuzi ni bora ukatae bao au penalti kama huna uhakika, kuliko kutoa vitu hivyo kimakosa. Ni kwa sababu mwamuzi anadhulumu haki ya mwingine.

Kwa leo inaweza kuonekana kama haina umuhimu, lakini ipo siku wanaweza kuja kuikumbuka. Geita Gold inaweza huko mbele kuhitaji pointi moja ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Afrika au Shirikisho ama kujinusuru kushuka daraja, ndipo watu watakapokumbuka kuwa kuna siku walinyimwa pointi yao kwa kuruhusu penalti ambayo si halali.

Nilichoshangaa na kuona ni mwamuzi akitoa penalti hiyo akionekana kabisa kuwa na uhakika, kwani pamoja na wachezaji wa Geita Gold kumzonga hakustuka na kuamua kwenda kumuuliza mwamuzi msaidizi.

Mwamuzi msaidizi naye ambaye naye alikaa kwenye sehemu ambayo alitarajiwa kuona tukio hilo vizuri zaidi, hakujishughulisha hata kumsaidia mwamuzi wa kati licha ya kuzongwa na wachezaji.

Kwa tukio hilo na mengine yaliyotokea kwa waamuzi, iwe kwa makusudi au bahati mbaya hayaleti taswira nzuri kwenye soka la Tanzania. Wale waandishi wa Afrika Magharibi wanaweza kuona kuwa aina hiyo ya uchezeshaji ndiyo maana timu za Tanzania hazifanyi vizuri zinapokwenda kucheza mechi za kimataifa.

Imefika wakati sasa wadau wote wa soka nchini Tanzania tuone aibu na kukataa mambo haya ambayo sasa yameanza kuonekana kama ya kawaida kwenye soka letu.

Ama imefika kweli wakati wa kuletwa mashine za kumsaidia mwamuzi (VAR), au iwekwe kanuni ya kualika waamuzi kutoka nje ya nchi kuchezesha baadhi ya mechi za Ligi Kuu nchini.

## Mfumo wa ununuzi wafanyiwa maboresho

**Na Waandishi Wetu,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, amesema serikali imeweka udhibiti wa mianya ya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma uliosababishwa na kasoro katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma (TANePS) kwa kufanya maboresho makubwa ya mfumo huo.

Aliyasema hayo jana mkoani Iringa alipofanya ziara ya kukagua maboresho ya mfumo huo yanayofanywa na wataalamu wa ndani kwa lengo la kuondoa shida zilizoko na kukidhi mahitaji halisi ya serikali na wazabuni.

Chande alisema kumekuwa na shida kupata thamani halisi ya fedha katika huduma na bidhaa kutokana na mianya ya rushwa iliyokuwapo katika mfumo wa ununuzi iliyosababisha utofauti mkubwa wa gharama kwenye eneo moja.

"Kumekuwa na usiri mkubwa katika michakato ya ununuzi, hali inayofanya mtu ajiulize huu usiri una nini katikati yake, ununuzi unatakiwa ufanyike kwa uwazi na haki, hivyo wataalamu mnaofanya maboresho haya mnaweza kututengenezea mfumo unaoakisi uhalisia katika ununuzi na utakaosaidia ununuzi kufanyika kwa haki," alisema Chande.

Aliongeza kuwa nia ya serikali ya kufanya maboresho hayo ni kuhakikisha taasisi nunuzi zinatoka katika mazoea ya kufanya michakato ya ununuzi nje ya mfumo kwa kuwa ununuzi wa nje ya mfumo unaongeza uwezekano wa rushwa na upotevu wa thamani ya fedha.

Chande alisema zipo faida nyingi ambazo serikali itazipata baada ya maboresho hayo kukamilika ikiwamo kuimarika kwa uchumi wa nchi kwa kuokoa mapato ya serikali yanayopotea kwa kuwa asilimia 70 ya matumizi yote ya bajeti ya nchi yameelekezwa katika ununuzi.

Pia alimtaka Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Eliakumu Maswi, kuhakikisha wote wanaotakiwa kutumia mfumo huo wanautumia kwa kuwa inasikitisha kuona wataalamu wanatumia muda na nguvu zao kufanya maboresho ya mfumo halafu wengine wanakaidi kuutumia.

Chande pia aliipongeza PPRA kwa juhudi inazoendelea nazo za kusimamia maboresho makubwa katika mfumo wa ununuzi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Sekta ya Ununuzi nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakumu Maswi, alimwahidi naibu waziri huyo kuwa maboresho ya mfumo huo yatauwezesha kuwa bora katika nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Pia atahakikisha wote wanaotakiwa kuutumia mfumo huo wanasajiliwa ili lengo la kufanya kazi za ununuzi wa umma kwa uwazi linafikiwa na kuwa chachu ya maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, aliipongeza serikali kwa kuhakikisha yanafanyika maboresho makubwa ya mfumo wa ununuzi wa umma kwa kuwa si jambo rahisi kuingia katika maboresho hayo bila kuwa na msaada kutoka kwa wataalamu wa nje ya nchi.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanatumia mfumo huo iwapo wanataka kufanya biashara na serikali kwa kuwa utakuwa rahisi kuutumia na umeangalia hali halisi ya Mtanzania na soko la ndani.

Uamuzi wa maboresho ya Mfumo wa Ununuzi nchini ulitokana na agizo la Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 bungeni.

Maboresho hayo yaliyoanza mwezi Julai mwaka huu, yanatarajia kufanyika kwa awamu sita ambapo mpaka sasa awamu ya kwanza tayari imeshakamilika na inatarajiwa majaribio yake yaanze mwezi Desemba mwaka huu.




Washindi wa shindano la kubuni wazo la kutatua tatizo la msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia teknolojia ya intelijensia bandia, wakipokea zawadi zao kwa Jaji Mkuu, Hilda Bukoko wa Wizara ya Afya. Washindi hao watapata nafasi ya kupata mafunzo zaidi kufanya wazo lao kuwa halisi katika kiota cha mafunzo cha Ujuzi Incubation Center. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Meli ya Kijeshi ya India yatia nanga Dar kimkakati

**Na Romana Mallya**

MELI ya Kijeshi ya India, (INS) Tarkash, imetia nanga kwa siku tatu katika Bandari ya Dar es Salaam, ikitumika kutoa fursa kwa wanajeshi wa nchi hiyo na wa Tanzania kufanya mazoezi.

Baada ya kuwasili, Mkuu wa Kikosi, Kapteni Abraham Samuel, akifuatana na Nahodha wa Ulinzi, Kapteni Nitesh Garg walimtembelea Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda pamoja na Kamanda wa Kikosi cha Jeshi la Wanamaji, Meja Jenerali Ramson Mwaisaka.

Oktoba 26 jioni, Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan pamoja na Mkuu wa Kikosi, Kapteni Samuel waliandaa hafla iliyofanyika kwenye meli hiyo. Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kiserikali na kijeshi akiwamo Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Salum Haji Othman pamoja na mabalozi kutoka nchi mbalimbali na raia wa India wanaoishi Tanzania.

Katika hafla hiyo, Balozi Pradhan pamoja na Luteni Jenerali Othman walizungumzia historia ya ushirikiano baina ya nchi hizo mbili.

Wakati wa ziara hiyo INS Tarkash ilishiriki kwenye mazoezi ya pamoja ya majeshi ya majini na Tanzania ambayo yalishirikisha pia wanajeshi wa Msumbiji.

Tukio hilo ni la kwanza la kujitolea kwa Jeshi la Maji la India kufanya pamoja na majeshi ya nchi za Afrika na limekuja baada ya Azimio la Gandhinagar kupitishwa wakati wa mjadala wa ulinzi kati ya India na Afrika wakati wa maonyesho ya kijeshi ya mwaka huu.

Mazoezi mbalimbali ya kijeshi yalifanyika ikiwamo namna ya kukabiliana na vitisho vya majini, ukaguzi kwa kutumia boti, uokozi, kuokoa kwa kutumia ndege, mapigano ya ana kwa ana na mizinga yalifanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 28.

Ziara za masomo kwa wanafunzi na diaspora yalifanyika wakiwa ndani ya meli hiyo na manahodha waliwatembeza wageni kwenye meli hiyo.

INS Tarkash ilizinduliwa kwenye Jeshi la Maji la India Novemba 9, 2012 na ilijiunga na Kamandi ya Jeshi la Maji la Magharibi mwaka huo huo. Jina lake lilitokana na lugha ya Sanskrit ambapo 'Tarkash' ina maana ya chombo chenye mishale ikiwa imebeba silaha za kutosha na ving'amuzi ikiwa na manahodha hodari, meli hiyo ni moja ya silaha kubwa za Jeshi la India.

## KABWELA

**Fadhili Mohamed**





Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni za Hill, Hillary Shoo (kushoto), akiwaonyesha wajumbe wa Bodi ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo mifuko ambayo huzalishwa na kiwanda hicho kwa ajili ya kufungashia bidhaa mbalimbali ikiwamo chakula cha kuku. Ujumbe wa TADB ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Ishamel Kasekwa, ulitembelea kiwanda hicho wilayani Bagamoyo mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ahamasisha waandishi mabadiliko ya sheria za habari

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amewahimiza waandishi wa habari na wadau wa habari nchini kuhakikisha wanapambana ili kubadili sheria za habari kwa kuwa utawala wa sasa umeridhia.

Amesema kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameshaonyesha nia ya kuzifanyia mabadiliko sheria hizo, wadau hao wa habari hawana budi kutumia vizuri fursa hiyo kwa kuwa hawajui Rais atakayeingia madarakani baada ya Rais Samia atakuwa na mtazamo upi dhidi ya tasnia ya habari.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo juzi jijini Arusha alipozungumza na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) pamoja na Wadau wa Haki ya Kupata Habari (CoRI), kuhusu mchakato wa mabadiliko ya sheria za habari nchini.

"Rais tuliyenaye sasa (Rais Samia Suluhu Hassan), ameonyesha moyo na nia ya kutetea na kutoa haki za vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini.

"Kwa sasa mazingira ni mazuri, sasa lisukumeni suala hili ili sheria zibadilishwe maana mkisubiri miaka 10 ijayo, hamuwezi kujua Rais atakayekuja baada ya hapo atakuwa na mtazamo gani juu ya vyombo vya habari," alisema Dk. Ndumbaro.

Wakati huo huo, Waziri Dk. Ndumbaro alisema baadhi ya nchi duniani huzuia zisitolewe na zisiwafikie wananchi kwa madai ya kulinda usalama wa taifa.

Alisema pamoja na umuhimu wa taarifa hizo zinazozuiwa kutolewa, baadhi huwa zinalenga zaidi kuficha maovu ya watu binafsi ili yasifahamike katika jamii tofauti na kauli zinazotolewa.

"Taarifa kuhusu usalama wa taifa si sahihi kutotolewa hadharani, lakini baadhi ya watawala duniani hutumia kigezo hicho kuficha taarifa ambazo ni muhimu wananchi kuzijua kwa kuwa zinaweza kuharibu maslahi yao.

"Kwa ujumla, tunapaswa kutunga sheria zenye viwango na zitakazodumu kwa muda mrefu na ninasema wakati wa mabadiliko ya sheria ya habari nchini ni huu," alisema Waziri Dk. Ndumbaro.

Pia alimmwagia sifa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kwa kile alichosema kwamba waziri huyo ameonyesha nia ya kusimamia mabadiliko ya sheria hizo zinazolalamikiwa ikiwamo Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016.

Sheria nyingine zinazolalamikiwa na wadau hao wa habari ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Huduma za Posta (EPOCA, 2010), Sheria ya Makosa Mtandaoni (2015), Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa (2016) na Sheria ya Kanuni za Maudhui Mtandao (2018).

Dk. Ndumbaro alisema yeye na wabunge wengine watashiriki kusaidia Tanzania kupata sheria nzuri za habari, kwa kuwa sheria nzuri zitawezesha kukuza haki ya kupata habari, uhuru wa vyombo vya habari na haki ya watu kutoa maoni itakayozalisha maendeleo ya haraka kwa nchi.

Pia alikubaliana na TEF pamoja na wadau wa habari kuwa suala la Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) nchini kuwa na mamlaka ya kuwa mlalamikaji, mwendesha mashtaka, mtoa hukumu na msimamizi wa hukumu aliyoipitisha, linafifisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria.

# Serikali yawapa angalizo watumishi mikopo umiza

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii amewataka watumishi wa umma kuvitumia Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa (SACCOS) zilizoko kwenye maeneo yao ya kazi ili kuepuka kuingia kwenye mikopo umiza mitaani.

Pia amewataka watumishi hao kutumia mikopo hiyo wanayopata kwenye SACCOS kuanzisha miradi ya ujasiriamali na biashara ambazo zitaongeza kipato chao.

Juma Mkomi alitoa angalizo hilo wakati wa kufungua mkutano mkuu wa pili wa Chama cha MNRT Saccos Ltd cha wizara hiyo uliofanyika jijini hapo mwishoni mwa wiki.

Mkomi aliwashauri wafanyakazi kutumia vikoba vya utawala kuhamasishana kujiunga kwenye SACCOS zilizoko kwenye maeneo yao ya kazi ili kuepuka kutumbukia kwenye mikopo umiza mitaani.

"Kujiunga na SACCOS sio tu kwamba kunasaidia kuweka akiba ya kukunusuru wakati wa changamoto, bali pia kunawajengeeni tabia ya kuweka akiba kwa ajili ya siku za mbeleni hususani baada ya kustaafu katika utumishi wa umma," alisema.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema mikopo hiyo ni rahisi kuipata pamoja na unafuu wa kulipa kwa mfanyakazi na anaweza kukopa tena hata kama ana mkopo mwingine.

Aliongeza kuwa baadhi ya watumishi wa umma hupumbazwa na mishahara wanayopata, jambo ambalo huwafanya kukaa bila kuwa na mpango maalum wa kujiwekea akiba ama kuwa na mbadala wa kuwanusuru mara dharura zinapojitokeza.

"Kama mnavyojua tena, tarehe za mwisho wa mwezi huwa zinajulikana sana kwa jamii inayotuzunguka na ni tarehe hizo hizo za mwisho wa mwezi ama siku za moshi mweupe maombi ya fedha kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki huongezeka, hivyo fedha ikikatwa juu kwa juu kwenda SACCOS husaidia kuongeza mpangilio mzuri na nidhamu ya matumizi ya fedha," alifafanua. Mwenyekiti wa SACCOS ya wizara hiyo, Wilfred Msemo alisema ina jumla ya wanachama 244 na wanaendelea kuwahamasisha wafanyakazi wengine kujiunga.

Msemo alibainisha kuwa SACCOS yao inatoa mikopo kwa wakati na wanaweza kutoa mkopo wa hadi Sh. milioni 20 na pia wanatoa mikopo ya dharura ya hadi Sh. milioni mbili kwa mwanachama wao.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2021 walitoa mikopo ya Sh. milioni 566 kwa wanachama wao na wamekuwa wakiwapatia kwa wakati wanapoomba.

# NBC yatanua huduma zake

**Na John Badi**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amezindua tawi jipya la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) eneo la Kibada wilayani Kigamboni, akitoa wito kwa wakazi wa wilaya hiyo na maeneo jirani kuchangamkia fursa za kiuwezeshaji, kiuchumi zinazoletwa na benki hiyo wilayani humo.

Hafla ya uzinduzi wa tawi hilo ilifanyika kwenye tawi hilo jana na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa chama na serikali, viongozi waandamizi wa benki hiyo na wafanyakazi, wawakilishi wa jumuiya ya wafanyabiashara na wananchi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Makalla alisema mitaji ya fedha ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi, hivyo kuwapo benki hiyo wilayani humo kutakuwa na tija zaidi iwapo tu wakazi wa wilaya hiyo watatumia vyema fursa hiyo.

"Ninajua fika kwamba kusogezewa karibu huduma za kifedha ikiwamo benki kama hivi ni jambo moja na kutumia ipasavyo kuwapo kwa huduma hizi ni jambo lingine. Ndio maana ninawaomba sana wana Kigamboni kutumia vyema kuwapo kwa benki kama hii ya NBC kwa kutunza akiba zenu na pia kukopa ili kuwekeza na kukuza biashara zenu," alisema.

Makalla alitoa rai kwa benki hiyo kuendelea kubuni mipango mbalimbali ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia benki sambamba na kubuni huduma zinazowagusa wananchi wa wenye hali ya kawaida kiuchumi ili waweze kutumia vyema fursa na huduma zinazotolewa na benki hiyo.

"Ninafahamu Benki ya NBC mmekuwa mkibuni njia mbadala za kuwahudumia wateja kupitia njia mbalimbali ikiwamo kupitia mawakala na huduma kupitia simu, yaani NBC Kiganjani, NBC Shambani na nyingine nyingi, ninawapongeza sana, lakini ninaomba sana endeleeni kuwaelimisha wateja wenu namna ya kutumia fursa za kibenki na kujiweza na kujikomboa kiuchumi," aliagiza.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatuma Nyangasa, aliishukuru benki hiyo kwa kusogeza huduma zake wilayani Kigamboni kwa kuwa itarahisisha upatikanaji wa huduma za kibenki ambazo kwa kiasi kikubwa wilaya hiyo inategemea kuzipata kupitia Wilaya ya Temeke.

"Wilaya ya Kigamboni kwa sasa inakua kwa kasi sana na wakazi wanaongezeka kila siku huku shughuli za kiuchumi pia zikiongezeka. Ongezeko hili la watu na ukuaji wa kiuchumi linahitaji kwenda sambamba na huduma mbalimbali ikiwamo hii ya kifedha, tunawashukuru sana NBC kwa kuliona hili," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema benki hiyo ambayo inamilikiwa na serikali kwa asilimia 30 inaendelea kuunga mkono dhamira ya serikali ya kuwawezesha wajasiriamali na wakulima na wazalishaji wengine katika sekta za uchumi kwa kwa kutoa mitaji ya kifedha na mikopo nafuu.

"Jitihada hizi tunazitekeleza kwa urahisi zaidi kutokana wingi wa matawi yetu katika mikoa mbalimbali nchini. Tawi hili jipya la Kigamboni tunalolifungua leo (jana), linafanya Benki ya NBC sasa kuwa na jumla ya matawi 16 mkoani Dar es Salaam pekee huku tukiwa na matawi 47 kote nchini," alibainisha.

Alisema tawi hilo linakwenda kuondoa shida iliyokuwapo kwa wateja wa benki hiyo wilayani humo waliokuwa wanalazimika kuvuka maji ili kufuata huduma ng'ambo ya pili.

## TANGAZO

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/09/2022 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2022 |
|---|---|---|
| | TZS | TZS |
| **A. MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 187 | 103 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,049 | 9,108 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | - | - |
| Mikopo Halisi Iliyopo | 22,960 | 19,499 |
| 12 Mali Nyingine | 1,858 | 2,061 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 1,523 | 1,551 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **30,577** | **32,322** |
| **B. DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 Amana za Wateja | 2,330 | 2,097 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | 3,207 | 3,513 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 7 | 7 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mte | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 783 | 679 |
| 27 Zitakazolipwa Baadae | 3,691 | 2,403 |
| 28 Dhima Nyingine | - | - |
| **29 Madeni** | **10,017** | **8,699** |
| **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30 MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **20,560** | **23,623** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 12 | 12 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 842 | 859 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,369) | (487) |
| 35 Akauti Nyingine za Mtaji | 1,875 | 2,040 |
| **36 Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **20,560** | **23,623** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 Mikopo Chechefu | **280** | 607 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **883** | 1,000 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | **-** | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **67%** | **73%** |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **1.2%** | **3.0%** |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **422%** | **357%** |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **76%** | **62%** |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **76%** | **79%** |
| (vi) Ongezeko la Amana | **-1.3%** | **3.6%** |
| (vii) Ongezeko la Mali | **-5.4%** | **-3.7%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2022 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/09/2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 Mapato ya Riba | 2,670 | 2,345 | 7,571 | 7,415 |
| 2 Gharama za Riba | 10 | 4 | 21 | 11 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **2,661** | **2,340** | **7,550** | **7,404** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (206) | **(70)** | (450) | **(243)** |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **780** | **542** | **2,075** | **1,287** |
| 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (27) | (16) | (43) | (16) |
| 6.2 Ada za Kamisheni | 522 | 412 | 1,501 | 877 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 285 | 147 | 618 | 427 |
| **7 Gharama Zisizo na Riba :** | **6,118** | **2,511** | **12,544** | **7,374** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,594 | 1,193 | 4,513 | 3,615 |
| 7.2 Gharama Nyingine | 4,523 | 1,318 | 8,032 | 3,759 |
| 7.3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(2,883)** | **302** | **(3,369)** | **1,074** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | - | 53 | - | 158 |
| **10 Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2,883)** | **249** | **(3,369)** | **916** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | **352** | **263** | **352** | **263** |
| 12 Mapato kwa Hisa | (135,981) | 11,755 | (158,937) | 43,212 |
| 13 Kipato kwa Hisa | (135,981) | 11,755 | (158,937) | 43,212 |
| 14 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 Vituo Vya Biashara | 36 | 54 | 36 | 54 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | -9.2% | 0.7% | -10.7% | 2.7% |
| (ii) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -13.0% | 1.0% | -15.3% | 3.6% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 178% | 87% | 130% | 85% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalish | **22%** | **20%** | **62%** | **62%** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2022 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| I: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **(2,883)** | **(311)** | **(3,369)** | **916** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 226 | 124 | 469 | 345 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,461) | (1,047) | (3,533) | (2,386) |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (73) | 194 | 131 | 725 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 203 | (235) | (158) | 942 |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 1,391 | (274) | 2,306 | 69 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(4,597)** | **(1,549)** | **(4,155)** | **611** |
| II: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (198) | (141) | (482) | (191) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | | | | |
| | **kwa Shughuli za uekezaji** | **(198)** | (141) | (482) | (191) |
| | | - | - | - | - |
| III: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (181) | (31) | (1,882) | (264) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **(181)** | **(31)** | **(1,882)** | **(264)** |
| IV: | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tast | (4,975) | (1,721) | (6,518) | 156 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwa | 9,211 | 10,932 | 10,754 | 11,703 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu / Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **4,236** | **9,211** | **4,236** | **11,859** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022

(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2022)** | **21,200** | **2,487** | **0** | **2,124** | **25,811** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **(3,369)** | **-** | **-** | **(3,369)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **-** | **(612)** | **-** | **(1,270)** | **(1,882)** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **(1,494)** | **0** | **854** | **20,560** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2021)** | **21,200** | **1,447** | **0** | **2,206** | **24,853** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **1,288** | **-** | **-** | **1,288** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **-** | **(248)** | **-** | **(82)** | **(330)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **2,487** | **0** | **2,124** | **25,811** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 14 Oktoba 2022 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | | 14 Oktoba 2022 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 14 Oktoba 2022 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | **Athanasia Soka ( Mwenyekiti ya Bodi)** | | 14 Oktoba 2022 |
| 2 | **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 14 Oktoba 2022 |

2171243O3



Inspekta Jenerali wa Polisi Tanzania, (IGP) Camilius Wambura, akiwa pamoja na Menejimenti ya Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) (kutoka kulia) ni Mkuu wa Idara ya Ulinzi na Usalama, Suleiman Machira; Makamu Rais wa AngloGold Ashanti anayeshughulikia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo; Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong na (kushoto) Mwanasheria Mwandamizi wa GGML, David Nzaligo, walipomtembelea IGP ofisini kwake jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuendelea kuimarisha uhusiano na serikali kupitia Jeshi la Polisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukame wamshtua Mkuu wa Wilaya

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, amesema ukame uliochangia kukosekana kwa mvua za vuli, umeanza kuleta athari ya kupungua kwa maji katika Manispaa ya Morogoro na kuwataka wananchi kutumia maji kwa uangalifu.

Msando alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa mwaka wa Baraza la Madiwani Manispaa ya Morogoro, akibainisha ukame umesababisha uhaba wa maji kwenye vyanzo vyake hasa vilivyo katika safu za milima ya Uluguru.

"Zipo changamoto ambazo tunaendelea kuzifanyia kazi. Kama mnavyoona waheshimiwa madiwani, ninyi ni mashuhuda huko katika kata zenu, hali sio nzuri," alisema Msando.

Alisema kumekuwa na mgawo wa siku mbili na baadhi ya maeneo siku tatu ili kupata maji na serikali ya wilaya inashughulikia kero hiyo kwa kuchukua hatua za haraka ili kuona ni namna ya kutatua shida hiyo.

Alisema uhaba wa maji unachangiwa na mito mingi kukauka ukiwamo Mto Morogoro, Mto Mzinga na mingine ambayo inachangia maji kwenye Bwawa la Mindu.

"Kupitia kwenu madiwani, ninawaombe mkawaeleze wananchi watumie maji kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa hivi sasa maji tuliyonayo ni kidogo, ninatambua mnapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi," alisema Msando.

Aliongeza kuwa ukame uliopo ni mkubwa na serikali inaendelea kuhakikisha inapambana hasa kudhibiti vyanzo vya maji visiharibiwe.

"Tuendelee kufunga mikanda. Kwa mujibu wa wataalamu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mvua za vuli zinatarajia kupatikana wiki ya pili ya mwezi Desemba, bado mwezi mmoja wa kupambana," alifafanua.

Katika kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa (RCC) cha Oktoba 23, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Morogoro (MORUWASA), Tamimu Katakweba, alisema nanispaa hiyo inakabiliwa na shida katika upatikanaji wa maji, akibainisha kuwa huduma hiyo kwa sasa inapatikana kwa asilimia 48, mahitaji ya sasa yakiwa lita milioni 73 kwa siku.

Alisema uzalishaji wa maji kwa sasa ni wastani wa mita za ujazo milioni 35 hadi 37 kwa siku na manispaa inategemea maji kutoka Bwawa la Mindu kama chanzo kikuu cha maji.

Katakweba alisema bwawa hilo lina maji ya kutosha na kwa makadirio utoshelevu wake wa uhakika hadi kufikia Desemba mwaka huu endapo hakutakuwa na tatizo lolote.

# Serikali yaonya 'tegesha' maeneo yanayolipwa fidia

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema itawachukulia hatua kali wananchi wanaogushi na kujenga kwenye maeneo yanayotakiwa kulipwa fidia kupisha upanuzi wa shughuli za uchimbaji madini kwenye migodi ya Barrick.

Kitendo hicho kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka migodi ni maarufu kwa jina la tegesha, wakimaanisha kufanya uwekezaji kwenye eneo lililo mbioni kufanyiwa uthamini ili kupisha shughuli za mgodi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wilayani Tarime mkoani Mara, Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, alisema serikali inawathamini wananchi wake na itahakikisha wale wote wanaostahili kulipwa fidia kutokana na maeneo yao kuchukuliwa kupisha miradi, wanalipwa stahiki zao.

"Lakini hatutakubali kulipa watu ambao baada ya kujua kuna mradi unakuja na maeneo fulani yanachukuliwa, wanaanza kuyaendeleza kwa lengo la kulipwa fidia. Jambo hili serikali halitakubaliana nalo na ninawaonya wananchi kuacha kufanya hivyo," aliagiza.

Alisema Kampuni ya Barrick inayomiliki migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu mkoani Shinyanga na North Mara mkoani Mara, iko tayari kulipa fidia katika kila maeneo itakayochukua kwa ajili ya kupanua shughuli zake.

"Wananchi wanatakiwa kufahamu kampuni hii ya Barrick inafanya kazi kwa kushirikiana na serikali na ndio maana ya kuwapo kampuni tanzu ya Twiga Mineral Corperation ambayo ni mali ya serikali, hivyo kila shughuli inayofanywa serikali inakuwa sehemu ya shughuli hiyo, tuwaunge mkono kwa maendeleo yetu," alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano uliopo kati ya Barrick na Twiga Mineral Corperation umeleta tija na kuipa serikali faida kutokana na kuwapo kwa migodi hiyo.

Awali Rais na Mkurugenzi Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow alisema kampuni hiyo inataka kupanua shughuli zake za uchimbaji nchini.

Alisema kuwapo kwa migodi miwili pekee hakutoshi na hivyo wanajiandaa kuongeza maeneo ya uchimbaji.

# Waomba chakula cha bei nafuu serikalini

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa Kijiji cha Sindeni, Kata ya Sindeni, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, wameomba serikali iwasaidie kupata chakula cha bei nafuu ili wakabiliane na upungufu unaowakabili kwa miaka mitatu sasa.

Mkazi wa Kijiji hicho, Selemani Hamza, aliiambia Nipashe juzi kijijini huko kuwa upatikanaji wa chakula katika eneo hilo umekuwa mgumu kutokana na kusimama kwa shughuli za kilimo kwa kuwa hakuna mvua ya kutosha.

"Nina miaka mitatu sasa kila nikilima mahindi katika ekari zangu nne sipati kitu, sasa nimekula mpaka mbegu na uwezo wa kununua kilo ya unga kwa Sh. 1,800 sina kwa kuwa nina familia kubwa," alisema Selemani.

Zuwena Abdi, mkulima katika kijiji hicho, alisema kutokana na vyakula kuuzwa bei ya juu, analazimika kula mlo mmoja kwa siku ili kubana matumizi na kumudu gharama za maisha.

"Kwa kweli tukishakunywa uji asubuhi, tunakuja kusonga ugali jioni, mchana tunauacha upite kwa sababu uwezo wa kununua kilo mbili mchana na jioni siwezi maana sina kazi yoyote, ninategemea kilimo ambacho kimekataa tena mwaka huu," alisema.

Mama huyo mwenye familia ya watu sita alisema kuwa fedha ya kununulia chakula anategemea kupewa na mtoto wake ambaye humpa Sh. 30,000 kila mwezi, anayolalamikia kuwa haitoshi hata kununua mahindi ya kutumia kwa kipindi hicho.

Saida Salehe, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alisema vyakula vikipatikana kwa bei nafuu, kutamsaidia kumudu kuhudumia mifugo yake ambayo nayo kwa sasa inakonda kwa kukosa malisho ambayo nayo upatikanaji wake unahitaji fedha.

"Fedha nyingi ninaitumia kununua chakula, matokeo fedha ya kulipia majani ya mifugo ninakosa, maana upatikanaji wa majani ni wa shida, inatulazimu kununua kwa wenye maeneo yao. Mifugo yangu imeathirika kiasi cha kwamba nanaiuza kwa bei ya hasara," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Haji Mhina, alikiri kuwapo tatizo hilo na kwamba walishatoa taarifa kwa halmashauri kupitia ofisi ya kata lakini mpaka sasa hawajapokea majibu yoyote.

Mwenyekiti huyo alisema kulingana na hali yao kiuchumi, wanakijiji wanahitaji chakula kitakachouzwa chini ya Sh. 1,000 kwa kilo kwa sababu vyanzo vyao vya mapato vimeathirika na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Sindeni, Zamilida Zabron, alisema walipokea malalamiko ya kuwapo njaa katika kijiji hicho kunakochangiwa na bei ya vyakula ikiwamo vya nafaka kuwa juu na kuwa waliandika muhtasari na kuupeleka kwa mkuu wa wilaya.

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (UNDP), Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazosababisha majanga kama vile mafuriko na ukame yanayoathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi na kurudisha nyuma juhudi za kupunguza umaskini.



# RC atengua zuio wafugaji kuingiza mifugo mnadani

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, ametengua zuio lililowekwa na serikali za wilaya kuwazuia wafugaji kuingiza mifugo yao mnadani, kwa kisingizio cha kushindwa kuweka hereni za kielektroniki kwenye mifugo yao.

Uamuzi wa Makongoro kuzuia utekelezaji wa amri hiyo, aliufanya mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na sekretarieti ya mkoa huo.

Alisema iwapo wataendelea kuwawekea zuio wafugaji la kutokuingiza mifugo yao mnadani, watasababisha kuzorota kwa uchumi wa mfugaji, halmashauri na taifa kwa kuwa yapo mapato yatapotea.

"Wauzaji wa ng'ombe wakifika mnadani ni vizuri wawekewe hereni kwanza, au wauze ndiyo wawekewe hereni. Wapewe fursa ya kuuza mifugo yao na siyo vinginevyo," alisema Makongoro.

Katika kikao hicho, Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Mkoa huo, Issa Mnzava, alisema gharama ya kuweka hereni kwa ng'ombe mmoja ni Sh. 1,750 na mbuzi mmoja ni Sh. 1,000.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa huo, Samweli Dahaye, akitoa taarifa ya hali ya kampeni ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa njia ya ya kielekroniki alisema:

"Halmashauri ya Wilaya ya Babati imeweka hereni ng'ombe 5,054 kati ya ng'ombe 315,680 sawa na asilimia 1.6, punda 48 kati ya punda 6,080 sawa na asilimia 0.79.

"Wamo pia, mbuzi na kondoo 6,664 ndio wamewekewa hereni sawa na asilimia 2.5 katika Kijiji cha Mwada."

Alisema: Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, wameweka hereni ng'ombe 2,360 kati ya ng'ombe 266,852 sawa na asilimia 0.89 punda saba kati ya punda 4,398 sawa na asilimia 0.16."

Alisema baada ya Oktoba 30, mwaka huu mifugo yote isiyokuwa imetambuliwa na kusajiliwa haitaruhusiwa kuingia minadani, kuuzwa, kuchinjwa mabuchani au kupelekwa mnadani ama kusafirishwa.

Kuhusu Halmashauri ya Kiteto, Simanjiro, Babati Mjini na Mbulu Mjini, Dahaye, alisema bado wanaendelea na mchakato wa kupata wazabuni na kununua hereni.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Sulaiman Serera, alisema bei ya hereni ni kubwa kwa wafugaji wenye mifugo mingi.

Dk. Serera alisema wafugaji wa wilaya hiyo bado wana maumivu ya kupoteza mifugo yao yaliyosababishwa na ukame.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Batenga, alisema wafugaji wengi wanaangaika kupata sehemu za malisho ya mifugo yao.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza katika harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya ufunguzi wa ofisi za mabaraza ya wazee mikoa yote mahususi kwa ajili ya wazee wanaume mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Jeshi la Polisi lakusanya silaha haramu 990

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JESHI la Polisi nchini limekusanya silaha zaidi ya 990 ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya usalimishaji wa silaha kwa hiari ambazo zinamilikiwa na watu kinyume na sheria.

Kadhalika, kampeni hiyo ambayo ni ya kimataifa imefungwa rasmi hapa nchini.

Kwa mujibu wa Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini (DCP), Salehe Ambika, Jeshi la Polisi hadi kufikia Oktoba 28, mwaka huu lilikuwa limepokea silaha 997, kati ya hizo silaha 52 zimekamatwa kwenye matukio ya uhalifu.

Ambika ambaye ni Naibu Kamishna wa Polisi alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa kongamano la kuhitimisha kampeni hiyo ya usalimishaji wa hiari wa silaha haramu.

Kongamano hilo liliandaliwa na Jeshi la Polisi nchini, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Maridhiano na Umoja wa Huduma za Kitume na Kinabii Tanzania.

Ambika alisema: "Kampeni hii sasa imefika ukingoni kwa muda uliotolewa na serikali. Kuanzia sasa watakaokutwa na silaha au silaha bandia watachukuliwa hatua za kisheria." Kampeni hiyo ya usalimishaji wa bunduki, bastola au bomu, ilizinduliwa rasmi Septemba 5, mwaka huu na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni jijini Dodoma. Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo alinukuliwa akisema ni mahususi kwa ajili ya baadhi ya watu wanaomiliki silaha hizo.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kutambua kuwa suala la ulinzi na usalama ni la kila mmoja wetu na kila Mtanzania mpenda amani anao wajibu wa kuhakikisha analinda amani ya nchi yetu kwani pasipo amani hata maendeleo hayawezi kupatikana," alisisitiza Misime.

Misime alisema mtu yoyote atakayesalimisha silaha anayomiliki kinyume cha sheria katika muda utakaotolewa hatakamatwa, kubugudhiwa au kuulizwa jambo lolote.

# TFS yaagizwa kulinda, kuendeleza rasilimali za misitu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Balozi Pindi Chana, ameiagiza Bodi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kuhakikisha wanalinda, kuwahifadhi na kuendeleza rasilimali zote za misitu nchini.

Alisema hatasita kuchukua hatua kwa watu watakaojaribu kufanya shughuli za kilimo na kuingiza mifugo yao kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati wa uzinduzi wa bodi ya nne ya TFS.

"Atakayekamatwa ameigiza mifugo au kufanya shughuli yoyote ya kilimo kwenye maeneo ya misitu bila kufuata utaratibu sheria kali zitachukuliwa dhidi yao kwa kuwa tunafanya hivyo kwa faida yetu, tukiacha kulinda na kuendeleza rasilimali hizi, tutapata matizo ya kukosa mvua na majangwa," alisema.

Alisema Tanzania inarasilimali za misitu na nyuki ambazo ni muhimu kwa maendeleo kwa kuwa imekuwa na mchango kiuchumi, kijamii, kimazingira.

Alisema ametoa agizo hilo kwa kuwa hivi sasa kumekuwapo na tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza mifugo yao ndani ya misitu kuilisha.

"Viongozi wa vijiji, mitaa na kata hakikisheni mnasimamia sheria tulizojiwekea kwa faida na maslahi ya Watanzania kwa kuwa idadi ya watu inaongezea ukilinganisha na rasilimali zilizoko,"aliongeza.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema suala la moto limekuwa tatizo katika hifadhi, hivyo alitoa rai kwa wananchi kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzake na kutumia njia mbadala za kusafisha mashamba badala ya kuchoma.

"Nawakumbusha Watanzania wenzangu, tuwe makini na moto kwa kuwa gharama ni kubwa mno kuuzima, tuangalie ni kwa namna gani wakati wa kuanda mashamba kuchukua mbinu mbadala na siyo kutumia moto kwa kuwa harasa yake ukitokea kurudisha hali kuwa kawaida inachukuwa muda," aliongeza.

Mwenyekiti wa Bodi ya TFS, Brigedia Jenerali Mbaraka Mkeremy, alisema wakati wamepokea kijiti cha kuiongoza taasisi hiyo, ilikuwa changa lakini kwa sasa imekuwa kubwa hadi kufikia hatua ya kutoa gawio serikalini.

Aalisema tangu bodi kuingia madarakani wamefanikiwa kuongeza mapato kutoka Sh.bilioni 130 hadi kufikia Sh. bilioni 137.

# Moto Mlima Kilimanjaro wazuka tena Machame

**Na Godfrey Mushi**, MOSHI

WAKATI Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akitangaza kufanikiwa kuudhibiti moto uliokuwa unawaka katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), moto huo umeanza upya kuwaka eneo la Machame.

Moto huo ulionekana ukiendelea kuteketeza sehemu ya hifadhi hiyo baada ya kugunduliwa siku ya kwanza, Oktoba 21 mwaka huu katika eneo la kupumzikia wageni maarufu 'Karanga Camp' kuelekea Baranco.

Juzi baada ya kutumia helikopta kufanya ukaguzi katika maeneo yaliyoathiriwa na moto, waziri huyo aliutangazia umma kuwa moto huo tayari umedhibitiwa.

"Hivi sasa moto umedhibitiwa nimetoka kupanda huko juu kwa kutumia helikopta. Moto umedhibitiwa ukichia maeneo machache ambayo yalikuwa yana moshi.

"Sasa hali ya mlimani inaendelea kuwa shwari na tunaendelea kuudhibiti moto huo. Kwa hiyo matumizi mabaya ya ghafla yasiyofaa yanaweza kusababisha moto kuwaka ni lazima yaepukike. Tuwe macho na kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake."

Kamishna wa Uhifadhi wa Kanda ya Kaskazini, Betrita James, alinukuliwa akisema: "Hali ya moto kwa leo (juzi) inaonyesha matumaini kwa maana ya kwamba moto tuliokuwa tunauona ni hatarishi ni pamoja na ule uliokuwa kwenye korongo la Karanga, ambapo kutokana na juhudi tulizoziweka na kutengeneza vidhibiti moto, umezaa matumaini."

Ili kuudhibiti moto huo usiendelee kuiteketeza hifadhi hiyo inayohudumia hifadhi nyingine zaidi ya saba, serikali ilipeleka vikosi vya uokozi kutoka vitengo mbalimbali vya watu zaidi ya 500.

Mara ya mwisho moto kama huo ulizuka na kuteketeza sehemu ya hifadhi hiyo, Oktoba 11, 2020 katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Kanzidata ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, inaonyesha kuwa mwaka 2015/16 eneo lililoteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3, mwaka 2020 hekta 22.05.

Kwa kipindi kisichozidi miaka mitano mpaka kufikia mwaka 2020, jumla ya hekta ambazo ziliteketea kwa moto katika hifadhi hiyo zinatajwa kufikia 242.48, huku chanzo kikitajwa kuwa ni uvunaji mbaya wa asali, ujangili na njia mbaya za kilimo.

Katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ya mwaka 2020/21 iliyotolewa Machi 30 mwaka Charles Kichere, alisema amefanya uchunguzi kuhusu ripoti ya tukio la moto la KINAPA la Desemba 2020 na kutoa mapendekezo manne kwa mamlaka husika.

CAG Kichere mbali na mambo mengine, alisema moto huo ulisababisha hasara ya Sh. bilioni 1.214 na kubainisha kuwa mamlaka za hifadhi za taifa hazina uwezo wa vifaa na maandalizi ya kupambana na majanga ya asili.



Wadau wa maendeleo mkoani Tanga wa kikundi cha New Generation wakichangia damu kwa ajili ya kusaidia watu wenye uhitaji katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tanga Bombo jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Wamlalamikia RC kulipishwa fedha kusafirisha watuhumiwa

**Na Hamida Kamchalla**, KILINDI

WAKAZI wa Negero Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, wamepeleka kilio chao kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, kutokana na kutozwa gharama za usafiri wa watuhumiwa wanaofikishwa mahakamani.

Wamesema baadhi ya watuhumiwa au washtakiwa, ndugu zao hutakiwa kuwajibika kuwasafirisha kwenda mahakamani kwa kutumia usafiri wa pikipiki.

Walitoa kilio hicho juzi kwa Mgumba, aliyekuwa akizungumza nao katika mkutano wa hadhara Kata ya Negero.

Mmoja wa wakazi hao Ezron Kinasa alisema: "Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hali hii imekuwa ni kero kubwa kwetu, kwa kuwa wengine wanaonewa na hawana uwezo wa kumsafirisha mtuhumiwa au mshtakiwa kutoka Negero hadi Makao Makuu ya Wilaya (Songe).

"Mtu unafanyiwa uhalifu, unaripoti na kesi inafunguliwa, inafika kipindi mshtakiwa kupelekwa kule makao makuu ya wilaya ambako ndiyo kwenye mahakama.

"Unaambiwa ukodishe pikipiki mbili ili mshtakiwa na msindikizaji wapande moja na mlalamikaji nae apande yake. Hizo pikipiki zinakodishwa moja shilingi 60,000 kwenda na kurudi; kwa hiyo hapo jumla ni shilingi 120,000".

Kinasa alieleza hawana sababu ya kuwalaumu askari katika kata hiyo, kwa kuwa hawana gari la kubebea watuhumiwa kuwapeleka mahakamani.

"Tunaomba utusaidie Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hii kazi ya kusafirisha watuhumiwa wa makosa ya jinai anahusika nani? Lakini naomba kwa niaba ya hawa askari, ufanye kila linalowezekana uwapatie gari pale kituoni ili waweze kusafirisha mahabusu wao wenyewe. Tunajua kwa mamlaka uliyopewa unaweza kuongea na ngazi za juu na gari ikapatikana hapa," alisisitiza.

Akijibu malalamiko hayo, Mgumba alisema anazo taarifa kwamba kituo kidogo cha polisi hakina gari, akiahidi kulichukua suala hilo na kwenda kulifanyia kazi kwa kushirikiana na viongozi wengine ngazi za juu serikali.

Aidha, alipiga marufuku kwa wananchi hao kukata miti na kuchoma mkaa ili wasiendelee kusababisha ukame ambao kwa sasa umeanza kukabili baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Tanga.

"Hali hii ikiendelea, mwishoni hata afya na pumzi zetu tunazopumua itakuwa ni shida kwasababu uzalishaji wa hewa utakuwa mdogo, tutakuwa tukivuta hewa chafu. Hii miti ndio inayotuletea mvua sasa mkiikata mvua itakuja vipi, kama mvua haikunyesha hamuwezi kupata mazao, kinachofuata hapo ni njaa," alisema.

# Hospitali ya Bombo yahitaji damu chupa 600

**Na Oscar Assenga**, TANGA

MKUU wa Idara ya Maabara wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, Sinde Ntobu, amesema hospitali hiyo inahitaji chupa 600 za damu salama kwa mwezi kutokana na idadi ya wahitaji kuongezeka.

Amesema kiasi hicho ni kikubwa kwa sasa tofauti ni kipindi cha nyuma.

Ntobu aliyasema hayo wakati wa kampeni ya uchangiaji damu salama inayoendeshwa na Shirika la Empower Society Bulid The Nation, wananchi mbalimbali walijitokeza.

"Uhitaji wa matumizi ya damu kwa sasa ni makubwa kwa mwezi, kwa vile tunatumia kati ya chupa 500 hadi 600 kuwasaidia wagonjwa mbalimbali.

"Wengi wa wahitaji wa damu salama ni mama wajawazito na watoto wadogo. Lakini wamo wanaofanyiwa upasuaji na wenye ugonjwa wa selimundu na sikoseli.

Zaidi aliongeza: "Kuna imani potofu kwamba ukichangia damu utakuwa unachangia mara kwa mara. Dhana hiyo siyo sahihi, wengine wanasema kutoa damu utakuwa na upotevu wa damu mara kwa mara."

Alisema kwa mujibu wa viwango cha Shirika la Afya Duniani (WHO), inaelekeza kila hospitali iwe na uhakika wa damu asilimia moja kwa wakazi wa eneo husika.

Halmashauri ya Jiji la Tanga, lina watu zaidi ya 200,000 lakini ni asilimia moja ya watu hao wanaochangia damu.

Naibu Meya wa Jiji hilo, Mwanaidi Kombo, alilipongeza Shirika la Empower Society Build The Nation, kwa kuona umuhimu wa kuchagia damu, huku akiwasihi kuendeleza utaratibu huo mara kwa mara wa kusaidia wenye uhitaji.

"Pamoja na hilo tuendelee kuelimisha jamii juu ya umuhimu kujitolea kuchangia damu kwa hiari ili kuendelea kuokoa vifo ya wagonjwa mbalimbali wanaopoteza maisha kutokana na upungufu wa damu mwilini," alisema.

Ofisa Utafiti wa Shirika hilo, Isihaka Mbwana, alisema wamepanga kuja na mikakati maalum wa kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha juu ya kupambana na magonjwa mbalimbali ikiwamo ebola na polio.

Alisema: "Tumeandaa bonanza la uchangiaji damu tulilolipa jina la Asante Mama, kwa kujali na kutambua vipaji vya vijana. Lengo hasa ni kutoa elimu ya magonjwa ya ebola, polio na corona pamoja na kuhamasisha jamii kufanya mazoezi".

NIPASHE JUMATATU OKTOBA 31, 2022
Nipashe
# Spotika




NYOTA WAKUBWA KOMBE LA DUNIA 2022 EPL UK.16

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, ndiye mchezaji aliyefikisha mapema zaidi mabao tisa kwenye LaLiga katika karne hii ya 21.





# 'MKONO IKULU'!...

Kiungo wa Liverpool, Fabinho (kushoto), katika harakati za kuwania kumiliki mpira dhidi ya winga wa Leeds United, Brenden Aaronson, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Anfield na Liverpool kuangukia pua kwa kichapo cha mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**



GARETH SOUTHGATE

# MAKOCHA WANAOVUTA MSHAHARA MKUBWA KOMBE LA DUNIA 2022

**LONDON,** England

HUKU Kombe la Dunia la FIFA la 2022, likikaribia kwa kasi, mwelekeo sasa unahama kutoka kwenye klabu na makocha hadi timu za taifa na makocha wao. Kuna makocha wengi kwenye uwanja wa soka wa kimataifa ambao watakuwa mstari wa mbele kwenye mchezo huo hivi karibuni.

Kuna shinikizo kubwa kwao wanapopeleka vikundi vyao vya wanasoka wenye vipaji vya hali ya juu kwenye tukio la maonyesho ya mchezo huo maridadi. Kazi ya makocha wa timu ya taifa si rahisi.

**Kuna majina mengi yanayotambulika katika mzunguko wa kufundisha siku hizi, litakuwa jambo la kuvutia kuona ni nani anayebeba fedha nyingi nyumbani. Makala haya yanawaangalia makocha watano wanaolipwa pesa nyingi zaidi kuelekea katika Kombe la Dunia la FIFA la 2022, twende sasa...**

**#5. LOUIS VAN GAAL (UHOLANZI) - PAUNI MILIONI 2.5 KWA MWAKA**

Louis van Gaal amekuwa na kazi nzuri ya ukocha. Ana umri wa miaka 71 sasa, na hili litakuwa Kombe la Dunia la mwisho kwa kocha huyo wa zamani wa Manchester United na Barcelona.

Van Gaal amefanikiwa kufanya kazi nzuri akiwa na Timu ya Taifa ya Uholanzi tangu alipostaafu kuinoa Agosti 2021. Alichukua nafasi hiyo baada ya Frank de Boer kujiuzulu kutokana na matokeo mabaya ya timu kwenye michuano ya Euro 2020.

Van Gaal ndiye kocha wa tano wa timu ya taifa anayelipwa zaidi duniani kwa sasa na anapokea pauni milioni 2.5 kwa mwaka.

**#4. TITE (BRAZIL) - PAUNI MILIONI 3 KWA MWAKA**

Tite amekuwa kocha mkuu wa Timu ya Taifa ya Brazil tangu mwaka 2016. Aliiongoza kutwaa ubingwa wa Copa America mwaka 2019, na tayari amefichua kuwa ana nia ya kujiuzulu kama kocha wa 'Selecao' hao baada ya michuano hii ya Kombe la Dunia.

Kwa hiyo Kombe la Dunia la 2022 litakuwa la mwisho kwa Tite akiwa na timu hii ya Brazil yenye vipaji vingi. Tite amefanya kazi nzuri sana akiwa na Brazil katika miaka ya hivi karibuni na timu yake haikufungwa kwenye mechi za Kufuzu Kombe la Dunia kwa ukanda wa Amerika Kusini.

Tite ni mmoja wa makocha wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani akiwa anapokea pauni milioni tatu kila mwaka.

**#3. DIDIER DESCHAMPS (UFARANSA) - PAUNI MILIONI 3.2 KWA MWAKA**

Didier Deschamps aliiongoza Ufaransa kutwaa taji la Kombe la Dunia mwaka 2018. Walipewa nafasi kubwa ya kushinda Euro 2020 pia, lakini timu hiyo ilitolewa katika hatua ya 16-bora.

Deschamps huenda akalazimika kuwa bila nyota wake wa kati wawili, N'Golo Kante na Paul Pogba kwa kuwa hao kwa sasa ni majeruhi. Wengi wa washindi wake wa Kombe la Dunia pia wamepitwa kiwango chao. Lakini hiyo haimaanishi kuwa kuna uhaba wa vipaji au ubora katika upande wa Ufaransa.

Mshahara wa Deschamps wa kila mwaka ni pauni milioni 3.2 na hiyo inamfanya kuwa kocha wa tatu anayelipwa zaidi katika Kombe la Dunia 2022.

**#2. GARETH SOUTHGATE (ENGLAND) - PAUNI MILIONI 4.9 KWA MWAKA**

Gareth Southgate amefanya kazi nzuri akiwa na Timu ya Taifa ya England. Licha ya hali yao ya sasa, England ilitinga nusu fainali ya Kombe la Dunia la 2018.

England kwa sasa ina kikosi chenye vipaji vya hali ya juu na chenye nyota wengi na wanaweza kucheza soka la kusisimua zaidi.

Southgate anapokea mashahara wa pauni milioni 4.9 kwa mwaka.

**#1. HANSI FLICK (UJERUMANI) - PAUNI MILIONI 5.5 KWA MWAKA**

Hansi Flick alishinda mataji matatu akiwa na Bayern Munich msimu wa 2019-20. Kisha akachukua jukumu la kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani ambayo imekuwa ikipitia nyakati ngumu hivi karibuni. Aliiongoza bila kufungwa katika mechi zake 10 za kwanza akiinoa Ujerumani.

Ujerumani ilitinga hatua ya makundi katika Kombe la Dunia 2018 na kuna shinikizo kubwa kwa Flick kubadili mambo wakati huu. Flick anaingiza pauni milioni 5.5 kwa mwaka kama kocha wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na ndiye kocha anayelipwa fedha nyingi zaidi katika Kombe la Dunia la 2022.

## MICHEZO

# ALI JUMA ABDALLA;

# KIPA TEMBO WARRIORS, KIPAJI KABLA NA BAADA YA ULEMAVU



**Na Saada Akida**

ANAYETAFUTA hachoki, akichoka basi ameshapata...Lakini mwisho wa kutafuta ni pale tu utakapozima pumzi yako ya mwisho hapa duniani! Hivyo ndivyo unavyoweza kuanza kueleza pindi unapoanza kummulika Golikipa wa Tembo Warriors, Ali Juma Abdalla, namna alivyopigania kipaji chake cha soka hadi sasa.

**Na kwa namna alivyopigana hadi sasa, hii inatupa fundisho kwamba kwa kila mwenye ulemavu awe amezaliwa au amekutana nao ukubwani kwa sababu mbal imbali akiwa na kipaji bado anaweza ku-fikia ndoto zake za juu akipewa ushirikiano wa kutosha.**

Hili limedhihirishwa kwa Timu ya soka ya Taifa ya Tanzania ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors) walivyofanya vizuri ikiwa ni mara yao ya kufuzu na kucheza michuano ya Kombe la Dunia nchini Uturuki mwaka huu, ambapo ilifika hatua ya robo fainali.

Wapo wachezaji wengi waliofanikisha hilo, lakini kwa leo hapa tunaye kipa namba moja wa Tembo Warriors, Ali Juma Abdalla, ambaye ni mlemavu wa mkono (ana mkono mmoja), ana mengi ya kusisimua kuhusu maisha yake ya soka, twende sasa...

### ALIVYOANZA SOKA

"Nilianza kucheza mpira nikiwa shuleni timu za madarasa baada ya hapo nikawa nacheza timu za mtaani na timu za ligi tofauti tofauti wakati huo nilikua sijapata ulemavu wa mkono, nilikuwa na mikono yote miwili.

"Timu nilizowahi kuzichezea kabla sijapata ulemavu wa mkono Chuoni fc na Amani Fresh, pamoja na Amani Fresh FC.

"Amani Fresh wakati huo ilikuwa Daraja la Tatu kabla ya kutua Negro FC nakuwa miongoni mwa wachezaji walioipandisha hadi Daraja la Pili," anasema Ally ambaye alizaliwa Oktoba 8, 1990, Mjini Magharibi, Zanzibar na kupata elimu visiwani humo hadi Kidato cha Nne.

### KUPATA ULEMAVU

Anasema amezaliwa akiwa mzima, mikono yake ikiwa kamili, lakini harakati zake za maisha ya soka ndizo zilizomsababishia hali hiyo.

"Ulemavu niliupata nikiwa mkubwa mnamo Septemba Mosi, 2011. Wakati huo tulikuwa tunarudi nyumbani kutoka kucheza mechi, ilikua ni muda wa jioni tunatoka kijijini kurudi mjini kwa bahati mbaya tukapata ajali ya gari.

"Kuna wachezaji wengine watatu waliumia kidogo tu, lakini mimi pekee ndiye nilivunjika mkono. Nilikaa siti ya mbele wakati ile gari inaanguka ililalia upande wangu na ndipo apo ulipovunjika mkono wangu wa kushoto na kulazimika kukatwa kabisa wakati huo nilikuwa naichezea Negro FC."

### BAADA YA ULEMAVU

"Nilikuwa na kipindi kigumu sana, sikuweza kufikiria chochote zaidi ya kuwapo katika wimbi kubwa la mawazo, ilichukuwa muda zaidi ya mwaka kukubaliana na hali hiyo," anasema.

Anasema kwa kuwa ndoto zake ni kucheza soka hali ambayo ndoto hiyo aliamini tayari imepotea baada ya ajali hiyo, hivyo soka la ushindani aliona halitawezekana tena kwake.

"Ilinichukua miezi kadhaa kukubaliana na hali yangu ya ulemavu baada ya kupona, nikawa naenda kucheza mazoezi na wasio na ulemavu wowote, nikiamini njia ya kujipa furaha kwa sababu ya kupoteza ndoto zangu," anasema kipa huyo.

Anasema baada ya kipindi kifupi kufanya mazoezi na timu zingine zilizokuwa na wachezaji ambao hawana ulemavu, hakuwahi kuwaza kama kuna siku ndoto zake za kucheza soka la watu wenye ulemavu zinaweza kutokea.

### BAADA YA KUJIUNGA NA TIMU YA WATU WENYE ULEMAVU

"Nilijisikia vizuri na matumaini ya kufikia ndoto zangu niliona ni njia sasa ya kwenda kutimia kwa sababu naweza kupata nafasi ya kucheza kulingana na uwezo wangu wa kucheza nafasi nyingi.

"Nilipata nafasi ya kuitwa katika Klabu ya Drogheda FC, maskani yake iliyopo Dar es Salaam, inayoshiriki Ligi ya Watu wenye Ulemavu, ambayo nacheza nafasi ya kipa hadi sasa," anasema kipa huyo.

Anasema kabla ya kupata ajali alikuwa akicheza nafasi ya kipa, lakini akiwa na uwezo wa kucheza nafasi mbili tofauti namba tatu na 11, ila baada ya ajali akaamua kubobea katika nafasi ya kipa kwa sababu ya sheria za mchezo huo wa soka la watu wenye ulemavu.

### KUITWA TEMBO WARRIORS

Anasema mchezaji wa mchezo wowote ule, hakuna ambaye hatamani kuchezea timu ya taifa na ndivyo ilivyokuwa kwake, ndoto ambayo imetimia.

"Nilijisikia furaha sana maana nilikua natamani sana kuitumikia timu ya taifa langu kupitia kipaji changu, kitu hicho nimefanikiwa katika maisha yangu," anasema Ally.

### SAPOTI YA FAMILIA

"Kwetu tupo tisa, kati ya hao hakuna anayecheza mpira zaidi ya mimi mwenyewe, bahati nzuri nilipata ushirikiano mzuri katika familia yangu kabla ya kupata ulemavu na hata sasa hivi nikiwa katika hii hali."

### CHANGAMOTO

"Nilikutana na unyanyasaji wakati sijapata timu ya kucheza, kipindi nacheza timu za mtaani, wachezaji wa timu pinzani walinikejeli kwa ulemavu wangu na kuniambia kuwa soka ndio basi.

"Niliumia sana na kuendelea kukata tamaa ya kuwa ipo siku nitakuja kutimiza ndoto zangu za kucheza soka la ushindani," anasema Ally kwa masikitiko.

Anasema anamshukuru rafiki yake Ali Khatib, ambaye naye alikuwa mlemavu akiishi Dar es Salaam, siku moja alifika Zanzibar kwa shughuli za Chama cha Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya elimu ya ujasiriamali.

"Tulipokutana hapo aliniahidi atanisaidia kutimiza ndoto zangu, alirejea Dar es Salaam, kisha baadaye alinipigia simu na kunieleza naweza kutimiza ndoto za kucheza soka la ushindani bila unyanyasaji baada ya Tanzania kuanzisha soka la Watu wenye Ulemavu," anasema Ally.

### MECHI YA KUKUMBUKWA

"Mechi ambayo sitaweza kuisahau ni wakati nipo Negro fc dhidi ya Mgeni Haji, ilikuwa mchezo wa kirafiki wa kujiandaa na ligi ndio mechi yangu ya mwisho wakati tunarudi nyumbani nikapata ajali na kusababisha ulemavu huu nilio nao hadi sasa," anasema kipa huyo.

Anasema ndoto zake kubwa ni kucheza soka la kulipwa nje ya nchi na kuendelea kupambania nafasi ya kipa namba moja wa Tembo Warriors kwa mafanikio makubwa zaidi ya msimu huu.

### KOMBE LA DUNIA UTURUKI

"Ilikuwa ni ngumu sana hasa ukizingati ugeni niliokuwa nao katika mashindano kwani ilikua mara yangu ya kwanza kushiriki Kombe la Dunia, nilikosa uzoefu.

"Nashukuru Mungu makocha waliweza kunisaidia kwa kunipa moyo na kunipa ujasiri kwamba naweza kufanya vizuri zaidi ya makipa wa timu zilizopo hapo hali hiyo imenisaidia na kufanikisha Tembo Warriors kufika hatua ya robo fainali lakini pia Tanzania kuwa nchi ya saba katika viwango ubora vya dunia kwa timu za watu wenye ulemavu," anasema Ally.

### USHAURI KWA WAZAZI

Anasema kuzaliwa na ulemavu au kupata ulemavu haimanishi huwezi kufanya vitu vikubwa. Naamini mtu mwenye ulemavu anaweza akafanya vitu vikubwa kuliko hata asiye na ulemavu.

"Nawashauri wazazi na walezi wasiwafungie watoto wenye ulemavu, wawape elimu watambue vipaji vyao na waviendeleze maana ulemavu ni hali ya kawaida tu kwa kipindi hiki," anasema kipa huyo wa Tembo Warriors.

**NJE YA UWANJA**

HOTELI ya Cristiano Ronaldo iliyoko Marrakesh nchini Morocco (Pestana CR7 Hotel), anayoiendesha kwa ushirikiano na Pestana Hotel Group, imetangazwa kuwa Hoteli Mpya Bora Afrika katika Tuzo za Dunia za World Travel Awards 2022.



# NYOTA WAKUBWA KOMBE LA DUNIA 2022



MBAPPE

**DOHA,** Qatar

KOMBE la Dunia ni onyesho la wanasoka bora zaidi duniani, lakini michuano ya Qatar inaweza kuwa ya mwisho kwa kundi la nyota mashuhuri, pamoja na kuibuka kwa kizazi kipya cha kuvutia cha vipaji.

**Lionel Messi na Cristiano Ronaldo huenda hii itakuwa michuano ya mwisho kwa nyota hao.**

Hata hivyo, pamoja na Messi na Ronaldo wanaowania taji lao la kwanza la dunia, mabingwa watetezi Ufaransa kwa mara nyingine wataongozwa na nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

### LINAANZA LINI?

Michuano ya Kombe la Dunia itaanza katika hatua ya makundi kuanzia Novemba 20, mwaka huu, huku wenyeji Qatar wakifungua pazia la michuano hiyo kwenye Uwanja wa Al Bayt katika mchezo wa ufunguzi dhidi ya Ecuador wa Kundi A na fainali yake itafanyika Uwanja wa Lusail, Desemba 18, mwaka huu.

### RATIBA DESEMBA 2: MICHEZO YA MWISHO YA MAKUNDI

Desemba 3-6: Raundi ya 16, Desemba 9-10 Robo fainali, Desemba 13-14: Nusu fainali, Desemba 17: Mechi ya Nafasi ya Tatu, Desemba 18: Fainali.

### NYOTA WAKUBWA

Michuano iliyopita ya Kombe la Dunia ilitoa majina ya wachezaji wakubwa na hapa tunawaangalia nyota wakubwa zaidi kwenye mashindano haya.

### KYLIAN MBAPPE (UFARANSA)

Mbappe alikuwa bora kwa Ufaransa wakati kikosi cha Didier Deschamps kikinyakua taji la dunia mwaka 2018, lakini nyota huyo wa PSG amepanda kiwango kingine katika misimu miwili iliyopita na atakuwa mmoja wa wachezaji bora kwa mabingwa hao watetezi.

### LIONEL MESSI (ARGENTINA)

Mazungumzo ya kufifia kwa uwezo wa Messi ulikuwa mjadala katika miaka michache iliyopita, huku Muargentina huyo akionyesha vipaji vyake kule PSG. Macho yote yataelekezwa kwake huku akitarajia hatimaye kuongeza Kombe la Dunia kwenye orodha yake ya mataji.

### KEVIN DE BRUYNE (UBELGIJI)

De Bruyne atapewa jukumu la kuisaidia Ubelgiji kuwa na nafasi kubwa kule Qatar. Hata hivyo, Mchezaji huyo wa Manchester City ataazimia kujidhihirisha kama kiungo namba moja katika soka la dunia.

### CRISTIANO RONALDO (URENO)

Licha ya wakati wa taabu ndani ya Manchester United, matarajio bado yatakuwa makubwa kwa Ronaldo huko Qatar, wakati anashiriki katika fainali ya tano, lakini Ureno ililazimika kufanya kazi ya ziada kupitia mchujo wa kufuzu.

Hatimaye waliifunga Macedonia Kaskazini na kujihakikishia nafasi yao kwenye michuano hiyo na mabingwa hao wa Ulaya wa 2016 wataangalia tena uwezo wa Ronaldo wa kuongoza safu yao ya ushambuliaji kama nguzo kuu.

### VINICIUS JR (BRAZIL)

Licha ya shinikizo la kujiweka kama mchezaji muhimu kwa Real Madrid na Brazil katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Vinicius Jr amepanda changamoto hiyo kwa njia ya ajabu. Ushirikiano wake na Karim Benzema kule Madrid pia ana uwezo wake wa kiwango cha juu kumfanya kuwa mmoja wa majina ya nyota wa Qatar 2022.

### TAKEFUSA KUBO (JAPAN)

Akiwa na umri wa miaka 21 pekee, Takefusa Kubo tayari amejitengenezea jina lake kabisa - baada ya kuibuka na lebo ya 'wonderkid' kwenye LaLiga akiwa na Barcelona na kisha Real Madrid. Kiungo huyo wa Kijapani alihamia Real Sociedad katika dirisha la usajili la majira ya joto mwaka huu (ingawa Real wamebakisha umiliki wake kwa asilimia 50, na wanaweza kumrejesha kwenye mji mkuu wa Hispania hadi 2025) na anathibitisha mara kwa mara uwezo wake uwa mchezaji muhimu kwa Japan.

### VIRGIL VAN DIJK (UHOLANZI)

Licha ya kucheza nafasi ya safu ya ulinzi ya Liverpool, Van Dijk hajawahi kushiriki Kombe la Dunia akiwa na taifa lake. Waholanzi wana nguvu zaidi kwenye safu ya nyuma na katikati kuliko ilivyokuwa miaka ya hivi karibuni, Van Dijk atakuwa na lengo la kuimarisha kundi la wachezaji bora katika nafasi yake kwenye soka duniani.

### NEYMAR (BRAZIL)

Mbrazil huyu anaendelea kubeba mzigo wa matumaini ya nchi yake kwenye hatua kubwa zaidi, na Qatar 2022 haitakuwa tofauti. Taifa linatarajia wakati wowote Neymar atakapovaa jezi na atakuwa na hamu ya kuwaongoza 'Selecao' hao kutwaa taji lao la kwanza la dunia tangu mwaka 2002.

### PEDRI (HISPANIA)

Nyota wa 'La Roja', Pedri ndiye kiungo bora zaidi kwenye safu ya kiungo ya Hispania, ambayo hapo awali imewatoa Sergio Busquets, Andres Iniesta na Xavi. Lakini, kuna maoni kule Camp Nou kwamba, Pedri siku moja anaweza kuwazidi watangulizi wake wa Barcelona na atatafuta kuendeleza mafanikio mazuri kwenye Euro 2020.

### KARIM BENZEMA (UFARANSA)

Uamuzi wa Deschamps wa kumuondoa Benzema kwenye michuano ya Euro 2020 ulikabiliwa na jibu tofauti la umma nchini Ufaransa, 'Les Bleus' walipotoka katika michuano hiyo katika hatua ya 16-bora. Na sasa ana nafasi kubwa kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

### LUKA MODRIC (CROATIA)

Modric ana uwezekano wa kuwafuata wachezaji kama Ronaldo, Messi na Benzema katika kumaliza muda wa kucheza soka la kimataifa baada ya Kombe la Dunia, lakini kiungo huyo mwenye umri wa miaka 37, atadhamiria kuiongoza Croatia kupata mafanikio pale Qatar, na licha ya umri wake kuwa mkubwa, anabakia kuwa nyota muhimu kwa nchi hiyo.

### ALPHONSO DAVIES (CANADA)

Canada wamefuzu Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu nchini Mexico mwaka 1986. Mwitikio wa kihisia wa mchezaji huyo wa Bayern Munich kwenye mitandao ya kijamii kwa Canada kupata nafasi yao Qatar ulionyesha umuhimu wake na atakuwa na hamu ya kung'ara kwenye hatua kubwa zaidi.

### CHRISTIAN PULISIC (MAREKANI)

Kama Marekani itahitaji kufika mbali zaidi katika mashindano hayo, watamhitaji Pulisic kuwaongoza. Mchezaji huyo wa Chelsea amekuwa kinara wa kampeni zao za kufuzu, na atatumaini kuchukua uzoefu wake wa mechi kubwa katika ngazi ya klabu hadi kwenye hatua ya dunia akiwa chini ya Kocha, Gregg Berhalter.

### SON HEUNG-MIN (KOREA KUSINI)

Son ameonyesha mara kwa mara katika maisha yake yote akiwa na Tottenham Hotspur kwenye Ligi Kuu England, kwamba ana uwezo wa kuwa na kipaji cha kipekee, akifunga baadhi ya mabao ya kuvutia zaidi kwenye ligi. Katika kiwango cha kimataifa ana mabao zaidi ya 30 kwa jina lake, na atakuwa miongoni mwa washambuliaji wanaotarajiwa kung'ara.

### HARRY KANE (ENGLAND)

Nahodha wa England Kane atakuwa mtu muhimu kwa kikosi cha kocha, Gareth Southgate huku 'Simba Watatu' hao wakipania kuendeleza kiwango chao. Kane alijiimarisha katika kiwango cha juu katika kipindi cha pili cha msimu wa 2021/22 wa Ligi Kuu England.

### NYOTA WATAKAOKOSA KOMBE LA DUNIA

Wakati Messi, Neymar, Kane na wengine wote watakuwa kwenye ndege kuelekea Mashariki ya Kati, majina kadhaa ya nyota yatalazimika kuridhika na kutazama mchezo huo yakiwa nyumbani.


Italia ilishindwa kufuzu mbele ya Macedonia Kaskazini na hiyo inamaanisha kwamba, Jorginho, Marco Verratti na wachezaji wenzao walioshinda Euro 2020 hawatakuwapo Qatar.

Mohamed Salah hatakuwapo pia, kwani nyota huyo wa Liverpool na Misri alishindwa katika mechi yao dhidi ya Senegal ya kuwania kufuzu katika Kanda ya Afrika, kwenye marudio ya fainali ya AFCON 2022.

Orodha ya waliothibitishwa kutokuwapo pia inajumuisha majina mengine kama Erling Haaland (Norway), Pierre-Emerick Aubameyang (Gabon), Naby Keita (Guinea) na Edin Dzeko (Bosnia), wote wakibakia nyumbani baada ya nchi zao kushindwa kufuzu.

## Nukuu

"Huwezi kufuzu Ligi ya Mabingwa ikiwa unacheza bila ulinganifu kama tunavyofanya kwa sasa. Tunapaswa kurekebisha hilo. Kisha tutaona wapi tutamaliza. Sote tunajua kwamba mambo mengi yanawezekana, lakini kwa hilo tunapaswa kushinda michezo ya soka ambayo hatujafanya hivyo mara nyingi," **Kocha Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya kipigo cha mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Leeds United juzi.**




"Hakuna mashabiki wengi wa United ambao kwa sasa wangekuwa na Ronaldo [Cristiano] kwenye kikosi chao cha kwanza. Ni bora bila yeye - wanafunga mabao mengi bila yeye na wanashinda pointi nyingi bila yeye. United ni timu bora bila yeye," **mchezaji wa zamani wa Manchester United na mchambuzi wa soka kwa sasa, Gary Neville.**



"Ndani yangu mimi ni Mghana, na ninajivunia kuwa Mwafrika. Lakini bila shaka mimi ni Muitaliano. Nilizaliwa Italia. Sijawahi kufika Afrika katika maisha yangu, lakini nitakwenda siku moja," **Mshambuliaji wa FC Sion, Mario Balotelli**






Kocha Denis Lavagne aliyetimuliwa hivi karibuni na Klabu ya Azam.

# 'KIMBUNGA' KIVYOPITA NA MAKOCHA LIGI KUU

Na Adam Fungamwangu

KABLA hata ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara haujamalizika, kumekuwa na mlolongo wa makocha kutimuliwa kutokana na timu kufanya vibaya.

**Kutokana na uwekezaji wa klabu mbalimbali kwa kununua wachezaji kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa, mishahara, posho na maandalizi, viongozi wamekuwa si wavumilivu pale wanapoona timu zao hazifanyi vizuri.**

Kwa sasa Ligi ya Tanzania imekuwa ni moja kati ya ligi ngumu licha ya changamoto za hapa na pale, baadhi ya timu ambazo zilikuwa zimezoea kushinda kirahisi zimejikuta zikipata wakati mgumu.

Ukiondoa Kocha Mkuu wa Simba, Zolan Maki, ambaye yeye aliondoka katika timu hiyo ikiwa imecheza mechi chache tu na sababu zikiwa wazi ni kupata timu nyingine ya Al Ittihad ya Misri, aliondoka huku timu yake ikiwa haijapoteza, waliobaki wametimuliwa kwa sababu za timu walioziongoza kufanya vibaya.

Azam inaongoza kwa kutimua makocha wawili kwenye msimu mmoja, ikiwa hata mzunguko wa kwanza haujamalizika, huku kocha Mfaransa Denis Lavagne akiweka rekodi ya kuongoza timu kwa muda mfupi tu. Wafuatao ni makocha waliotimuliwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mkapa sasa ikiwa raundi ya tisa...

**ABDIHAMID MOALIN - AZAM**

Kocha huyo aliyepewa mkataba baada ya kuiongoza Azam kwa mechi kadhaa za msimu uliopita na kushinda, alitimuliwa Agosti mwaka huu baada ya timu hiyo kufanya vibaya kwenye mechi za mwanzo tu za Ligi Kuu.

Aliletwa Azam FC kama Mkurugenzi wa Ufundi kwenye kituo cha kukuza vipaji, lakini baada ya kutimuliwa kwa Kocha George Lwandamina, Moalin alikaimu nafasi hiyo ukocha mkuu kwa mwezi mzima kabla ya kuthibitishwa kuwa kocha mkuu mwezi Januari mwaka huu.

Alihusika kwenye usajili na maandalizi ya msimu mpya, lakini timu yake haikuwa na mwanzo mzuri kwenye ligi, akaonyeshewa mlango wa kutokea na kupelekwa kwenye kazi ambayo alikuwa nayo awali.

**MASOUD DJUMA - DODOMA JIJI**

Oktoba mwaka huu, Klabu ya Dodoma Jiji ilimfungashia virago kocha wake mkuu, Mrundi Masoud Djuma baada ya matokeo mabovu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Masoud ambaye naye kama Moalin, aliingia kwenye timu ya Dodoma Jiji katikati ya msimu, akichukua nafasi ya kocha mwingine aliyefukuzwa, Mbwana Makata.

Naye pia alihusika kwenye usajili na maandalizi ya ligi, lakini ilipoanza timu ilikuwa inaambulia vipigo kiasi cha viongozi kuamua kumtimua yeye na benchi lake lote la ufundi na sasa Mmarekani Melis Medo amechukua nafasi yake.

**DENIS LAVAGNE - AZAM**

Kocha huyu Mfaransa aliajiriwa na Azam FC baada ya kutimuliwa kwa Abdihamid Moalin Agosti mwaka huu.

Mwezi uliofuata, Septemba, Azam ilimshusha kocha huyo na kuiongoza kwa michezo sita tu, ikipata ushindi mara tatu na kupoteza tatu. Kati ya mechi hizo nne ni za Ligi Kuu na mbili za michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Baada ya kutolewa kwenye kombe hilo, ikifungwa mabao 3-0 dhidi ya Al Akhdar ya Libya na kushinda nyumbani 2-0, siku chache tu baadaye uongozi wa klabu hiyo ukatangaza kuvunja naye mkataba, na hii ni baada ya kufungwa mabao 2-1 dhidi ya KMC kwenye mechi ya Ligi Kuu, Oktoba 21. Lavagne ndiye kocha aliyedumu kwa muda mfupi zaidi mpaka sasa, akiifundisha timu hiyo kwa muda usiozidi mwezi mmoja tu.

**JOSLIN SHARIF - POLISI TANZANIA**

Wiki iliyopita, Klabu ya Polisi Tanzania ilitangaza kumtimua kocha wake, Joslin Sharif raia wa Burundi baada ya matokeo mabaya ya muda mrefu ya timu hiyo.

Kocha huyo aliyeingia mkataba na klabu hiyo Julai mwaka huu, aliondolewa yeye na benchi lake la ufundi baada ya uongozi wa klabu hiyo kuwaita kutoka jijini Mbeya na kwenda Moshi mkoani Kilimanjaro kwenye Makao Makuu ya klabu kwa ajili ya mazungumzo yanayohusiana na mwenendo wa timu.

Ni mazungumzo yaliyofikia mwafaka wa kuamua kuacha na ambapo sasa kikosi kinanolewa na John Tamba, Kocha Msaidizi wa timu hiyo.

**FRANCIS BARAZA - KAGERA SUGAR**

Klabu ya Kagera Sugar nayo imeamua kumwachisha kazi kocha wake, Francis Baraza kwa kile kile ambacho kinaitwa mwendo usioridisha kwa timu hiyo msimu huu, nayo imekuwa kwenye mwendo ambao haujazoeleka na mashabiki wengi nchini.

Kocha huyo maarufu na mwenye heshima kubwa nchini, alijiunga na timu hiyo Machi mwaka jana akitokea Biashara United ambako aliipa timu hiyo mafanikio.

Baraza aliingia mkataba wa miaka miwili na nusu na klabu ya Kagera Sugar, hivyo ameutumikia kwa takriban mwaka mmoja na nusu.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinalidai huenda kocha wa zamani wa klabu hiyo, Mecky Mexime akarejeshwa tena kuifundisha timu hiyo.

NDANI YA 18



KIUNGO wa zamani wa Manchester United na Kocha Mkuu wa sasa wa Timu ya Taifa ya Wales, Ryan Giggs, ndiye anayeshikilia rekodi ya kutoa pasi nyingi za mwisho 'assists' kwenye Ligi Kuu ya England, akifanya hivyo mara 162, akifuatiwa na Cesc Fabregas (111), Wayne Rooney (103), Frank Lampard (102) na Kevin De Bruyne (95).

# SOKA




**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Victor James Osimhen
**KUZALIWA:** Desemba 29, 1998 (miaka 23)
**ALIPOZALIWA:** Lagos, Nigeria
**KIMO:** 1.86 m (6 ft 1 in)
**NAFASI:** Mshambuliaji
**KLABU:** Napoli
**JEZI NAMBA:** 9
**MABAO:** Saba (Kinara wa mabao Serie A)

Nipashe

# Spotika

KOMBE la Dunia ni onyesho la wanasoka bora zaidi duniani, lakini michuano ya Qatar inaweza kuwa ya mwisho kwa kundi la nyota mashuhuri, pamoja na kuibuka kwa kizazi kipya cha kuvutia cha vipaji.

Uk. 16-17



# WACHEZAJI WA5 WENYE KASI ZAIDI UWANJANI EPL

**LONDON,** Uingereza

LIGI Kuu England (EPL), inajulikana kwa asili yake ya kasi na kwa hiyo imekuwa na wachezaji wenye kasi zaidi kwa miaka mingi.

**Theo Walcott, Aaron Lennon, Leroy Sane, Adama Traore, na Kyle Walker ni miongoni mwa baadhi ya wachezaji wenye kasi zaidi katika historia ya ligi hiyo.**

Kama tunavyojua, kasi ni uwezo muhimu sana kwa wanasoka wa hali ya juu, kwani asili ya mchezo inahitaji kukimbia sana.

Hata mwaka 2022, hali ya sasa bado haijabadilika katika Ligi Kuu kwani bado kuna wachezaji wengi wenye kasi.

Makala haya yanaangalia wachezaji watano waliorekodi kasi ya juu zaidi kwenye ligi hiyo msimu huu, shuka nayo sasa...

**#5. JACK STACEY - BOURNEMOUTH**

Beki wa Bournemouth, Jack Stacey, kwa sasa ni mmoja wa wachezaji wenye kasi zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Raia huyo wa England mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na klabu hiyo mwaka 2019 akitokea Luton Town kwa ada ambayo haijawekwa wazi. Pia amewahi kuzichezea klabu za Reading, Exeter City, Carlisle United na Barnet.

Stacey hadi sasa amerekodi kasi ya juu ya kilometa 35.6 kwa saa katika msimu huu unaoendelea wa ligi wa 2022-23. Kwa hiyo inamfanya kuwa mchezaji wa tano kwa kasi zaidi kwa sasa.

**#4. ALLAN SAINT-MAXIMIN - NEWCASTLE UNITED**

Mfaransa huyo anachukuliwa kuwa mmoja wa mawinga bora katika Ligi Kuu England kutokana na tabia yake ya kukimbia sana kutoka winga zote za Newcastle United.

Allan Saint-Maximin ni mkimbiaji hodari ndani na nje ya mpira. Pia ana uwezo bora wa kubeba mpira na anashika nafasi ya juu kati ya wachezaji wanaocheza chenga za kusisimua zaidi.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 25, hadi sasa amerekodi kasi ya juu ya kilometa 35.7 kwa saa msimu huu, na kumfanya kuwa mchezaji wa nne mwenye kasi zaidi.

Amefunga bao moja na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi tano alizoichezea Newcastle United msimu huu wa ligi.

**#3. DIOGO DALOT - MANCHESTER UNITED**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, anatajwa kuwa mmoja wa mabeki wa pembeni wanaotegemewa zaidi kwenye Ligi Kuu kutokana na uwezo wake mkubwa.

Diogo Dalot amejiweka kuwa chaguo la kwanza la beki wa kulia wa Manchester United chini ya Erik ten Hag msimu huu.

Amecheza mechi zote 10 za ligi za 'Mashetani Wekundu' hao msimu huu, akishika nafasi ya tatu kwa kasi kubwa uwanjani akikimbia kilometa 35.8 kwa saa.

**#2. GABRIEL MARTINELLI - ARSENAL**

Mchezaji mwingine ambaye anaingia kwenye orodha ya wachezaji wa Ligi Kuu ambao wamerekodi kasi zaidi msimu huu ni winga wa Brazil, Gabriel Martinelli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, kwa sasa anafurahia kampeni ya soka yenye tija akiwa na Arsenal, ambao kama jana wameshinda mechi yao dhidi ya Nottingham Forest wamerejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Hadi sasa amefunga mabao manne ya kuvutia kwenye ligi akiwa na 'Washikabunduki' hao, huku akisajili pasi mbili za mabao kwa wachezaji wenzake kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Nottingham Forest.

Pia anajulikana kwa kasi yake, Martinelli amerekodi kasi ya juu ya kilometa 35.9 kwa saa msimu huu, na hivyo kumfanya kuwa wa pili kwa kasi kwa sasa.

**#1. DARWIN NUNEZ - LIVERPOOL**


Mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez, alikuwa mmoja wa wachezaji wa hadhi ya juu waliosajiliwa kujiunga na timu za Ligi Kuu msimu huu wa majira ya joto.

Kumbuka kwamba Liverpool walipa ada ya uhamisho ya rekodi ya klabu pauni milioni 85 ili kumsajili mshambuliaji huyo kutoka Benfica.

Nunez anafahamika kwa ukimbiaji wake mkali na uwezo wa ajabu wa kupachika mabao, jambo ambalo linamfanya kuwa 'jinamizi' kwa mabeki wa timu pinzani.

Hadi sasa amerekodi kasi ya juu ya kilometa 36.5 kwa saa, ambayo inamfanya kuwa mchezaji mwenye kasi zaidi kwenye ligi hiyo kwa sasa. Nunez amefunga mabao matatu na kusajili bao moja katika mechi saba za ligi akiwa na Liverpool.

**JE, WAJUA?**



BAO la Gabriel Martinelli baada ya sekunde 58 dhidi ya Liverpool Oktoba 9, mwaka huu, linashika nafasi ya pili kwa kuwa la haraka zaidi kuwahi kupatikana katika mechi za nyumbani za Arsenal kwenye Ligi Kuu England, tangu Oktoba 2011 (Robin van Persie, alipofunga sekunde ya 29 dhidi ya Sunderland). Pia ndilo la mapema zaidi ambalo Arsenal imewahi kufunga dhidi ya Liverpool kwenye ligi hiyo.



# TUCTA yatakiwa kuwapeleka viongozi wao chuoni kunolewa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VYAMA vya wafanyakazi nchini vimeshauriwa kuwapeleka viongozi wao katika Chuo cha Wafanyakazi kilichoko jijini Mbeya ili wapate mafunzo ya uongozi yatakayowasaidia kuendesha vizuri vyama hivyo ikiwamo kuondoa migogoro.

Wito huo umetolewa na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa kamati tendaji ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU). Pamoja na mambo mengine alitoa ushauri kwa taasisi za umma nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kuwapeleka viongozi wa TUCTA kwenye chuo hicho.

Nyamhokya alisema chuo hicho kinasaidia kuondoa ama kupunguza migogoro kwenye vyama vya wafanyakazi na maeneo ya kazi kutokana na kila kiongozi wa chama kujua mipaka ya majukumu yake.

Alisema chuo hicho ni kikongwe na kimesaidia kuwatengeneza viongozi mbalimbali ambao baadhi yao wako serikalini akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye aliwahi kuwa kiongozi wa vyama hivyo vya wafanyakazi.

"Kwa hiyo, ninaviomba vyama vyote vya wafanyakazi ambavyo vipo kwenye shirikisho na ambavyo vipo nje ya shirikisho, viwalete viongozi wao hapa ili wapate mafunzo ya namna bora ya kuviendesha vyama vyetu," alisema Nyamhokya na kuongeza.

"Lakini nawaomba viongozi wenzangu ambao hawajapita kwenye chuo hiki waje wapate mafunzo, mimi mwenyewe nilipata mafunzo hapa mwaka 2001 kwa muda wa mwezi mmoja," aliongeza.

Makamu Menyekiti wa TALGWU Taifa, Romward Mwashiuya, alisema chama hicho kimekuwa kikitenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuwapeleka viongozi wa ngazi mbalimbali kwenye chuo hicho ili kuwajengea uwezo. Alisema mafunzo hayo yamewasaidia kuwa na utaratibu mzuri wa kuongoza wanachama pamoja na kuwawezesha wanachama kuwa na utaratibu mzuri wa kudai madai yao kutoka kwa wajiri kwa kutumia njia za majadiliano. Alisema kwa mwaka huu walitenga bajeti kwa ajili ya kuwapeleka viongozi wa kamati tendaji na kwamba wataendelea na utaratibu huo ili kuhakikisha wanakuwa na viongozi bora na wenye kujua mipaka ya majukumu yao.

"Tunaushukuru sana uongozi wa chuo chetu hiki kwa kutupatia mafunzo haya, mafunzo haya yametusaidia sana kuwa na chama bora ambacho sasa kinakimbiliwa na wanachama wengi wapya ambao wanafurahia huduma," alisema Mwashiuya.

Baadhi ya wajumbe wa kamati tendaji walisema mafunzo waliyoyapata yatawasaidia katika uongozi na kuhakikisha wanapigania haki za wafanyakazi kwa kufuata misingi bora.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (TUCTA), Tumain Nyamhokya (kushoto), akimkabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo ya uongozi mmoja wa wajumbe wa Kamati Tendaji ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# H'shauri Mbeya yaanza ujenzi madarasa shule za sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya imeanza ujenzi wa madarasa 29 katika shule za sekondari wilayani humo, ili kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza watakaochaguliwa wanaanza masomo kwa wakati.

Uzinduzi wa ujenzi wa madarasa hayo ulifanyika mwishoni mwa wiki katika Shule ya Sekondari Juhudi iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambayo ni miongoni mwa shule zinazonufika na ujenzi huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema wamepoa Sh. milioni 580 kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema kwa mujibu wa maelekezo waliyopewa ni kwamba wanatakiwa kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo kabla ya Desemba 15, mwaka huu.

Alisema watakamilisha ujenzi wa madarasa hayo kabla ya Novemba 10, mwaka huu. Katemba alisema kati ya madarasa 29 wanayotakiwa kuyajenga kwenye halmashauri hiyo, asilimia 60 yameshafikia hatua ya uwezekaji na machache yapo kwenye hatua ya msingi.

"Tunataka mpaka kufikia Novemba 10 tuwe tumekamilisha ili tujipange kwa mambo mengine, mpaka sasa yapo madarasa ambayo mafundi wameanza kupiga mbao na kasi yetu ni kubwa sana," alisema Katemba.

Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Mbeya, Mwalimu Aliko Mbuba, alisema wanatarajia kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 8,971.

Alisema kutokana na idadi hiyo kunatakiwa kuwa na madarasa 180 na viti 8,971, kwamba kwa sasa madarasa yaliyoko ni 151 na madawati ni 8,001.

Alisema fedha walizopokea kwa ajili ya ujenzi wa madarasa zitatosha kununua viti 1,450 kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wa shule husika.

# Zawadi za NMB zakwamua wateja

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa nne wa kampeni ya NMB MastaBata umeanza baada ya promosheni hiyo ya kuchagiza malipo kidijitali kuzinduliwa Mbeya mwishoni mwa wiki huku sehemu ya zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 350 ikipangwa kutumika kuwawezesha wateja kiuchumi.

Sh. milioni 173 na pikipiki 14 zitatumika kuwakwamua kiuchumi washindi wa shindano hilo linalojulikana kama NMB MastaBata, Kote-Kote

Kwa mujibu wa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, utaratibu huo utasaidia kuimarisha vipato vya wateja watakaoibuka washindi.

Akifafanua zaidi, kiongozi huyo alisema MastaBata ya mwaka huu itaua ndege wawili kwa jiwe moja, ikihamasisha matumizi zaidi ya kadi za NMB Mastercard and Masterpass QR (lipa mkononi) na kuwapa fursa wateja kuboresha hadhi zao kiuchumi.

"Tofauti na mwaka jana, mwaka huu tumeamua kuwa na zawadi ya fedha pamoja na pikipiki sababu tunahitaji sio tu kuhamasisha matumizi ya kadi lakini kuwa chachu ya mabadiliko ya kiuchumi ya wateja wetu, tunaamini pikipiki hizi zinakwenda kutumika katika biashara na kuongeza kipato cha washindi wetu," Mponzi alibainisha.

Zawadi kubwa itakayohitimisha kampeni ya NMB MastaBata, Kote-Kote ni washindi saba kujishindia tiketi za kusafiri kuelekea Dubai pamoja na wenzi wao kwa siku nne.

Pia zitakuwapo droo za kila wiki na kila mwezi na shindano hilo litaendeshwa kwa wiki 10.

"Jumla ya Sh. milioni 350 zitatolewa kama zawadi kwa washindi 854," Mponzi alisema na kubainisha kuwa shughuli hiyo ni miongoni mwa mikakati yao ya kurudisha sehemu ya faida inayopatikana kwa wateja.

Kupitia zawadi hizo, NMB inataka na msimu unaokuja wa Krismasi na Mwaka Mpya kufana zaidi kwa wateja wake kwa kuwa kila wiki wateja 75 watajishindia Sh. 100,000 kila mmoja.

"Jumla watanyakua Sh. milioni 7.5 na shindano litakapotamatika Januari 2023 zawadi hiyo itakuwa imefikia Sh. milioni 75. Kila baada ya siku 28 kwa miezi miwili mfululizo washindi 49 wataibuka na Sh. milioni moja kila mtu ambazo ni sawa na Sh. milioni 49 kila droo na Sh. milioni 98 kwa droo zote mbili.

"Kila wiki kutakuwa na zawadi ya pikipiki moja na mbili kila mwezi na jumla zitakuwa pikipiki 14 kampeni itakapomalizika," alisema.

Mgeni rasmi wakati wa uzinduzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa, Juma Homera.

Kiongozi huyo alisema uwekezaji ambao NMB inaufanya ni sahihi kwa ulimwengu wa sasa wa kidijitali na uchumi wa dunia unaoendelea kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

Chuachua alisema kupitia NMB, Mbeya na Tanzania yote kwa ujumla imepata mshirika wa dhati wa maendeleo aliye tayari kuchangia ustawi wa jamii.



# Wataalamu bingwa 524 sekta afya wasomeshwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesomesha wataalamu bingwa 524 kwa katika kipindi cha miaka miwili 2020/21 na 2021/22 wanaoendelea na masomo kwenye vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuimarisha huduma za kibingwa na bobezi nchini.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango wa serikali ya awamu ya sita kuendeleza watumishi wa sekta ya afya katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi nchini.

Alisema lengo ni kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopata rufani za matibabu nje ya nchi.

Ummy alisema wizara hiyo imejiwekea lengo la miaka mitano (2020-2025) la kusomesha wataalamu bingwa na bobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha.

Alifafanua hadi kufikia Desemba 2021, mahitaji ya wataalamu bingwa katika hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na kibobezi nchini yalikuwa 1,782 wakati huo serikali ilikuwa imeshawasomesha wataalamu 992 wa fani mbalimbali za kibingwa na kibobezi.

"Hatua hii imewezesha uboreshaji wa huduma za afya za kibingwa na bobezi katika hospitali mbalimbali nchini hali inayochangia kuimarika kwa huduma za matibabu nchini na idadi ya wagonjwa wanaopata rufani ya matibabu nje ya nchi imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka."

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya jitihada mbalimbali za kuboresha huduma za kibingwa na bobezi kwa kuongeza bajeti ya kuwaendeleza watumishi wa sekta hiyo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 serikali imeongeza fedha za kusomesha wataalamu bingwa na bobezi hadi kufikia Shilingi bilioni nane kutoka Shilingi bilioni tatu za mwaka wa fedha 2021/22.

"Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na bobezi nchini kuanzia mwaka huu wa fedha, wizara imeanzisha mkakati mpya wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa sekta ya afya.

Kupitia utaratibu huu, utahusisha kusomesha timu za wataalamu wanaohitajika kwa ajili ya kukamilisha utoaji huduma za kibingwa na bobezi," alisisitiza.

Alisema utaratibu huo umeanzishwa ili kuhakikisha huduma za kibingwa zinazotolewa zinakuwa na wataalamu wote wanaohitajika ili huduma husika iweze kutolewa kwa ukamilifu.

Alisema watumishi hao wanapochaguliwa kwenda kusoma wanakuwa kwenye seti ya wataalamu wa fani mbalimbali watakaokamilisha huduma husika mfano matibabu ya upandikizaji figo (Renal Transplant) na matibabu ya saratani (Oncology).

"Mfano wataalamu watakaosomeshwa kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu ya figo kikamilifu katika seti ni daktari bingwa wa upasuaji figo, matibabu ya figo, utoaji dawa ya usingizi kwa wagonjwa wa figo, wa mionzi, muuguzi bingwa wa mionzi, mteknolojia mionzi, muuguzi bingwa wa figo, muuguzi bingwa wa usimamizi wa huduma za chumba cha upasuaji kwa wagonjwa wa figo na mtaalamu wa vifaa tiba vinavyotumika kwa ajili ya matibabu ya figo," alisema.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia mpango wa kufadhili watumishi wa afya katika fani za ubingwa na ubobezi, wizara itatoa ufadhili wa mafunzo ya seti yaliyowasilishwa na taasisi mbalimbali katika maeneo ya kibobezi na kibingwa kupitia mpango huo.

Jumla ya watumishi 139 wamechaguliwa kupata ufadhili wa masomo na kati ya hao 136 watasomeshwa nje ya nchi na watatu ndani ya nchi.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kukubali kuongeza fedha kiasi cha Shilingi bilioni nane zitakazotumika kugharamia wataalamu waliochaguliwa kusoma mafunzo haya kwa lengo la kuwa na wataalamu wa kutosha kukamilisha mahitaji ya utolewaji wa huduma katika fani husika za kibingwa na bobezi.

## Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi kutangazwa leo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kutangaza matokeo ya sensa ya watu na makazi iliyofanyika Agosti, mwaka huu.

Mwongozo wa matumizi ya takwimu za sensa utazinduliwa ili kuanza kutumika kwa ajili ya mipango ya maendeleo kwa serikali na taasisi zingine.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, jijini hapo.

Simbachawene alisema uzinduzi huo utahudhuriwa na viongozi wakuu wa kitaifa kutoka Tanzania Bara na visiwani wakiwamo marais wastaafu na mabalozi.

Alisema sensa hiyo ilihusisha takwimu za vitu vingi na kwa siku hiyo Rais atatangaza matokeo ya sensa ya watu na makazi huku matokeo ya takwimu za vitu vingine yanatolewa kwa awamu.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hamza Hassan Juma, alisema watakuwa na ujumbe wa watu zaidi ya 150 watakaoshiriki siku hiyo.

Juma alisema sensa ya mwaka huu ilifanikiwa kwa kiwango cha juu kwa sababu ya kuungwa mkono na viongozi wa kisiasa na kidini.

Vile vile, viongozi walishirikiana na serikali ya Muungano na Zanzibar kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa na matokeo hayo yatakuwa ni halisi.

Pia alisema matokeo hayo yatasaidia serikali na taasisi zingine kupanga mipango ya kuwahudumia wananchi.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkomi (kushoto), akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa pili wa Mnrt Saccos Ltd uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, (kulia) ni Mwenyekiti wa Saccos, Wilfred Msemo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TBA yataka miradi ujenzi ikamilishwe kwa wakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Ushauri ya Wakala wa Majengo nchini (TBA), imepongeza utekelezaji wa miradi mbalimbali inayojengwa na wakala huo jijini hapo, huku ikitaka ikamilishwe kwa wakati kulingana na matakwa ya mikataba.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa jengo la Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), jengo la Shirika la Umeme nchini (TANESCO), nyumba za viongozi kisiasa, la utumishi na ujenzi wa nyumba 3,500 za watumishi katika eneo la Nzuguni jijini humo.

Akizungumza baada ya kutembelea miradi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Ombeni Swai, alisema utekelezaji wa miradi hiyo ya serikali inaendelea vizuri.

"Tunapongeza TBA kwa sehemu kubwa kwa kazi waliyofanya kuna miradi ambayo ipo hatua za mwisho kukamilika na mingine inasubiri wahusika wahamie kwenye majengo yao, tumeona ubora wa kazi ni mzuri na ushirikiano wa watendaji wa TBA," alisema.

Alisema wanatumai sehemu zilizobaki kwenye miradi waliyotembelea zitakamilika kwa wakati.

"Tunaendelea kusukuma menejimenti ifanye kila linalowezekana kuhakikisha tarehe iliyopangwa kukamilisha hii miradi zinakamilika," alisema.

Kadhalika, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuipa miradi TBA na kuomba serikali iendelee kuwathamini na kuwapa miradi mingine mikubwa ya kitaifa kutokana na uwezo wa ujenzi iliyonayo TBA.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TBA, Daudi Kondoro, alisema ushauri waliopewa na bodi hiyo wameupokea na wataufanyia kazi. "Tumepata maelekezo mbalimbali binafsi nimeyachukua kwa maana ya kuyafanyia kazi tutakutana na wenzetu ili tuweze kutafsiri kwa vitendo," alisema.

Meneja Wakala wa Majengo (TBA) Mkoa wa Dodoma, Victor Bartazari, alisema wametembelea mradi wa Wakala wa Misitu ambao wanajenga jengo la kanda.

Alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 85 na unatarajiwa kukabidhiwa Novemba 27, mwaka huu.

Pia alisema wametembelea mradi wa TANESCO ambao umefikia asilimia 97 ya utekelezaji na ifikapo Novemba 22, mwaka huu jengo hilo liwe limekamilika.

Alisema wametembelea ujenzi wa nyumba 20 za viongozi kwenye eneo la Kisasa ambao unafanyika katika maeneo mawili.

Alisema kwa ujenzi wa eneo A, umekamilika kwa asilimia 100 na nyumba hizo zimekabidhiwa viongozi na wamenza kuishi.

"Kwenye upande wa eneo B nyumba zipo sita nazo zimekamilika kwa asilimia 90 tunategemea ifikapo mwisho wa mwezi huu majengo hayo yawe yamekamilika kwa ajili ya matumizi," alisema.



# Serikali kufuta sheria zinazokwaza ukuaji TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali ipo tayari kufuta sheria zinazokwaza ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema pia ipo tayari kusikiliza na kushauriana na wadau kufanya maboresho ya sheria na miongozo mbalimbali ili kama kuna sheria za ovyo zifutwe.

Aliyasema hayo juzi mjini hapo wakati akifunga kongamano la sita la TEHAMA, alipowakilishwa na Waziri wa Habari, Nape Nnauye.

Alisema huduma za intaneti ni haki ya kibinadamu ni vyema Watanzania wote wakapata haki hiyo bila ya kuachwa mtu nyuma.

Alisema serikali imedhamiria kutumia mabadiliko ya kidigitali ndani ya uchumi wa buluu ili kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii.

Alisema ili kuharakisha mabadiliko ya kidigitali katika jamii lazima kuwe na ujenzi wa umahiri wa kidijiti kwa wananchi, kuongeza usalama wa kimtandao, kupeleka huduma ya mawasiliano yenye gharama nafuu kwa wananchi, kujenga uchumi madhubuti wa kidijitali na kuimairisha utafiti, ubunifu na ujasiriamali katika sekta ya TEHAMA.

"Iwapo tutayatilia mkazo mambo haya yatatuwezesha kufikia mapinduzi ya kidigitali na serikali tumedhamiria kutumia mabadiliko ya kidigitiali ndani ya uchumi wa buluu ili kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi katika nchi," alisema.

Alisema miundombinu ya TEHAMA ni uti wa mgongo wa maendeleo ya kiuchumi na serikali inatekeleza miradi mbalimbali yenye kuhakikisha Tanzania inakua na miundombinu iliyo rafiki na kuwaunganisha watu walio katika maeneo ya pembezoni.

Alisema hatua hiyo itachangia hatua za wananchi katika uchumi wa kidijitali na TEHAMA imekuwa ni nguzo kuu ya kimaendeleo ya kiuchumi na kuna umuhimu wa kuweka mazingira ya kisera yanayovutia wawekezaji katika miundombinu ya kiintaneti.

Alisema, serikali itasimamia kukuza ubunifu katika TEHAMA ili kufungua fursa za kiuchumi kwa vijana na itaendelea kuweka mkazo katika uchumi wa kidijitali ambao unachangiwa na biashara mtandao.

"Tutaweka mkazo mkubwa katika utafiti hatutaki kwenda kesho yake kwa kubahatisha kwa sababu TEHAMA kasi yake ni kubwa lazima tufanye utafiti wa kutosha," alisema.

Naye Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB ambayo ndiyo mdhamini mkuu wa kongamano hilo, Abdulmajid Nsekela, alipongeza tume ya TEHAMA na wizara husika kwa kazi nzuri iliyofanya katika kongamano hilo ambalo limekuwa na faida kwa Watanzania na wawekezaji.

Alisema huduma jumuishi katika fedha ni jambo muhimu na kwamba ni vyema kushirikiana kwa kutumia teknolojia itakayo wafikia wengi.

Alisema Watanzania wengi hawapati huduma za kibenki hasa wanawake ambao hawajapata huduma jumuishi ya kifedha.

Aliwahakikishia kuwa benki yake ipo mstari wa mbele kuyafikia makundi mbalimbali hasa wanawake kwa kuwaletea bidhaa bunifu ili kuwa matajiri wa baadaye.

Alisema wanawake wanahitaji uendeshaji wa mafunzo ya kifedha na biashara, hawahitaji kukopeshwa fedha pekee.

Katika kongamano hilo CRDB imetoa Sh. bilioni 50 kwa kampuni bunifu zinazochikupia katika masuala ya TEHAMA.

Kwa upande wao washiriki wa kongamano hilo walisema wamejifunza vitu vingi vizuri katika kukuza sekta ya hiyo na kuahidi kuwa watayafanyia kazi yale yote waliojifunza.



Mkamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (wa pili kulia), akiwa na watendaji wakuu wa Wizara ya Afya Zanzibar katika ofisi za wizara hiyo baada ya kumaliza ziara fupi ya kutembelea wagonjwa wa surua katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja mjini humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi kufungua mkutano wa siku 2 utafiti na sera

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, amesema mkutano wa kiutafiti wa warsha ya 26 ya utafiti na sera utafanyika Novemba 2 hadi 3 mwaka huu mjini hapa.

Alisema warsha hiyo, imeandaliwa na Taasisi ya Utafiti na Sera Tanzania (REPOA) kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar na Benki ya CRDB na itafunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema warsha hiyo itajadili masuala ya mabadiliko ya tabianchi na kaulimbiu ni uhaulishaji wa biashara na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya ukuaji, ushindani wa uchumi wa kijani.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yanaathiri kilimo na upatikanaji wa nishati mbalimbali na kwamba ni muhimu kutafakari suala hilo.

Alisema, lengo la warsha hiyo ni kubadilishana mawazo na kupata matokeo ya tafiti ili kuimarisha uwezo wa kisera hasa kukabiliana na mahitaji ya uchumi wa mseto na biashara shindani. "Wakati taasisi mbalimbali duniani zikiimarisha juhudi za kupunguza joto...na wenzetu wa Taasisi ya utafiti wa kupunguza umaskini, REPOA, wanakuja na majibu ya kiutafiti wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la joto," alisema. Alisema warsha hiyo itawakutanisha wataalamu, wenye uzoefu mkubwa, mabalozi wa nchi mbalimbali na wadau wa maendeleo.

Pia alisema kuna shughuli za kiuchumi ambazo zinaathirika na mabadiliko ya tabianchi na kuwa ni vyema kuzingatia mwenendo wa mabadiliko tabianchi na utafiti umeonesha kuwa mabadiliko ya hali ya hewa huathiri biashara na ugavi. Aidha, alisema madhara ya mabadiliko ya tabianchi hayaathiri uzalishaji pekee katika minyororo ya thamani, pia biashara katika mikondo ya awali kama zinavyodhibitiwa na shirika la biashara ulimwenguni.

Naye Mkurugenzi wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela, ambayo ni mdhamini mkuu wa warsha hiyo, alisema mkutano huo una umuhimu wake kwa Zanzibar kwa vile sera, biashara na tabianchi inaumuhimu kwa maisha ya watu.

Alisema benki hiyo imejipanga katika mipango yake endelevu kuwasaidia wananchi hasa wanaojiajiri kuwakopesha kwa riba nafuu kwa maendeleo yao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya REPOA, Donald Mmari, alisema mkutano huo unaofanywa kwa kushirikiana na CRDB na utatoa fursa kwa Wazanzibar kujadili sera, utafiti na biashara katika kukabiliana na tabianchi.

# Watoto wanane wafariki kwa ugonjwa wa surua

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO wanane wamefariki dunia kutokana na ugonjwa wa surua na wengine 1,315 wanaendelea kupatiwa matibabu.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, alisema hayo juzi akiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja baada ya kuwatembelea watoto wanaougua surua waliolazwa katika hospitali hiyo.

Othman aliutaka uongozi wa Wizara ya Afya Zanzibar kufanya jitihada ya kuelimisha na kujenga uwelewa kwa jamii kuhusu mlipuko wa ugonjwa huo.

Alisema, kufanya hivyo ni silaha muhimu inayoweza kuongeza nguvu kwa jamii na serikali kwa pamoja kukabiliana vyema na ugonjwa huo na hatimaye kuudhibiti na kumalizika katika kipindi kifupi.

Pia alisema kutaondoa mkanganyiko na upotoshaji wa taarifa unaofanywa na baadhi ya watu kulielezea suala hilo kinyume na hali na kusababisha sintofahamu kwa wananchi na wageni wanaotembelea Zanzibar.

Othman alisema tatizo la surua lililojitokeza katika kipindi cha miezi michache iliyopita Zanzibar sio la Wizara ya Afya ama serikali pekee, linawahusu Wazanzibar wote na kila mmoja anapaswa kushiriki katika mapambano hayo ili kuumaliza kabisa ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisikitishwa na na baadhi ya watu wanaopotosha kuhusu ugonjwa huo na kuwataka wataalamu wa Wizara ya Afya kuhakikisha wanawaeleza wananchi na jamii kuhusu hali halisi ya suala hilo.

Alisema suala la mlipuko wa maradhi hayo ni lazima lichukuliwe kama ni tatizo la kitaifa kwa kuwa athari inayopatikana inamgusa kila mmoja na ushiriki wa kila taasisi yakiwamo mashirika ya kimataifa.

Alisema wananchi wanapaswa kuunga mkono juhudi na mipango ya serikali katika kukabiliana na kupambana na tatizo hilo ili kuudhibiti na kuondoa kabisa usiendelee kuathiri zaidi watoto. Naye Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salimu Nassir Slimu, alisema maradhi hayo yalianzia katika wilaya za Magharibi A na B Unguja na kwamba licha ya kufanywa chanjo katika wilaya hizo, ulisambaa katika wilaya nyingine.

Alisema, wengi waowaliothirika ni watoto chini ya umri wa miaka mitano na zaidi wenye lishe duni ambao afya zao ziko dhaifu kuhimili vishindo vya maradhi mbalimbali.



# Mtoto wa miaka 3 anajasiwa na mtu asiyejulikana Shy

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MTOTO mwenye miaka mitatu (jina limehifadhiwa), Manispaa ya Shinyanga, amedaiwa kunajisiwa mtu asiyefahamika uchochoroni jirani na nyumbani kwao.

Tukio hilo limetokea Oktoba 28, 2022 majira ya saa nne asubuhi baada ya mama mzazi wa mtoto huyo (jina lake limehifadhiwa), kumuona mtoto wake akirudi nyumbani akichechemea na kushika sehemu zake za siri.

Alieleza kuwa mtoto alikuwa akilia kwa sauti kubwa akiwa ameshikilia sehemu zake za siri na alipomwangalia akagundua kuwa amenajisiwa.

Akielezea tukio hilo juzi kwa njia ya simu, Mwenyekiti mtaa anaoishi mama wa mtoto huyo, Solomoni Najulwa, alisema taarifa za kunajisiwa kwa mtoto huyo alizipata kutoka kwa mama wa mtoto kwa kupigiwa simu kwa kuwa alikuwa safarini na kuahidi kufuatilia tukio hilo. Alisema wajumbe walipofika eneo la tukio hawakumkuta mtoto kwa kuwa mama yake alishampeleka hospitali.

"Majira ya saa sita mchana nilipigiwa simu na mmoja wa wakazi katika mtaa wangu ambapo aliniambia mtoto wake amebakwa na mtu asiyefahamika, ndipo nilipowatuma wajumbe wafike eneo hilo haraka ili kutoa msaada, lakini walikuta mama huyo ameshampeleka hospitalini," alisema Najulwa. Aidha, aliahidi kushirikiana na wananchi wote kumsaka aliyehusika na tukio hilo la kikatili na kuhakikisha anakamatwa na kujibu tuhuma zote zilizowahi kutokea kipindi cha nyuma ili kukomesha tabia hiyo isijitokeze tena. Alisema mtaani kwake kumekuwapo na wimbi la vijana wengi wakizurura bila kazi maalum wakituhumiwa kuwa miongoni mwa wahusika wa matukio ya ubakaji pamoja na uhalifu mwingine huku akiahidi atakomesha vitendo hivyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Kwa upande wake Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema hajapata taarifa ya tukio hilo.



Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wakiwa kwenye kikao cha baraza la robo ya kwanza ya mwaka wa fedha (2022/2023) juzi wakijadili masuala mbalimbali kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo ya manispaa hiyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# H'shauri kudhibiti ubadhirifu miradi ya shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, imepanga kudhibiti wizi wa fedha za ujenzi wa miradi ya maendeleo Sh. milioni 800 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya vyumba 41 vya madarasa katika shule za sekondari.

Vyumba hivyo vya madarasa vinavyotarajiwa kutumiwa na wanafunzi 5,500 waliohitimu elimu ya msingi mwaka huu na kuanza kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo wa 2023.

Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Leonard Mabula, alibainisha hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema, atahakikisha vyumba hivyo vinakamilika kwa wakati ili mwakani wanafunzi hao wapate mazingira mazuri ya kujisomea.

Alisema, mkakati walionao kwa sasa ni kuziingiza pesa hizo kwenye akaunti za shule na kuunda kamati za usimamizi kwa kufanya ukaguzi kila wakati ili kujua zinatumia katika matumizi yaliyopangwa.

Katika halmashauri hiyo miradi ya ujenzi wa hospitali ya wilaya kwenye fedha zilizotolewa na serikali ulitokea wizi Sh. milioni 60 na kusababisha baadhi ya watumishi idara ya fedha akiwamo mtunza hazina kufukuzwa kazi.

"Haitaweza kujitokeza tena hali ya watumishi wasiokuwa waaminifu kuiba fedha za serikali kama ilivyokuwa kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya, tuko makini na tutakuwa tunakagua ujenzi huu mara kwa mara ili kujua mtiririko wa fedha na thamani ya mradi," alisema Mabula.

Ofisa Elimu Sekondari wa halmashauri hiyo, Seleka Ntobi alisema, hali ya ujenzi wa vyumba hivyo 41 vya madarasa unaendelea vizuri hadi kufikia mwezi Desemba yatakuwa yamekamilika.

Kadhalika, wanafanya ukaguzi wa ujenzi mara kwa mara kuhakikisha fedha hizo zinatumika ipasavyo ili kama kutatokea dalili za ubadhirifu wahusika wachukuliwe hatua za kisheria haraka kabla hazijapotea na kukwamisha ujenzi.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu alisema, fedha hizo zimetoa ahueni kwa wazazi ambao kwa sasa wana hali mbaya ya upungufu wa chakula kutokana na mwaka jana kutokuwa na mavuno ya kutosha.

Katika hatua nyingine, Manispaa ya Kahama imepokea Sh. bilioni 1.2 kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 60 vya madarasa katika shule za sekondari 14 zenye upungufu mkubwa wa madarasa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani.

Shule hizo ni pamoja na sekondari ya Abdulrahim Busoka, Anderson Msumba, Bugisha, Isunuka, Kabela Gold, Malunga, Mpera, Ngogwa, Nyashimbi, Nyasubi, Nyihogo, Seeke pamoja na Sekondari ya Mama Samia.

# Maofisa polisi watakiwa kuchangamkia mikopo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, amewataka maofisa polisi nchini kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa katika Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Jeshi la Polisi nchini, Usalama wa Raia (URA-SACCOS) ili kupiga vita tamaa na vitendo vya rushwa.

Sajini alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mwanza, akifungua mkutano wa 14 wa chama hicho huku akiwataka maofisa polisi kuweka akiba na kukopa kutokana na chama hicho kuwa na mikopo yenye masharti nafuu kulinganisha na taasisi nyingine za kifedha.

"Kwanza nitoe pongezi kwa kuanzishwa kwa chama hichi ambacho kwa kiasi kikubwa kitasaidia katika kuinua, kuboresha ustawi wa askari polisi kiuchumi, kurahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika kazi ikiwa ni pamoja na kujilinda dhidi ya vitendo vya rushwa," alisema.

Aidha, alionyesha kufurahishwa na chama hicho kinavyoendelea kukua na kuongeza idadi ya wanachama kutoka 4,300 hadi 46,024.

Alisema miaka 16 tangu kuanzishwa kwa chama hicho kimefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 394, huku zaidi ya asilimia 75 ya mikopo hiyo ikitumika katika ujenzi wa makazi binafsi ya wanachama wake.

Alisema ni dhahiri kuwa kiasi hicho cha fedha kimeingia kwenye mzunguko wa fedha na kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa na uchumi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya chama hicho, Kamishna wa Polisi (CP) Benedict Wakulyamba, alisema kupitia ushirika wa chama hicho umewawezesha askari Polisi na watumishi raia wa wizara hiyo kuwa watulivu nchini na kutekeleza majukumu yao vizuri.

Naye Mrajisi Msaidizi kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Josephat Kisamalaa, alisema chama hicho ni miongoni mwa SACCOS kubwa nchini inayowafikia watu wengi.

"Tunaipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kuisaidia taasisi hii ambayo inaendelea kuwahudumia Watanzania wengi wanaohitaji huduma za kifedha," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Moto ulivyoua watoto kwenye banda la kuku

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO wawili; Meshack Ndimbwa (6) na Agrey Mgimba (2) wa Kijiji cha Lugarawa wilayani Ludewa mkoani Njombe wamefariki dunia kwa kuungua na moto wakati wakicheza ndani ya banda la kuku nyumbani kwao.

Katika tukio hilo, Anold Mgimba (4) pia alijeruhiwa kwa kuungua na moto akiwa ndani ya banda hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo alipotafutwa na Nipashe jana.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya St. John Lugarawa, Dk. Camilo Msigwa, alisema alipokea miili ya watoto wawili waliofariki na mmoja akiwa na majeraha.

"Huyu mtoto mmoja ambaye ni majeruhi, anaendelea na matibabu na hali yake sio mbaya sana. Ameungua sehemu ya kichwani, kifuani na mikononi.

"Kwa sasa yupo kwenye matibabu na madaktari wanaendelea kumpatia huduma, lakini watoto wawili walioletwa hapa hospitalini walikuwa wameshafariki dunia kwenye eneo la tukio," alisema Dk. Msigwa.

Tabibu huyo alifafanua: "Watoto hao waliungua kwa asilimia kubwa kiasi kwamba yule mdogo aliungua hadi fuvu la kichwa lilikuwa likikaribia kuteketea, baadhi ya vitu vya ndani kuonekana, utumbo ulikuwa umetoka, hivyo ilikuwa vigumu kusema tuweze kuwahifadhi hapa hospitalini, hivyo walizikwa jana jioni, wote wawili."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lugarawa, Thomas Kayombo, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 29, mwaka huu majira ya saa tano asubuhi.

"Ilikuwa ni Magufuli Day (Siku ya Magufuli) kuna kijana anaitwa George alikuwa amechoma mabua nyumbani kwake, sasa ile nyumba inapakana na nyumba ya pili ambayo kulikuwa na vibanda vya kuku na nguruwe, sasa alivyochoma ule moto palivyokuwa pametulia akaondoka, kuna watoto watatu waliingia kucheza kwenye vile vibanda.

"Sasa ulipopuliza upepo ule moto ukashika vile vibanda watoto wale wote watatu wakawa ndani kwenye vibanda vya nyasi na walipokuwa mule ndani walipoona moto unakuja, mtoto mmoja alitoka na kuanza kukimbia, wawili walishindwa kutoka, yule aliyekimbia alipofika mbele akaamua kurudi ili awaokoe wenzake wakati moto ulishakolea.

"Sasa kwa bahati nzuri pale jirani kulikuwa na fundi anapaua nyumba alipoona mtoto anarudi anakimbia, ikabidi aruke kutoka kule juu akaenda kumkamata huyo mtoto lakini alikuwa ameshaungua," alisimulia.

Diwani wa Lugarawa, Erasto Mhagama alisema tukio hilo lilisababishwa na moto ambao ulikuwa umechochewa na upepo mkali.

## Wanakijiji washuhudia magari yakipita kwa mara ya kwanza

**Na Gideon Mwakanosya,** NYASA

WANANCHI wa Kijiji cha Ndonga, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma wameshuhudia kwa mara ya kwanza magari yakipita kijijini kwao baada ya serikali kutoa fedha za kuitengeneza barabara.

Wakizungumza kwa furaha kijijini hapo na waandishi wa habari, wameupongeza Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA), kwa kuimarisha miundombinu na kuanzisha barabara mpya mkoani Ruvuma inayounganisha vijiji vya Njambe na Ndonga.

Akitoa taarifa mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, wakati wa ufunguzi wa barabara hiyo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ndonga, Edward Ndunguru, alisema kwa muda mrefu wananchi wa kijiji hicho walikuwa wanapata adha ya usafiri kwa kukosa barabara.

Ndunguru alisema Kijiji cha Ndonga kina kaya 311 na wakazi wapatao 1,080 na kwamba kufunguliwa kwa barabara hiyo kutaleta ukombozi mkubwa kwa wakazi wa kijiji hicho na kuwaunganisha kiuchumi na vijiji jirani.

Kwa upande wake, Mhandisi wa TARURA, Wilaya ya Nyasa, Thomas Kitusi, alisema kuwa serikali imetoa fedha kupitia mfuko wa barabara (Road fund) na zaidi ya Sh. milioni 220 zimetumika kutengeneza barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 6.9 ambayo itaondoa shida ya usafiri.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, alisema kwa kipindi chote walipoteza maisha kutokana na ukosefu wa miundombinu ya barabara na mwananchi anapougua na kutaka kuwahishwa hospitali walikuwa wanashindwa kutokana na kutokuwapo kwa barabara.

Kanali Thomas alisema Kijiji cha Ndonga kilikuwa kama kisiwa, kwenda makao makuu ya kata walikuwa wanatumia mtumbwi au waende kijiji cha Njambe watafute usafiri wa gari.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya NBC wilayani Kigamboni katika hafla iliyofanyika wilayani humo jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi na Mkuu wa Wilaya, Fatma Nyangasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadai kugombea maji na mifugo

**Na Beatrice Shayo,** MPWAPWA

BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Sazima, Kata ya Mima Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma wameiomba serikali kuwapatia majisafi na salama ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Nipashe ilizungumza na wananchi hao kwa nyakati tofauti Kitongoji cha Mgogo, wanaotegemea maji katika visima vya asili.

Walisema maji wanayotumia sio safi na salama, lakini inabidi wayatumie kutokana na mazingira magumu ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Mika Malonga, alisema pia upatikanaji wa maji hayo ni shida.

Alisema inawalazimu kugombea na wanyama katika visima kutokana na umbali wa kuyafuata majisafi na salama yalipo.

"Serikali imetengeneza kisima kutoka huko kuyafuata ni zaidi ya kilomita saba hatuwezi kufika huko tunajikuta tunaamua kuyatumia haya ya visimani hapa yenyewe kuyafuata haya ya visimani tunatembea zaidi saa mbili," alisema.

Malonga alisema wanapoamka alfajiri kuyafuata maji kuna wakati usalama wao unakuwa mdogo kwa kuwa hukutana na wanyama wakali ikiwamo chui.

Mwananchi mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Alice alisema kufuata maji umbali mrefu wanakutana na kipigo cha kuchelewa kufika nyumbani kwa wakati.

"Huwezi kufika na kuchota maji unakutana na foleni wenye mifugo mpaka wawape maji mifugo yao ndipo na mimi nichote na kama yameisha katika kisima nikae pembeni kusubiri yaongezeke," alisema.

Alisema mtu anaweza kupoteza saa tatu hadi tano kusubiri maji na bado muda anapoteza muda njiani kwa kutembea umbali wa saa mbili kufika nyumbani, anamweleza mwenzake haamini kama muda wote huo ametumia kutafuta maji.

"Nikifika naulizwa ulikuwa wapi muda wote namweleza maji hayakuwapo anahisi nilikuwa na wanaume wamenichelewesha na kuanza kunipiga bila kujali matatizo niliyokutana nayo," alisema.

Diwani wa Kata ya Mima, Bezarery Mnyambwa, aliomba serikali iangalie uwezekano wa kuongeza kisima kwa wakazi hao ili waweze kupata majisafi na salama badala ya kuendelea kugombea na mifugo.

Alisema mazingira ya visima hivyo usalama wa afya zao upo hatarini kwa kuwa kuna wakati mifugo huanguka na kwa sababu havijatengenezwa katika ubora.

Naye Mkurugenzi wa Wilaya ya Mpwapwa, Mwanahamisi Ally, alisema wanakabiliwa na hali ya ukame kutokana na mabadiliko ya tabianchi ya kukosekana kwa mvua za kutosha na kusababisha uhaba wa maji katika baadhi ya maeneo.

"Tatizo la maji ni kubwa kutokana na eneo hili kuwa la ukame sio tu huko vijijini hata hapa mjini tuna tatizo la maji," alisema.

Alisema Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) inatakiwa kuwajengea wananchi miundombinu mikubwa ya maji ili wananchi waweze kupata majisafi yenye kuwatosheleza binadamu na mifugo.

# Wafugaji waomba muda zaidi kusajili mifugo yao

**Na Elizabeth Zaya,** LONGIDO

WAFUGAJI katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha wameiomba serikali kuwaongeza muda wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo unaofanywa kwa sasa, wakiwa na hoja kwamba wameyumba kiuchumi na kushindwa kumudu kulipia gharama za utambuzi huo.

Kwa mujibu wa mwongozo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ulioanza kutumika mwaka jana, mifugo yote nchini inapaswa kutambuliwa ili kuweka utaratibu mzuri wa kuwezesha utambuzi, usaili na ufuatiliaji wa mifugo kwa kuonyesha mahitaji, majukumu na wajibu wa kila mdau ili kufikia lengo la jumla la mifugo yote ya Tanzania kutambuliwa na kusajiliwa.

Mwongozo huo unaeleza kuwa mifugo inayotakiwa kutambuliwa ni ng`ombe, punda, kondoo na mbuzi wenye umri wa miezi zaidi ya mitatu huku bei elekezi za usajili wa mifugo ni Sh. 1,750 kwa ng`ombe na punda, wakati mbuzi na kondoo ni Sh. 1,000.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wilayani hapo, wafugaji hao walisema wanashindwa kumudu kulipia usajili wa mifugo yao kwa sababu inaendelea kufa kutokana na kukosa malisho na maji na haiuziki sokoni kutokana na kukonda.

Kingozi wa Mila katika Wilaya hiyo, Mutel Laizer alisema katika kipindi hiki wafugaji wengi wana hali ngumu kiuchumi kutokana na mifugo yao kufa baada ya kukosa malisho na hata iliyobakia hawama uhakika kama itapona endapo hali ya ukame itaendelea, hivyo hawana kipato cha kuwawezesha kulipia gharama za usajili.

"Wafugaji wengi kwa sasa wameshindwa washike lipi na waache lipi, wamechanganyikiwa kwa sababu wakiangalia mifugo yao inaendelea kufa, na hata wakitaka kuuza hiyo iliyobaki ili iwasaidie kulipia kazi hiyo ya utambuzi wa mifugo yao, haiuziki.

"Kwa hiyo, ni ombi letu kwa serikali angalau iahirishe kazi hiyo kwa sasa. Kwa sababu hata hicho kiasi kilichowekwa kwa ajili ya kulipia ni kazi kubwa kwa sasa wafugaji kukipata kwa sababu nguvu kubwa wanayoiweka katika kipindi hiki ni kupata chakula kwanza," alisema.

Seembo Dirai, mkazi wa Kijiji cha Dirai wilayani hapa, alisema ng`ombe wake 170 wamekufa tangu kutokana na kukosa malisho katika kipindi cha kuanzia Januari mwaka huu hadi sasa.

Ni athari zilizomkumba Marya Oreteiti, mjane na mkazi wa Kijiji cha Longaiki, akiwa amebakiwa na ng'ombe 20 na mbuzi 18 baada ya wengine kufa (ng'ombe wanne na sita wamekufa) kutokana na ukame.

Ofisa Mifugo, Wilaya ya Longido, Nestory Dakaro alisema mifuko ambayo imekufa tangu Januari mpaka sasa ni zaidi ya 58,000, akisisitiza wanaendelea na tathmini kufahamu athari zaidi katika eneo hilo.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema mwisho utambuzi, usajili ya ufuatiliaji wa mifugo ni mwezi huu.

"Huu utambuzi tangu uanze tuna mwaka mmoja na tumehamasisha, tumepiga ngoma sana na tuliimba nyimbo zote za utambuzi, sasa baada ya tarehe ya kusweka hereni kwa hiari itakuwa ni mwisho wa mwezi huu, na baada ya hapo sheria ya utambuzi na ufuatiliji itaanza kutumika.

"Sheria hiyo inasema adhabu ya kwanza kwa atakayeshindwa kutekeleza atatozwa faini ya fedha zisizopungua Sh. milioni mbili au asipolipa hiyo faini anaweza kuhukumiwa kwenda jela miezi sita au vyote kwa pamoja," alisema Prof. Nonga.

## Mabadiliko tabianchi yawapa somo wakazi

**Na Rahma Suleiman,** Zanzibar

KATIBU wa Jumuiya ya upandaji na uhifadhi mikoko (JUMUKISI) katika kijiji cha Kisakasaka Zanzibar, Khatib Ali Vuai, amesema baada ya kijiji hicho kuathirika na mabadiliko ya tabianchi, wameamua kupanda na kuhifadhi mikoko ambayo imesaidia kuzuia mmong'onyoko wa ardhi kijijini huko.

Akizungumza na Nipashe kijiji huko mwishoni mwa wiki, Vuai alisema miongoni mwa athari zilizojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni maji ya bahari kuvamia visima vya maji safi.

Alisema pia kulikuwa na upungufu wa samaki kijijini huko na kipindi cha upepo nyumba nyingi zikiezuliwa.

Vuai alisema baada ya athari hizo kutokea, walijikusanya na kuazisha jumuiya hiyo ambayo wanachama wake ni vijana kwa mchanganuo wa wanaume 10 na wanawake wanane.

Alisema eneo walililopanda mikoko lina ukubwa wa hekta 70 ambapo kwa sasa mafanikio yameanza kupatikana ikiwamo kuzuia maji ya bahari kupanda katika makazi ya watu na athari zilizosababishwa na upepo zimepungua.

Alisema kuwa awali wakazi wa kijiji hicho walikuwa wakikata mikoko kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwamo kuni, mkaa na shughuli za ujenzi.

"Katika miaka ya 1990, hali ya kimazingira ilikuwa mbaya kwa sababu maji yetu hapa tunayotumia ni ya kisima, hivyo yalibadilika ladha na kuwa ya chumvi kutokana na maji ya bahari kuvamia maeneo ya wakazi, lakini kwa sasa maji yamerejea katika hali yake ya kawaida," alisema.

Alikumbusha kuwa miaka 1980, kijiji hicho kilikuwa na mikoko mikubwa lakini hali ilibadilika katika miaka ya 2000 baada ya miti mingi kukatwa.

Hata hivyo, Vuai alisema licha ya mafanikio hayo, bado kuna uharibifu wa mikoko ingawa kiwango sio kwa kiwango cha kutisha kulinganishwa na awali.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James (kulia), akijadiliana na Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Bia ya Serengeti Breweries (SBL), Rispa Hatibu, katika uzinduzi wa kampeni ya SBL kupinga ulevi katika umri mdogo kwa wanafunzi iitwayo 'SMASHED', iliyofanyika Shule ya Sekondari Urafiki, jijini Dar es Salaam mwishoni wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni kuzuia wanafunzi kunywa pombe yazinduliwa

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imezindua programu ya kupambana na unywaji wa pombe kwa watu wenye umri chini ya miaka 18 inayolenga kudhibiti tabia ya unywaji pombe miongoni mwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyopewa jina la SMASHED mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, aliipongeza SBL kwa kuja na mpango huo wa kukabiliana na tatizo la unywaji wa pombe miongoni mwa vijana wenye umri mdogo hasa wanafunzi.

"Niwaombe wazazi, walimu, wanajamii, tuna jukumu la kuilinda na kujenga jamii yetu. Kwa pamoja tuunganishe nguvu na Serengeti Breweries Limited ili tufanikiwe katika kupunguza utumiaji wa pombe na maeneo mengine kwa wanafunzi.

"Moja ya maeneo ambayo tunayaona yanaanza kuwa na shida ni pamoja na hilo ambalo watoto wadogo sasa wanatumia mihadarati, watoto wadogo sasa wanatumia vinywaji na vileo.

"Sasa kwa pamoja tukiweka nguvu tunaweza kufanikiwa kwenye eneo la pombe na maeneo mengine, maana wengine wanatumia sigara, wengine bangi, tusipoilinda jamii ya watoto wa sasa, maana yake tumechagua jamii ya ovyo ya baadaye," alisema James.

Kwa mujibu wa Meneja Mawasiliano wa SBL, Rispa Hatibu, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zenye kundi la watu wenye umri mdogo wanaotumia pombe. Alisema utafiti uliofanywa mwaka 2019 katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro ulibaini kuwapo mwenendo wa matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15 na zaidi kutoka asilimia 12.9 miongoni mwa wasichana mkoani Mwanza hadi asilimia 63.9 miongoni mwa wavulana mkoani Kilimanjaro.

Aliongeza kuwa mwenendo wa matumizi ya pombe miongoni mwa wanafunzi wenye umri wa miaka 13-15 jijini Dar es Salaam ulikuwa wa asilimia 5.6.

"Kampeni hii imepewa jina la SMASHED, ni kampeni ya kupambana na unywaji wa pombe ya SBL, inayotumia michezo ya kuigiza ya jukwaani kwa wanafunzi inayowapa uzoefu wa kipekee na kusisimua. "SMASHED hufanyika shuleni na huelimisha wanafunzi wa sekondari kuhusu madhara ya matumizi ya pombe katika umri mdogo, kwa kuwashauri kujiepusha na matumizi ya pombe kabla ya kukomaa.

"Mpango huu unahusisha utoaji wa mafunzo muhimu juu ya athari mbaya za unywaji pombe katika umri mdogo kwa vijana na jamii.

"Programu inachanganya matumizi ya maonyesho ya maigizo na ushiriki wa wanafunzi katika mazingira ya motisha ya kujifunza ili kuwapa ukweli, ujuzi na ujasiri wa kufanya uchaguzi wa kuwajibika na kuendeleza mitazamo ya uwajibikaji katika masuala yanayohusiana na afya," alisema.

# Killy, Cheed washauriwa kurudi kwa Ali Kiba

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva na 'chawa' wa Diamond Platnumz, 'Baba Levo', aliwashauri wanamuziki Killy na Cheed kumwomba radhi Ali Kiba ili warudi kwenye lebo yake ya Kings Music.

Levo amesema kuwa anawaamini wasanii hao wawili kuwa na kipaji kikubwa na wana uwezo mkubwa kwenye sanaa yao.

Alisema kwamba aliamini kuwa Ali Kiba ana uwezo wa kuwasaidia Killy na Cheed katika muziki wao na kuwa ana fedha za kutosha kuwasimamia wawili hao bila utatanishi wowote wala kuwa na majuto baadaye.

"Warudi kule walikotokea, King Kiba tayari ni mtu mkubwa kwa hiyo naamini kuwa watafanya vizuri kwani walikuwa washaanza kufanya vizuri ila labda walishikwa na tamaa ya kwenda kwa Harmonize," alisema.

"Nimeona Diamond alivyotumia hela kwa Zuchu, zaidi ya milioni tatu au nne, ukilipa milioni tano kisha uje ulie baadaye ina maana kuwa huna, nilijua kuwa atashindwa," alisema.

Aliwashauri wasanii kujipanga na kuwa sawa kifedha kabla ya kuwa na lebo kwani kusimamia wasanii wengine kunahitaji hela.





# GIGY MONEY HATATOA ALBAMU

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kike wa muziki wa Bongo Fleva, Gift Stanford 'Gigy Money', amesema anashindwa kufikiria suala la kuandaa albamu kwani mashabiki wana mtindo wa kusikiliza wimbo mmoja au mbili tu.

Gigy amesema hayo alipokuwa kwenye uzinduzi wa albamu fupi ya Mbosso Khan ambapo alipoulizwa na waandishi wa habari kwamba ni lini naye atatoa albamu, ndipo alipotoa mtazamo wake huo na kuwachana mashabiki.

"Mashabiki si poa, unatoa albamu yeye anasikiliza wimbo mmoja tu hizo nyingine anakuachia wewe," alisema Gigy.

Gigy alisema, yeye hana kipato kikubwa cha kuweza kuandaa nyimbo nyingi hivyo ataendelea kuwa anatoa wimbo mmoja mmoja maana hela zake ni za kuungaunga.

# *AT abadili jina lake*

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva kutoka Zanzibar, Ally Tolu maarufu AT, ametoa taarifa rasmi ya kutokutumia tena jina la AT na sasa atatambulika kwa jina la Bey.

AT kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameeleza kwamba moja ya sababu iliyomfanya akaachana na jina lake hilo la zamani ni kutokana na msanii mwingine nje ya Tanzania kutumia jina hilo.

"Hellow, leo ni siku maalumu kwangu sababu najiona kama nimezaliwa upya kwenye game ya muziki.

"Nilitangaza kuacha muziki wa mduara na leo rasmi natangaza kuachana na kutumia jina la AT kwa sababu nyingi, moja wapo ikiwa mwingiliano wa jina langu na msanii mwingine ambaye yupo nje ya mipaka ya Tanzania, ikiwa mipango yangu mikubwa ni kufika kimataifa nimeona nitumie fursa hii kujiandaa mapema.

"Kwa sasa nitatambulika kama Bey na si AT, na nitakuwa kwenye muziki wa kisasa wa kibiashara zaidi na Yaya ndio wimbo wangu wa kwanza kama Bey, ahsanteni."



# PHIRI SASA AZIWEKA KIPORO YANGA, AZAM FC LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema straika wao, Moses Phiri ameonekana kusikitika baada ya kushindwa kufunga mabao kwenye mechi kati timu hizo dhidi ya Yanga na Azam FC.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema ameongea na straika huyo raia wa Zambia na kumweleza kwamba hakujisikia vizuri kutokana na kutopata bao kwenye mechi hizo, lakini hajakata tamaa kwani kuna mechi za marudiano.**

"Phiri ni mchezaji anayependa kufunga mabao muda wote, kwa hiki kilichotokea kutofunga kwenye mechi dhidi ya Yanga na Azam, kimemfanya asijisikie vizuri kwa sababu yeye anapenda kufunga mabao na kinachomuuma zaidi ni kutofunga kwenye mechi kubwa.

"Mchezaji mkubwa mwenye kariba yake anapenda kufunga na kung'ara kwenye mechi kubwa, kwa hivyo amesema amesikitika sana, lakini hajakata tamaa kwa sababu kuna mechi za mzunguko wa pili," alisema Ahmed.

Alisema pamoja na kwamba yote haya yametokea, lakini lengo lake lipo pale pale ambalo ni kuisaidia Simba kwenye Ligi Kuu na mechi za kimataifa kuona inaweka rekodi nzuri, lakini kuwa mfungaji bora msimu huu.

"Anakitaka Kiatu cha Dhahabu msimu huu, unajua moja kati ya usajili mkubwa ambao tumeufanya msimu huu ni Phiri na alikuwa anasubiriwa na mashabiki wa Simba kwa muda mrefu, na mpaka sasa hajawaangusha," alisema.

Kwa sasa mchezaji huyo ana mabao manne kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu katika mechi saba alizocheza, akiwa amefunga mabao kwenye mechi nne, akikosa kufanya hivyo mechi tatu.

Mechi alizofunga mabao ni dhidi ya Geita Gold, Kagera Sugar, KMC na Dodoma Jiji, na hakufanikiwa kufunga kwenye mechi dhidi ya Yanga, Azam na Tanzania Prisons.

Kwenye mechi za kimataifa, amepachika mabao matano, akifunga kwenye michezo yote minne ambayo alicheza mbili dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi, na mbili dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola.

HUPITI HAPA...




Beki wa kulia wa Geita Gold FC, George Wawa, akimkabili winga wa Yanga, Bernard Morrison, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba na Yanga kushinda bao 1-0 kwa penalti. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vijana Tanzania hoi kufuzu Afcon

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Taifa za Tanzania za Vijana chini ya miaka 20 na 23, juzi zilikumbana na vipigo kwa kuchapwa mabao 2-0 kila moja kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika chini ya umri huo.

Timu ya vijana chini ya miaka 23, ikiwa kwenye Uwanja wa Lekan Salami, Adamasingba jijini Ibadan, Nigeria ilijikuta ikifungwa 2-0 na kuondoshwa nje ya michuano hiyo kwa jumla ya mabao 3-1.

Oktoba 22, mwaka huu timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, yote yakipatikana kwa mikwaju wa penalti, Success Makanjuola akiifungia Nigeria na Ally Msengi akifunga kwa upande wa Tanzania.

Kwenye mechi ya juzi, Makanjuola aliifungia tena Nigeria bao kwa mkwaju wa penalti dakika ya 68. Lilikuwa ni bao la pili kwenye mchezo huo lililozima kabisa ndoto za timu hiyo kukata tiketi ya kufuzu fainali ya AFCON chini miaka 23 inayotarajiwa kufanyika mwakani nchini Morocco. Dakika saba nyuma, Tanzania ilikuwa imekubali bao la kwanza kupitia kwa Timileyin Ogunniyi.

Nchini Sudan ambako michuano ya kusaka tiketi ya kucheza AFCON kwa vijana chini ya miaka 20, Kanda ya CECAFA, Tanzania ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Uganda chini ya umri huo.

Mechi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa Al Hilal, Khartoum, nchini humo.

Tanzania ipo Kundi B, ikiwa na timu za Uganda na Ethiopia, huku Kundi A likiwa na wenyeji, Sudan, Burundi, Sudan Kusini na Djibouti.

Bingwa wa michuano hiyo Ukanda wa CECAFA, ndiye atakayeiwakilisha kanda hii kwenye fainali za AFCON akiungana na mabingwa wa kanda zingine.

# Idd Cheche aanza kwa cheche Championship

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache tu baada ya kujiunga na Pan African, Kocha wa zamani wa Azam FC, Idd Cheche, ameiongoza timu hiyo kupata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi ya Championship kwa kuichapa Gwambina mabao 3-1, mechi ikichezwa juzi Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo, Dar es Salaam.

Cheche ambaye alipewa jukumu la kuinoa timu hiyo baada ya klabu hiyo kumtimua kocha Twaha Beimbaya kutokana na matokeo yasiyoridisha, amekiongoza kikosi hicho kwenye mechi yake ya kwanza kupata ushindi huo, ambapo wafungaji walikuwa ni Alex Peter, Abdallah Rashid na Khalifa Nolo.

Pan African, Mabingwa wa Ligi ya Muungano Tanzania mwaka 1982, walikuwa wamecheza mechi sita kwenye Ligi ya Championship bila kupata ushindi wowote.

Matokeo hayo yanaifanya kuwa kwenye nafasi ya 12, ikicheza mechi saba, ikishinda moja, sare tatu, ikiwa imeshapoteza mechi tatu pia, ikivuna pointi sita.

Kwenye mechi zingine za ligi hiyo ambapo timu zinasaka nafasi za kucheza Ligi Kuu msimu ujao, African Sports imepata ushindi wa bao 1-0 ikiwa nyumbani, Mkwakwani Tanga dhidi ya Copco, Mbuni FC ikiendeleza ushindi, safari hii ikiitandika Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Mashujaa, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, ikiichakaza KenGold mabao 2-1, Kitayosce ikashindilia Mbeya Kwanza mabao 2-0 mechi ikipigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi na Fountain Gate ikipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ndanda kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI KUREJESHWA BARCA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, anataka kumrejesha mshambuliaji wa Paris St-Germain, Lionel Messi, 35, katika klabu hiyo ya Hispania Januari, lakini uhamisho wowote wa mchezaji huyo wa Argentina utakabiliwa na vikwazo kadhaa mbeleni. ***(Sport)***

### LIONEL KUAMUA PSG

LIONEL Messi ataamua kuhusu mustakabali wake baada ya Kombe la Dunia na hataondoka PSG Januari hata kama ataamua kutosaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ligue 1. ***(Ben Jacobs)***

### KANTE NA MKATABA

MKATABA wa kiungo wa kati wa Chelsea, N'Golo Kante, 31, katika klabu ya Chelsea unakamilika msimu ujao wa majira ya joto na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa analengwa na Barcelona wakati huu klabu hiyo ya Nou Camp ikitafuta atakayejaza pengo lililoachwa na Sergio Busquets, 34. ***(Relevo)***

### RONALDO ATAKIWA URENO

KLABU ya Sporting Lisbon ya Ureno iko tayari kuwasilisha ombi kwa Manchester United ili kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, kwa mara ya pili. ***(Sunday Mirror)***

### ALVAREZ AIOTA CHELSEA

KIUNGO wa Ajax na Mexico, Edson Alvarez, 25, amesema "alisikitishwa" na kutokamilika kwa uhamisho wa kwenda Chelsea msimu wa majira ya joto. ***(ESPN, via 90 Min)***

### DEPAY KUUZWA JANUARI

BARCELONA wanatarajia kumuuza mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay, 28, Januari huku Klabu ya Juventus ya Italia ikionyesha nia ya kutaka kumnunua mchezaji huyo. ***(Sport)***

### KESSIE KURUDI SERIE A

KIUNGO wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, 25, hajafurahishwa kutoshirikishwa katika kikosi cha kwanza akiwa Barcelona na anataka kurejea Serie A nchini Italia, ambako aliichezea AC Milan. ***(Fichajes)***

### SILVA KUPEWA MKATABA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kumpa kiungo wa Ureno, Bernardo Silva, 28, mkataba mpya wa miaka mitano kwa masharti yaliyoboreshwa. ***(Football Insider)***

### CAICEDO GHALI SOKONI

KLABU ya Brighton iko tayari kumuuza kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, 20, lakini wanataka pauni milioni 85 kwa mchezaji huyo ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea na Newcastle United. ***(Sunday Morror)***

### HENRIQUE AWINDWA EVERTON

KLABU za Everton na Brighton zinavutiwa na beki wa kushoto wa Monaco, Caio Henrique, 25. ***(IG Esporte)***

### DAWSON KUONDOKA JANUARI

MLINZI wa West Ham, Craig Dawson, ambaye nusura ajiunge na Wolverhampton Wanderers msimu huu wa majira ya joto, anataka kuondoka kwa 'Wagonga Nyundo' hao wa London Januari. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: LIVER SASA IKO KATIKA WAKATI MGUMU

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amewataka wachezaji wake kushikamana na kupambana na matatizo yao msimu huu.

**'Wekundu' hao walikutana na kichapo chao cha kwanza cha Ligi Kuu kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Anfield ndani ya takriban miaka mitano, juzi Jumamosi walipolazwa mabao 2-1 na Leeds United.**

Kipigo hicho kinaifanya Liverpool kuwa nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, baada ya mechi 12, na Klopp alikiri kwamba timu yake iko mbali na ubora wao kwa sasa.

"Ilikuwa kikwazo, kabisa," aliiambia Sky Sports. "Nilidhani tulikuwa na mwanzo mzuri kisha tukakubali bao la kushangaza.

"Tulifunga bao la kusawazisha, lakini kwa sababu fulani halikuturudishia usalama. Tulijitahidi kudhibiti mchezo na kutoa mipira mingi sana.

"Vijana walijaribu, tulikuwa na mpira mzuri na tulipata nafasi kubwa, lakini mwisho, ikiwa ni 1-1 na unalinda hali ya bao la pili kama hii, unaacha kila kitu wazi.

"Mwishowe, walikuwa wawili dhidi ya mmoja kwenye boksi na wanaweza kumaliza hali hiyo. Tatizo ni kwamba hatuwezi kudhibiti aina hii ya mchezo kwa sasa."

Alipoulizwa jinsi ya kurekebisha masuala ya sasa ya timu yake, Klopp alielekeza umakini kwenye mapambano ya majeraha ya timu yake, akisisitiza wachezaji wake wengi hawakuwa na wakati wa kurejea kwenye hali yao bora kwa sababu ya ratiba ngumu na kikosi chembamba.

"Labda baadhi ya wachezaji wamechezeshwa kupita kiasi, Harvey (Elliott), amekuwa wa kipekee kwetu msimu huu," alisema Klopp.

> ●●● Labda baadhi ya wachezaji wamechezeshwa kupita kiasi, uchezaji wa timu siku zote...

"Alikuwa na mwanzo mzuri, lakini hakuweza kuendelea. Thiago amekuwa mgonjwa, mbele wachezaji ni wale wale wanacheza kila wakati - ni washambuliaji watatu ambao tumewaacha. Ni lazima tupambane na hilo ndilo tunalopaswa kufanya.

"Uchezaji wa timu siku zote unatokana na uchezaji wa mtu binafsi, mmoja anaongoza kwa mwingine, unaweza kuutazama mchezo huu kabisa, huwezi kujilinda kama tulivyofunga bao la pili, lakini tukafanya hivyo ndiyo maana tumepoteza, vinginevyo ingekuwa hivyo.

"Lazima tulete ubora wetu uwanjani na kupambana nao, tulikuwa na matatizo tangu siku ya kwanza, kutokana na majeraha. Wachezaji walilazimika kucheza tangu siku ya kwanza, ni hali yetu na ina maana kwamba ni lazima tujisaidie."

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 389

MECHI KALI

AZAM
VERSUS
IHEFU FC

1 | 1.52
X | 3.90
2 | 6.40

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KOCHA AONYA KUWATEGEMEA MESSI, NEYMAR NA MBAPPE

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Christophe Galtier amekiri kuwa Paris Saint-Germain hawana uwiano na hawawezi kutegemea nyota wao wa mbele kuwaokoa baada ya ushindi wa 4-3 dhidi ya Troyes, juzi.

Mabingwa hao watetezi wa Ligue 1 mara mbili, walikuwa nyuma kwa mabao ya Mama Balde, kabla ya Carlos Soler kupunguza pale kwenye dimba la Parc des Princes.

Lionel Messi alifunga bao zuri la kusawazisha kisha akamtengenezea pande zuri Neymar na kuiweka PSG mbele kwa mara ya kwanza, kabla ya Kylian Mbappe kufunga kwa mkwaju wa penalti.

Badala ya kuonyesha kujivunia uwezo wa PSG wa kupambana na kusonga mbele kwa pointi tano kileleni, Galtier alikosoa uchezaji wa safu yake ya ulinzi.

"Timu haikuwa na usawa tangu mwanzo," alisema Galtier akiiambia Amazon Prime. "Wachezaji wengine walipata shida kupata viwango vyao.

"Tulishinda mipira michache sana juu ya uwanja na kupoteza upambanaji sana. Katika kiwango cha ulinzi, tulifanya makosa mengi sana.

"Hili ni jambo ambalo tunatakiwa kutumia muda kulirekebisha, jambo ambalo ni lazima tulifanyie kazi, ikibidi tufunge mabao manne ili kushinda kila mara, itakuwa ngumu.



# Simeone sasa amsifu Felix

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amimsifu Joao Felix kwa mchango wake wakati wakipoteza kwa mabao 3-2 Jumamosi dhidi ya Cadiz huku kukiwa na ripoti kuhusu kutaka kuondoka kwa fowadi huyo wa Ureno.

Atletico, ambao waliondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya sare ya 2-2 na Bayer Leverkusen Jumatano, walikuwa nyuma kwa mabao 2-0 dakika za lala salama kabla ya Joao Felix aliyetokea benchi dakika ya 60 kupunguza idadi.

Alianza kwa kufungwa kwa kichwa dakika ya 85, kabla ya Mreno huyo kusawazisha kwa shuti kali dakika ya 89. Mabao hayo yalikuwa ya kwanza kwake tangu Aprili mwaka huu.

Hata hivyo, juhudi za Felix hazikusaidia, baada ya Ruben Sobrino kufunga bao la ushindi kwa Cadiz dakika ya 98.

Licha ya kushindw[...] Simeone alimsifu Joao Fel[...] kwa mchango wake, huk[...] kukiwa na ripoti kwamb[...] Mreno huyo anawaniwa n[...] Bayern Munich.

"Joao aliingia kufanya ki[...] anachojua kufanya, alifany[...] vizuri sana," alisema Sim[...]one akiiambia DAZN.

"Alifunga bao la baha[...] lakini kwa mpango wa k[...]zalisha hatari, alikuwa h[...]tari zaidi ya washambulia[...] waliokuwa ndani ya muc[...] mfupi alioingia.

## HABARI MICHEZO

,471,330

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/11/22 | 20:30 | Racing Santander vs Alaves | 2.90 | 2.85 | 2.65 |
| 02. 01/11/22 | 20:45 | Porto vs Atletico Madrid | 2.38 | 3.27 | 2.83 |
| 03. 01/11/22 | 22:45 | Hull City vs Middlesbrough | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 04. 01/11/22 | 22:45 | Coventry vs Blackburn | 2.41 | 3.17 | 2.87 |
| 05. 01/11/22 | 23:00 | Marseille vs Tottenham | 2.93 | 3.42 | 2.24 |
| 06. 01/11/22 | 23:00 | Sporting Lisbon vs Eintracht Frankfurt | 2.32 | 3.38 | 2.83 |
| 07. 01/11/22 | 23:00 | UD Ibiza Eivissa vs Leganes | 2.37 | 3.07 | 3.02 |
| 08. 02/11/22 | 22:45 | Birmingham vs Millwall | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 09. 02/11/22 | 22:45 | Huddersfield vs Sunderland | 2.67 | 3.16 | 2.57 |
| 10. 02/11/22 | 23:00 | Mirandes vs Tenerife | 2.85 | 3.05 | 2.55 |
| 11. 03/11/22 | 20:45 | Olympiakos vs Nantes | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 12. 03/11/22 | 20:45 | Zalgiris vs Slovan Bratislava | 3.04 | 3.39 | 2.24 |
| 13. 03/11/22 | 23:00 | Silkeborg vs Anderlecht | 2.36 | 3.40 | 2.85 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 31/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:45 | 4308 | Darya Babol vs Shahrdari Hamedan | 3.32 | 2.43 | 2.59 |
| 13:45 | 4739 | Arman Gohar Sirjan vs Mes Shahr-e Babak | 2.29 | 2.63 | 3.55 |
| 14:00 | 3261 | Kolos Kovalivka vs Veres Rivne | 2.05 | 3.10 | 3.44 |
| 14:00 | 4321 | Khosheh Talaei vs Shahrdari Astara | 1.87 | 2.83 | 4.69 |
| 14:00 | 5145 | Artsakh vs Pyunik Yerevan | 5.65 | 3.65 | 1.54 |
| 14:15 | 5994 | Shams Azar Qazvin vs Esteghlal Khuzestan | 2.17 | 2.58 | 3.99 |
| 15:30 | 1202 | Al Orubah vs AL Qaisoma | 2.32 | 2.95 | 3.35 |
| 16:00 | 1761 | Al-Arabi vs Sama AL Sarhan | 4.00 | 3.61 | 1.75 |
| 16:00 | 1828 | Al-Yarmouk vs Al Ahli Amman | 5.20 | 3.70 | 1.66 |
| 16:00 | 1943 | Crewe U23 vs Birmingham U21 | 2.82 | 4.38 | 1.94 |
| 16:00 | 3088 | FK Sloga Simin Han vs Zeljeznicar | 2.44 | 3.08 | 2.74 |
| 16:00 | 5116 | AL Hashemeya vs DAR AL Dawa | 1.69 | 3.75 | 4.80 |
| 16:00 | 5490 | Ruvu Shooting vs Mbeya City | 2.65 | 2.80 | 2.95 |
| 16:00 | 5910 | Krsko Posavje vs NK Ilirija | 3.99 | 3.51 | 1.77 |
| 17:00 | 1736 | Atalanta Youth vs Hellas Verona Youth | 1.64 | 3.98 | 4.18 |
| 17:00 | 1874 | Millwall U23 vs Cardiff City U21 | 1.93 | 4.29 | 2.87 |
| 17:00 | 3625 | Reading U21 vs Swansea U23 | 1.90 | 3.64 | 3.35 |
| 17:50 | 2605 | AL Riyadh vs AL Hazm | 5.20 | 3.40 | 1.72 |
| 18:00 | 2447 | El Ittihad Alexandria vs Talaea El Gaish | 2.25 | 2.94 | 3.44 |
| 18:30 | 5230 | Bouake FC vs Club Omnisports de Korhogo | 1.95 | 2.97 | 3.99 |
| 19:00 | 2274 | Azam vs Ihefu FC | 1.52 | 3.90 | 6.40 |
| 19:00 | 2618 | CS Mioveni vs Hermanstadt | 2.57 | 2.82 | 2.97 |
| 19:00 | 2651 | PAS Giannina vs Asteras Tripolis | 2.47 | 3.14 | 2.84 |
| 20:00 | 1787 | Arab Contractors vs Farco FC | 2.10 | 2.88 | 3.97 |
| 20:00 | 1931 | Omonia Nicosia vs Anorthosis Famagusta | 2.38 | 3.21 | 2.95 |
| 20:00 | 2048 | Puszcza Niepolomice vs Skra Czestochowa | 1.68 | 3.55 | 4.47 |
| 20:00 | 2232 | Basaksehir vs Giresunspor | 1.50 | 3.98 | 6.36 |
| 20:00 | 3926 | Sivasspor vs Antalyaspor | 2.25 | 3.28 | 3.08 |
| 20:00 | 4391 | Genclerbirligi vs Manisa BBSK | 2.63 | 3.26 | 2.42 |
| 20:00 | 5944 | Doxa Katokopia vs Aris Limassol | 3.79 | 3.49 | 1.92 |
| 20:30 | 3171 | Verona vs Roma | 4.07 | 3.52 | 1.82 |
| 21:00 | 1179 | Vasalunds IF vs Taby FK | 1.31 | 5.25 | 6.80 |
| 21:00 | 1962 | Midtjylland vs Odense | 1.55 | 4.19 | 5.18 |
| 21:00 | 3698 | Radomiak Radom vs Warta Poznan | 2.10 | 3.06 | 3.36 |
| 21:00 | 4607 | Osnabruck vs Hallescher | 1.56 | 4.06 | 5.15 |
| 21:00 | 5004 | CF Estrela vs Vilafranquense | 2.64 | 3.18 | 2.55 |
| 21:00 | 5183 | Elfsborg vs Helsingborg | 1.27 | 5.26 | 7.98 |
| 21:10 | 5060 | Norrkoping vs Djurgardens IF | 3.26 | 3.55 | 1.96 |
| 21:30 | 1275 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Tel Aviv | 3.60 | 3.41 | 1.89 |
| 22:00 | 1980 | Universitatea Cluj vs Steaua Bucuresti | 3.80 | 3.31 | 1.94 |
| 22:00 | 3553 | Pecs MFC vs Szeged | 2.11 | 3.50 | 3.25 |
| 22:00 | 5555 | Jong Ajax vs Willem II Tilburg | 2.51 | 3.49 | 2.51 |
| 22:30 | 3321 | Piacenza Calcio vs Padova | 4.19 | 3.29 | 1.90 |
| 22:45 | 1709 | Monza vs Bologna | 2.18 | 3.22 | 3.22 |
| 23:00 | 3058 | Plymouth vs Exeter | 1.98 | 3.42 | 3.52 |
| 23:00 | 3176 | Elche vs Getafe | 2.66 | 2.96 | 2.81 |
| 23:00 | 4913 | Levante vs Sporting Gijon | 2.05 | 3.27 | 3.47 |
| 23:15 | 5136 | Vitoria Guimaraes vs Famalicao | 2.08 | 3.18 | 3.58 |
| 23:30 | 2128 | Curico Unido vs Nublense | 2.36 | 3.16 | 2.77 |
| 23:30 | 3340 | Tacuary Asuncion vs Nacional Asuncion | 3.60 | 3.31 | 1.92 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TANZANIA YATWAA TAJI LA MISS VIZIWI DUNIA 2022

**Na Shufaa Lyimo**

TANZANIA imeweka rekodi kwenye Shindano la Dunia la Warembo, Watanashati na Mitindo kwa Viziwi (Miss and Mister Deaf International 2022), baada ya washiriki watatu kushinda mataji mbalimbali.

Katika shindano hilo lililofanyika jijini Dar es Salaam Jumamsoi iliyopita, Khadija Kanyama kutoka jijini Tanga, amefanikiwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kwa kushinda taji la dunia (Miss Deaf International 2022), huku Rajani Ally akishika nafasi ya pili kwa upande wa Watanashati (Mister Deaf International 2022).

Mshiriki mwingine alikuwa ni Ruso Songoro (Mister Deaf), ambaye ameshinda taji la mwanamitindo bora wa kwanza kwenye mashindano hayo.

**Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Waziri wa Jinsia, Wanawake na Watu wenye Mahitaji Maalum, Dorothy Gwajima, aliwapongeza washindi hao baada ya kupata mataji hayo na kuifanya Tanzania ing'are katika shindano hilo kimataifa.**

"Ninawapongeza washindi wote wameipa heshima nchi yetu kupitia shindano hili ambalo lilikuwa linafuatiliwa dunia nzima, ambayo imeona uwezo wa Watanzania," alisema Gwajima.

Aliwataka wazazi wawatoe watoto wao wenye mahitaji maalum kushiriki michezo kila inapotokea fursa kama hizo badala ya kuwaficha majumbani.

Kwa upande wa Miss Dunia Viziwi, Khadija alisema amefurahi kupata ushindi huo na kwamba haikuwa kazi rahisi kutokana na idadi kubwa ya washiriki aliochuana nao.

"Nitaweka msisitizo kwa serikali kuhakikisha inasapoti watu wenye ulemavu kama huu, ninaamini vipaji vipo vingi," alisema.

Shindano hilo lilishirikisha washiriki 107 kutoka nchi mbalimbali ambapo mshindi huyo wa dunia atapata ubalozi kwenda nchini Korea kuhudhuria mkutano mkuu wa viziwi duniani utakaofanyika hivi karibuni pamoja na kutembelea nchi mbalimbali.

## Kiungo Simba Queens aiona fainali CAF

INATOKA UKURASA 32

hiyo, Daniella Ngoyi, alisema kikosi chao kiko imara kuhakikisha kinawapa furaha mashabiki wa klabu ya Simba na wadau wote wa soka kutoka nchi wanazotoka.

"Mimi ninapenda kucheka, naamini wachezaji wenzangu tutapambana katika kila mechi ili baada ya dakika 90 kumalizika tuendelee kucheka pia," alisema Daniella.

Simba Queens itamaliza mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi Novemba 5, mwaka huu kwa kukabiliana na Green Buffalo kutoka Zambia kwenye Uwanja wa Grand Stade de Marrakech.

TUPO FITI...



Baadhi ya wachezaji wanaounda kikosi cha Simba Queens kilichoshuka dimbani jana dhidi ya ASFAR FC ya Morocco kwenye mechi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyoanza jana nchini humo. **PICHA: SIMBA**

## *Nabi aanika mkakati Yanga kwa Watunisia*

INATOKA UKURASA 32

kwanza ya Kombe la Shirikisho baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika katika raundi ya kwanza.

Licha ya kutinga raundi ya kwanza kwa kishindo baada ya kuitoa Zalan FC ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 10-0, Yanga ilikutana na mfupa mgumu kwa kusukumizwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1.

Yanga ililazimishwa sare nyumbani ya bao 1-1 kabla ya ugenini kukubali kipigo cha bao 1-0, hivyo kuangukia Kombe la Shirikisho, ambapo inahitaji ushindi wa jumla ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa ukubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Klabu pekee ya Tanzania ambayo inasubiri tu kupangwa droo ya hatua ya makundi Novemba 16, mwaka huu ni Simba iliyofuzu hatua hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Michezo

Jumatatu Oktoba 31, 2022

Nipashe



Klopp: Liver iko katika wakati mgumu UKURASA 29

JAMANI RAHA...




Thomas Partey akishangilia sambamba na Granit Xhaka, baada ya kuifungia Arsenal bao la nne wakati ikishinda 5-0 dhidi ya Nottingham Forest kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa jana katika Uwanja wa Emirates. Mabao mengine yalifungwa na Gabriel Martinelli, Reiss Nelson (mawili) na Martin Odegaard. **PICHA: MTANDAO**

## Kiungo Simba Queens aitabiria fainali CAF

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

KIUNGO nyota wa Simba Queens, Vivian Corazone, amesema licha ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yaliyoanza kufanyika nchini Morocco kuanzia jana kuwa magumu, anaamini timu yake itafika fainali.

Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika za mwaka huu zinazoshirikisha timu nane, zinafanyika katika miji ya Rabat na Marrakech hapa Morocco.

Simba Queens ilianza kampeni ya kuwania taji hilo jana usiku kwa kuvaana na wenyeji AS-FAR FC na itashuka tena dimbani keshokutwa, Jumatano kucheza dhidi ya Determine Girls FC ya Liberia kwenye uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan ulioko jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Corazone, alisema Simba imejiandaa vizuri na imekuja Morocco kupambana na kuonyesha haikubahatisha kuchukua taji la Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Kiungo huyo alisema kila mchezaji wa Simba Queens, anafahamu umuhimu wa michuano hii na wanataka kujitangaza kwa mawakala ambao watafika kusaka vipaji.

"Sisi tumekuja hapa kupambana, hatutaondoka mapema, tuko mpaka siku ya mwisho, tutacheza fainali, tunataka kuonyesha tunaweza," alisema Mkenya huyo ambaye alikuwa Mchezaji Bora wa CECAFA.

Naye beki wa timu

INAENDELEA UK. 31

# NABI AANIKA MKAKATI YANGA KWA WATUNISIA

### ●●● Asema mpira unabadilika na hakuna linaloshindikana, huku akiichambua Club Africain kuwa...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanya vizuri na kuendelea kuweka rekodi ya kutopoteza ('Unbeaten') kwa mechi 45, kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, sasa amekigeukia kikosi chake kuelekea mechi yao ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

Juzi, Jumamosi Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Geita Gold FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, shukrani kwa Bernard Morrison aliyeiwezesha kuvuna pointi tatu hizo muhimu kwa mkwaju wa penalti baada ya mchezaji wa Geita kudaiwa kunawa mpira ndani ya 18, ingawa ilionekana kuwa ya utata kutokana na tukio hilo kutokea nje ya eneo la hatari.

Ushindi huo unaifanya Yanga kufikisha mechi 45, bila kupoteza tangu msimu uliopita, huku ikiendelea kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara msimu huu kwa alama 20.

Lakini sasa Yanga moja kwa moja imegeukia mechi yao ya keshokutwa, Jumatano ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kurudiana nchini Tunisia Novemba 9, mwaka huu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anafahamu wapinzani wao hao na anaamini mpira unabadilika na wanajiandaa kufanyia kazi madhaifu yao na kuweka umakini kwenye safu ya ulinzi na ushambuliaji.**

Alisema kulingana na ugumu wa mechi hiyo aliwapumzisha baadhi ya wachezaji wake akiwamo mshambuliaji Fiston Mayele na beki Djuma Shabaan kwa ajili ya kujiweka fiti kwa mchezo huo ambao wanahitaji ushindi wa jumala ili kufuzu.

"Hii ni mechi ya ushindani mkubwa, Club Africain ni wazuri hawajacheza ligi muda mrefu, wamepata muda wa kupumzika kujiandaa na michuano hii, tumemaliza mechi ya ligi na sasa tunajiandaa kwa mchezo huo," alisema Nabi.

Alisema ameangalia mechi mbili za Club Africain wakicheza ugenini na nyumbani, wanavyokuwa na wanamna ya kuwazuia kutopata matokeo mazuri kwa Mkapa.

"Mpinzani wetu si rahisi na alikuja kucheza hapa nchini na timu moja ya Zanzibar, tumepata taarifa zao na kuendelea kuwafuatilia hasa safu ya ulinzi na ushambuliaji," alisema Nabi.

Alisema kufahamu kwake soka la Tunisia ni faida kubwa katika kuhakikisha wanapata matokeo mazuri wakiwa nyumbani kabla ya kwenda nchini humo kwa ajili ya mchezo wa marudiano.

Nabi alisema kitendo cha baadhi ya wachezaji kutoonekana katika michezo miwili iliyopita, ni kwamba wako tayari kwa ajili ya kupambania klabu hiyo kupata matokeo mazuri na kutoruhusu bao kwa wapinzani wao hao.

Katika hatua nyingine Club Africain imetua jana asubuhi tayari kwa mchezo huo wa amali.

Timu ya Club Africain ambayo ilianzia raundi ya kwanza ya michuano hiyo, iliitoa Kipanga FC ya Zanzibar kwa jumla ya mabao 7-0 baada ya mechi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar kumalizika kwa sare tasa.

Yanga imeangukia kucheza mechi za mchujo na timu zilizopenya raundi ya

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >